

**KUWEPO ‘KUTOKUWEPO’ KWA WAHUSIKA WA KIKE KATIKA TAWASIFU YA
MBALI NA NYUMBANI YA ADAM SHAFI (2013)**

NA

KAMWANZA ROSEMARY MUMBUA

C50/67409/2013

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA
SHAHADA
YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.**

JULAI 2015

UNGAMO

Nakiri kuwa tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kuwasilishwa kwa utahini katika chuo kikuu kingine chochote.

.....

Kamwanza Rosemary Mumbua

Tarehe

TASNIFU HII IMETOLEWA KWA IDHINI YETU KAMA WASIMAMIZI WA KAZI HII
WA CHUO KIKUU CHA NAIROBI.

.....

Dkt. Omboga Zaja

Tarehe

Dkt. Swaleh Amiri

Tarehe

TABARUKU

Kazi hii naitabaruku kwa mamangu Naom Wavinya Kamwanza na marehemu babangu Mtemi Stephen Kamwanza Nthenge. Kunizaa, kunilea, kunielimisha na kunifunza kwamba mbinu mwafaka katika kupambana na panda shuka za ulimwengu ni elimu.

Baba, ungekuwa hai ungefurahia kutimia kwa ndoto hii ambayo ilikatizwa na hali zako za kijamii na kiuchumi. Ulinifumbua, ukanihimiza niendelee nami nikakuahidi na kuapa nitatimiza. Nimetimiza ahadi yangu sasa.

SHUKRANI

Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa wema na neema zake alizonijalia muda huo wote tangu nilipoianza safari hii ya miaka miwili. Uwezo na nguvu zake haviwezi kukadiriwa. Alinilinda katika safari ya kila asubuhi na jioni kuannzia mwaka wa kwanza hadi wakati huu. Alinilinda kutokana na visa na mikasa ya barabarani pamoja na ajali ambazo hazishi kuwaua na kuwajeruhi waja kila mara. Nikupe nini Bwana wangu isipokuwa kuzidi kukuabudu na kukutegemea wewe tu. Ulinifungulia mlango wa kifedha kiasi kwamba sikuwahi kupata kikwazo chochote katika ulipaji wa karo na nauli ya kila siku kutoka Kangundo hadi Nairobi. Nakushukuru pia kwa kunijalia afya njema kwa muda huo wote kwani sikuwahi kukosa darasa hata moja tangu siku ya kwanza hadi siku ya mwisho. Nitakutumainia ee Mungu wa majeshi.

Shukrani za dhati ziwaendee wasimamizi wangu wawili, Dkt. Zaja Omboga na Dkt. Amiri Swaleh. Bila shaka uelekezi na usaidizi wenu umechangia pakubwa mno katika kukamilisha kazi hii. Mlinifumbua macho na kuninoa akili kiusomi. Mlinivumilia kwa kila hali na mkanipa mielekeo inayofaa hadi nikajitambua kiusomi. Juhudi zenu zilichangia pakubwa katika kuiboresha kazi hii. Mungu awabariki kwa uvumilivu wenu na kukubali niwasumbue wakati ufaao na wakati usiofaa. Ungwiji na usongora wenu hauwezi kuelezeza kwa ukurasa tu.

Ninatoa shukrani pia kwa wahadhiri wote katika idara ya Isimu na Lugh, Chuo Kikuu Cha Nairobi. Mafunzo ambayo wamenifundisha ndiyo yamenifanya nifike hapa nilipo sasa. Kando na mafunzo walnipatia mawaidha ya kufana na kunifumbua macho kuhusu baadhi ya vipawa ambavyo sikufikiria ningeweza kuvikuza. Wahadhiri hawa ni pamoja na; Profesa Abdul Aziz, Profesa Kineene Wa Mutiso, Profesa Kithaka Wamberia, Profesa Rayya Timammy, Profesa John

Habwe, Profesa Wamitila, Daktari Ayubu Mukhwana, Daktari Evans Mbuthia, Daktari Buregeya na Bwana Mungania. Siwezi kusahau kumshukuru Profesa Kithaka Wamberia kwa mawaidha na wosia alionipa kuhusu ukuzaji wa kipawa cha ushairi na uandishi. Mawaidha yako yatazaa matunda hivi karibuni. Mungu akubariki kwa wema wako.

Shukrani maalumu zimwendee Profesa John Habwe kwa kazi nzuri anayoifanya kama mwenyekiti wa Idara ya Kiswahili. Juhudi zako za kiofisi katika kutatua matatizo ya wanafunzi haziwezi kupuuzwa hata kidogo. Nakushukuru kwa kukubali kunifaa hata ukiwa likizoni. Mungu akubariki.

Nawashukuru wanafunzi wenzangu wote kwa usaidizi wa aina mbalimbali ulionifaa sana. Tulisaidiana kwa mengi ikiwa ni pamoja na nasaha wakati mioyo ilikuwa imetushuka kutokana na changamoto mbalimbali za kiusomi. Tulifaana la mvua na la juu. Hao ni pamoja na ; Biasha Khamis, Rita Magara, Rose Dama, Evans Makhulo, Stephen Machira, Hezekiel Gikambi, Gathara Kabiru, Otuchi Timothy na Indindi Henry ambaye alituvumilia kama Rais wa darasa.

Siwezi kusahau kuishukuru familia yangu kwa usaidizi mkubwa walionipatia wakati wote niliokuwa nikipambana na masomo haya. Hawa ni pamoja na; Mume wangu, mpenzi, Charles Noah, nakushukuru kwa kujitolea kutembea nami tangu Septemba 2013 hadi wakati wa kukamilika kwa masomo yangu. Ulijitwika jukumu la kuhakikisha kwamba chochote nilichohitaji nimekipata ili kuifanikisha ndoto hii ya familia yetu. Ulinielewa kila nilipokuwa na changamoto za kiusomi. Uliketi na kunisikiza. Ulinihimiza wakati nilipolegea na kutamauka.

Ulinipa mkono wa heri kila asubuhi bila kuchoka. Mungu mwenye rehema akumiminie baraka. Nitakutua majukumu ambayo nilikuwa nimekutwika kwa muda huo wote.

Kwenu nyinyi mabinti zangu Janet Mwikali, Jacquiline Mwende na Joan Wavinya. Sipati njia mwafaka ya kuwashukuru ila kila mmoja anahitaji shukrani maalumu. Janet, nakushukuru kwa kunihimiza na kunifunza masuala ya kiteknolojia. Ulinivumilia na kunielewa kwa kila hali hasa wakati nilipokusumbua ukiwa kazini. Kazi hii isingekamilika bila ujuzi huo ambao ulinifunza. Jacquiline, ulinielewa na ukavumilia kukosekana kwangu maishani mwako hasa katika mikutano na sherehe za wazazi shulen. Nitafidia yote hayo. Joan japo wewe ni mtoto mdogo tu, ulikubali kunikosa asubuhi niliporauka mapema na kunikosa jioni nipochelewa kufika nyumbani mapema. Nitafidia yote hayo. Abraham, mjukuu wangu, nyimbo ulizotaka nikufunze wakati huo ambapo sikuwa na muda, sasa niko radhi kutimiza ahadi yangu.

Mwisho, nitakuwa nimekosa kutomshukuru Evans Makhulo kwa kunihimiza hasa wakati changamoto za kiusomi zilinikumba. Mungu akujalie mema maishani mwako. Seth, ulinisaidia sana kuihariri kazi hii. Ujuzi wako hauwezi kupuuzwa na hata kidogo. Wahudumu wote wa maktaba ya Jomo Kenyatta nawashukuru kwa huduma zao nzuri na kujitolea kwao kuwashudumia wanafunzi pasi kuwabagua.

YALIYOMO

| | |
|---|-----|
| UNGAMO..... | ii |
| SHUKRANI..... | iv |
| YALIYOMO..... | vii |
| IKISIRI | xi |
| ORODHA YA VIFUPISHO..... | xii |
| SURA YA KWANZA | 1 |
| 1.0 Utangulizi..... | 1 |
| 1.1 Tatizo la utafiti..... | 3 |
| 1.2 Madhumuni ya utafiti..... | 5 |
| 1.3 Nadharia tete | 5 |
| 1.4 Sababu za kuchagua mada | 5 |
| 1.5 Upeo na mipaka ya utafiti..... | 6 |
| 1.6 Msingi wa nadharia..... | 7 |
| 1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada hii..... | 16 |
| 1.8 Njia za utafiti..... | 20 |
| SURA YA PILI..... | 22 |
| DHANA YA KUWEPO: UBAINISHAJI WA WAHUSIKA WANAWAKE KATIKA <i>MBALI NA NYUMBANI</i> | 22 |
| 2.0 Utangulizi..... | 22 |
| 2.1 Dhana ya kuwepo kwa wahusika wa kike | 22 |
| 2.2 Uhusika na wahusika katika fasihi..... | 23 |
| 2.2.1 Wahusika wa kihistoria | 24 |
| 2.2.2 Wahusika wa kihalisia..... | 25 |
| 2.2.3 Mhusika wa kisaikolojia | 25 |

| | |
|--|----|
| 2.3 Dhana ya mandhari | 26 |
| 2.3.1 Mandhari ya kijiografia..... | 28 |
| 2.3.2 Mandhari ya kihistoria | 29 |
| 2.3.3 Mandhari ya kidhanifu/kinjozi | 30 |
| 2.4 Muhtasari wa <i>Mbali na Nyumbani</i> | 32 |
| 2.5 Uwasilishwaji wa wahusika wa kike katika <i>Mbali na Nyumbani</i> | 43 |
| 2.5.1 Mazingira ya kijamii. | 44 |
| 2.5.1.1 Muktadha wa kinyumbani | 44 |
| 2.5.1.2 Muktadha wa safari | 51 |
| 2.5.2 Mazingira ya kiuchumi | 53 |
| 2.5.2.1 Muktadha wa kikazi | 54 |
| 2.5.2.2 Muktadha wa kibashara..... | 57 |
| 2.5.3 Mazingira ya Kielimu..... | 60 |
| 2.5.4 Mazingira ya Kiburudani | 61 |
| 2.6 Hitimisho..... | 62 |
| SURA YA TATU | 65 |
| DHANA YA “KUTOKUWEPO”: KUBAINISHA MAZINGIRA NA MIKTADHA AMBAMO WAHUSIKA WA KIKE HAWAPO KATIKA <i>MBALI NA NYUMBANI</i> | 65 |
| 3.0 Utangulizi..... | 65 |
| 3.1 Dhana ya kutokuwepo kwa wahusika wa kike | 65 |
| 3.2 Mazingira ya kijeshi..... | 66 |
| 3.2.1 Askari polisi | 67 |
| 3.2.2 Askari Jeshi | 70 |
| 3.2.3 Wapiganiaji uhuru | 71 |
| 3.3 Mazingira ya kisiasa | 75 |

| | |
|--|-----|
| 3.3.1 Vyama vya wafanyakazi na vya kisiasa..... | 76 |
| 3.3.2 Wanasiasa..... | 78 |
| 3.4 Mazingira ya kidini | 81 |
| 3.4.1 Dini ya Kiislamu | 82 |
| 3.4.2 Dini za Kienyeji | 86 |
| 3.5 Mazingira ya kuhama na uhamiaji..... | 87 |
| 3.5.1 Kuhama kutoka Zanzibar hadi Aden..... | 88 |
| 3.5.2 Kuhama kutoka Mombasa hadi Bungoma | 89 |
| 3.5.3 Kuhamia hadi Kampala | 90 |
| 3.5.4 Uhamiaji Sudan | 92 |
| 3.5.5 Kuhamia Kairo | 94 |
| 3.5.6 Kuhamia Ujerumani | 95 |
| 3.5.7 Kuhama kwa Abdalla na Shaabani..... | 96 |
| 3.6 Mazingira ya kazi..... | 96 |
| 3.6.1 Kazi katika usafiri | 96 |
| 3.6.1.1 Usafiri wa barabarani | 97 |
| 3.6.1.2 Usafiri wa majini | 98 |
| 3.6.1.3 Usafiri wa treni..... | 101 |
| 3.6.1.4 Usafiri wa ndege..... | 102 |
| 3.7 Hitimisho..... | 103 |
| SURA YA NNE..... | 104 |
| UKIMYA NA UCHELEWESHWAJI: SABABU ZA KUWEPO NA “KUTOKUWEPO” WA WAHUSIKA WA KIKE KATIKA MBALI NA NYUMBANI | 104 |
| 4.0 Utangulizi..... | 104 |
| 4.1 Uwepo wa wanawake kimajukumu: Ukimya wa kianthropolojia | 104 |

| | |
|---|------------|
| 4.2 Uwepo finyu wa wanawake: Ucheleweshwaji | 106 |
| 4.3 Utokuwepo wa wanawake: Ukimya | 107 |
| 4.4 Ukimya na ucheleweshwaji wa wanawake katika elimu..... | 108 |
| 4.5 Ukimya na Ucheleweshwaji katika kujiunga na jeshi | 117 |
| 4.6 Ukimya na Ucheleweshwaji katika shughuli za siasa..... | 121 |
| 4.7 Ukimya na ucheleweshwaji katika masuala ya dini | 127 |
| 4.8 Ubanifu wa uhamaji na uhamiaji | 132 |
| 4.9 Hitimisho..... | 133 |
| SURA YA TANO | 135 |
| HITIMISHO..... | 135 |
| 5.0 Utangulizi..... | 135 |
| 5.1 Hitimisho..... | 135 |
| 5.2 Mapendekezo | 138 |
| MAREJELEO | 139 |

IKISIRI

Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa kuchunguza uwasilishwaji wa wahusika wa kike kimajukumu katika *Mbali na Nyumbani* kwa lengo la kubainisha kuwepo na “kutokuwepo” kwao kwa uwazi katika baadhi ya miktadha na “kutokuwepo” kwao kwa uwazi katika miktadha mingine. Ubainishaji huu ulilenga kuonyesha sababu nzuri na chanya za kihistoria na kianthropolojia ambazo zinaeleza uwasilishwaji wa aina hiyo.

Tulidurusu kazi mbali mbali ambazo zimechunguza masuala ya usawiri na taswira ya wanawake ili tufahamu jinsi tathmini zimehitishwa. Nadharia ilioongoza utafiti huu ni tapo la anthropolojia ambalo ni anthropolojia ya kiutamaduni na kijamii. Nadharia hii inatambua kuchunguzwa kwa masuala ya wanawake kihistoria, uhalisi wa maisha katika jamii na michakato ya kianthropolojia ili kuwapa wanawake tathmini chanya.

Matokeo ya utafiti yalidhihirisha kwamba, sababu za kuwepo na “kutokuwepo” kwa wahusika wa kike katika mazingira na miktadha katika *Mbali na Nyumbani* ni za kihistoria na kianthropolojia bali sio za kiusawiri. Utafiti ulionyesha pia kwamba, baadhi ya tathmini hasi katika tafiti za awali zinaweza kufikiriwa upya.

ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|----------------|--|
| Dkt | Daktari |
| PSV | Public Service Vehicle |
| PAFMECA | Pan African Freedom Movement for East and Central Africa |

SURA YA KWANZA

1.0 Utangulizi.

Mbali na Nyumbani (2013) ni tawasifu ya Adam Shafi. Mbali na kazi hii, mwandishi huyu ameandika kazi nyingine za kifasihi kama vile *Kasri ya Mwinyi Fuad* (1978), *Kuli* (1979), *Vuta N'kuvute* (1999) na *Haini* (2003). Adam Shafi ni mzaliwa wa Zanzibar na ni mmoja kati ya waandishi waliokomaa katika uandishi. Swaleh (2011) anasema kwamba, tawasifu ya kwanza kabisa kuandikwa katika fasihi ya Kiswahili ni *Maisha ya Hemedi Bin Muhammed el- Mujereb-yaani Tippu Tip*. Tawasifu zilizoandikwa baadaye ni *Maisha Yangu Na Baada Ya Miaka Hamsini* (1966) ya Shaaban Robert. *Nasikia Sauti ya Mama* ya Ken Walibora (2014) ambayo inaangazia kipande kidogo halisi cha maisha yake mwenyewe ambapo maudhui mengine kama vile ya kisiasa yamejitokeza kama ilivyo katika *Mbali na Nyumbani* ya Adam Shafi.

Kwa mujibu wa Madumulla (2009:61), riwaya ya kitawasifu hujihusisha na maelezo juu ya maisha ya mwandishi mwenyewe katika kujieleza binafsi na inaweza kueleza matukio yaliyopita au hata matarajio ya mtu. Kutokana na maoni haya, *Mbali na Nyumbani* ni riwaya ya kitawasifu kwa kuwa inaakisi sifa zilizoelezwa na Madumulla. Mwandishi anaeleza matukio aliyokumbana nayo katika safari yake ya kusaka elimu. Mwandishi anasema;

‘Hekaya hii si riwaya lakini nimeandika mwandishikwa mtindo kama ule wa uandishi wa riwaya.Tofauti ya hekaya na riwaya ni kwamba,katika riwaya mara nyingi,visa matukio na taswira zake ni vya kubuni tu.Wahusika huumbwa na kuumbuliwa. Matukio mengi yaliyomo katika hekaya hii ni ya kweli na wahusika wengi ni watu halisi. Wengine bado wanaishi mpaka leo wengine wameshakufa.....’(uk vi).

Kutokana na nukuu hii, *Mbali na Nyumbani* ni riwaya ya kitawasifu inayosimulia historia halisi aliyoiandika yeye mwenyewe. Matukio mengi ni ya kweli, wahusika wengi ni halisi na wamewasilishwa katika mazingira halisi. Wamitila (2008:119) ameainisha riwaya kiwakati. Riwaya ya kihistoria ni riwaya ambayo hujikita kwenye masuala ya kihistoria kwa kuchukua dhamira, wahusika, au matukio ya kihistoria na kuyafanya kiini cha msuko wa hadithi yenewe. Riwaya ya kihistoria yaweza kuangaliwa kimaudhui na kiwakati. Wamitila ametoa mifano ya riwaya za kihistoria kama vile *Kasri ya Mwinyi Fuad, Kuli na Haini* ambazo zimeandikwa na Shafi Adam Shafi. Kazi hizi zinasimulia matukio ya kihistoria katika nchi ya Zanzibar kuanzia utawala wa mamwinyi hadi mapinduzi ya mwaka 1964. *Mbali na Nyumbani* inaakisi sifa za riwaya ya kihistoria kwa kuwa matukio yanayosimuliwa ni ya kihistoria. Kwingineko Wamitila (k.h.j) ameeleza kuwa riwaya ya kihalisa ni riwaya inayoonyesha mwelekeo mkubwa wa kuibua athari za hali halisi kwa kusawiri wahusika kwa uchangamano na undani huku wakikitwa kwenye matabaka mahususi ya kijamii. Anazidi kusema kuwa wahusika huwa na muundo mpana wa kijamii na huingiliana na wahusika wengine zaidi. Kati ya mifano aliyotoa ni *Kasri ya Mwinyi Fuad*, iliyoandikwa na Adam Shafi Adam. *Mbali na Nyumbani* ni kazi inayoakisi sifa za riwaya ya kihalisa kwa sababu mwandishi amewawasilisha wahusika halisi ambao wanaibua uhalisi wa kihistoria. Vile vile wahusika wamekitwa katika matabaka mahususi ya kijamii huku wakionyesha mwingiliano mpana kati yao. Kutokana na uelewa kuhusu kazi za mwanzo za Adam Shafi, tunaweza kudai kuwa ni mwandishi anayeandikia zaidi masuala halisi ya kihistoria.

Njogu (2014) katika ‘*Creative - Non Fiction In Kiswahili Writing: Reading Mbali na Nyumbani*, anasema kwamba, japokuwa Kiswahili kina kazi nyingi za kifasihi katika tanzu za riwaya, tamthilia na ushairi, pamekuwa na upungufu wa kazi za kitawasifu katika fasihi hii. Ni kutokana

na upungufu huu ndipo tumegundua pana uhaba wa mijadala kuhusu uhusika na wahusika katika kazi za kitawasifu. Hali hii imetichochea katika kutafiti watusika wa kike katika *Mbali na Nyumbani*. Utanza wa tawasifu kwa kipindi kirefu umehusishwa na mwandishi kueleza maisha yake mwenyewe. Waandishi kama Shaaban Robert katika *Maisha Yangu Na Baada ya Miaka Hamsini* amesimulia maisha yake kuanzia utotoni hadi wakati wa kuoa katika sehemu ya kwanza, kisha anaelezea maisha yake kazini na sehemu ya mwisho anaelezea maisha ya baadaye. *Mbali na Nyumbani* ni tawasifu ilioandikwa kwa kuhusisha wahusika wengi na maudhui mbali mbali. Hapajakuwepo na kazi nyingine ya kitawasifu ilioandikwa kwa mtindo huu wa riwaya. Huu ni uandishi mpya wa tawasifu katika fasihi ya Kiswahili. Uandishi huu mpya umetichochea katika uchunguzi mpya wa wahusika wa kike katika kazi hii. Vile vile, usawiri wa wahusika katika *Mbali na Nyumbani* si wa kiubunifu. Wahusika ni halisi na wamesawiriwa katika miktadha halisi ya maisha. Hali hii imechochea utafiti wa wahusika halisi katika *Mbali na Nyumbani* ili kuonyesha uchanya wao kimiktadha na kimajukumu. Tawasifu ya *Mbali na Nyumbani* imeteuliwa kwa kuwa ina uwezo mkubwa katika kuonyesha uhalisi mpya unaochochea kufikiriwa upya kwa tathmini zilizohitimisha kwa kukisia au uchukulizi tu. Usawiri wa wanawake katika riwaya, tamthilia na ushairi umeshughulikiwa na watafiti ambao baadhi wamehitimisha kwa tathmini hasi bila kuzingatia masuala kama historia ya wanawake na mabadiliko yao pamoja na asasi na mifumo ya utamaduni katika jamii za Kiafrika, jambo ambalo utafiti huu unakusudia kounyesha katika *Mbali na Nyumbani*.

1.1 Tatizo la utafiti.

Masuala mengi kuwahuwanne wanawake yameshughulikiwa na watafiti wengi katika fasihi na hasa tanzu za riwaya, tamthilia na ushairi. Kuanzia miaka ya themanini watafiti ambao wamechunguza

usawiri wa wanawake katika kazi za kifasihi wameonyesha usawiri hasi wa wanawake kuliko usawiri chanya. Tathmini nyingi zimehitimisha kwa kuonyesha wanawake wamenyimwa hadhi, wameonewa au kudhulumiwa. Utafiti huu unachunguza usawiri wa wahusika wanawake katika *Mbali na Nyumbani* kwa kujikita katika misingi ya kubainisha kuwepo, “kutokuwepo” kwao kwa uwazi katika baadhi ya miktadha na “kutokuwepo” kwao kwa uwazi katika miktadha mingine. Utafiti huu unadai tangu mwanzo kwamba kuna sababu nzuri na chanya za kihistoria, kianthropolojia na kiuandishi zinazoeleza kusawiriwa kwa wahusika wanawake kwa njia hizi. Vile vile utafiti huu unadhamiria kutumia nadharia ambazo hazitachochea mahitimisho ya kihisia na ya kiuchukulizi kuwa, wanawake wananyimwa hadhi, wanaonewa au wanadhulumiwa, bali nadharia zitaeleza ni kwa nini uhalisi wa maisha ya wanawake uko vile ulivyo. Hii ni kwa sababu wanawake katika *Mbali na Nyumbani* si viumbe wa kubuniwa, ni watu halisi katika hali na miktadha halisi ya maisha. Uchunguzi wa usawiri wa wahusika wanawake unaokita katika misingi ya kihistoria, uhalisi wa maisha katika jamii ya mwandishi na uelewa wa michakato ya kianthropolojia inayoshawishi maisha hayo, ni mambo yanayotupa fursa ya usomaji mbadala wa jinsi wahusika wanawake walivyosawiriwa kiubunifu. Ukweli huu unatuchochea kudai, kuna uwezekano kwamba tathmini zilizohitimisha kwamba wanawake wamesawiriwa kwa njia hasi, kwa kiasi ni za kukisia. Kila jamii ina tamaduni na taasisi zake ambazo kabla ya athari za ukoloni zilienziwa, kukubaliwa na kuheshimiwa na wanajamii, na hii ina maana kwamba usawiri wa wanawake katika *Mbali na Nyumbani* unaakisi ukweli zaidi kuliko wahusika wanawake wa kiubunifu. Fauka ya hayo, utafiti huu kwa kujikita katika nadharia za Kiafrika na hasa masuala ya kiathropolojia, kutafiti suala la kuwepo na “kutokuwepo” wahusika wanawake katika *Mbali na Nyumbani*, ulinuia kuonyesha kwamba tathmini hasi kama zile tumetaja awali zinaweza kufikiriwa upya.

1.2 Madhumuni ya utafiti

Utafiti huu ulikuwa na madhumuni yafuatayo;

- a) Kubainisha uwasilishwaji wa wahusika wa kike kimajukumu katika mazingira na miktadha mbali mbali katika *Mbali na Nyumbani*.
- b) Kubainisha mazingira na miktadha ambamo wahusika wa kike hawajawasilishwa katika *Mbali na Nyumbani*.
- c) Kuonyesha sababu za kuwepo na “kutokuwepo” kwa wahusika wa kike katika *Mbali na Nyumbani*.

1.3 Nadharia tete

Utafiti huu uliongozwa na nadharia tete zifuatazo;

- a) Wahusika wa kike wamewasilishwa kimajukumu katika mazingira ya kijamii, kiuchumi, kielimu, kiburudani na usafari.
- b) Mazingira ambamo wahusika wa kike hawajawasilishwa katika *Mbali na Nyumbani* ni ya kijeshi, kisiasa na miktadha fulani ya kidini.
- c) Sababu za kuwepo na “kutokuwepo” kwa wahusika wa kike katika *Mbali na Nyumbani* ni za kianthropolojia na kihistoria.

1.4 Sababu za kuchagua mada.

Suala la wanawake limeandikiwa na waandishi wengi na kutafitiwa na watafiti wengi. Waandishi huandika wakiwa na dhamira tofauti tofauti kuhusu masuala ya wanawake katika riwaya, tamthilia na ushairi. Sababu yetu ya kwanza iliyochochea utafiti huu ni mtindo mpya katika tawasifu ya *Mbali na Nyumbani* ambao umetupa fursa ya kudadisi upya usawiri wa

wanawake. Pili, kazi hii imetupa fursa ya usomaji mbadala wa jinsi wahusika wa kike walivyosawiriwa kiubunifu. Tatu, tumepata fursa ya kudadisi kauli nyingi za awali kuhusiana na usawiri hasi wa wanawake katika kazi za kifasihi. Nne, hakuna ushahidi wa mtafiti yejote ambaye ametafiti usawiri wa wanawake katika *Mbali na Nyumbani*, kwa hivyo kazi hii itakuwa mchango wa kwanza. Tano, nadharia ya anthropolojia tuliyotumia kutafiti usawiri wa wanawake katika *Mbali na Nyumbani*, haijawahi kutumiwa kutafiti masuala ya wanawake katika fasihi ya Kiswahili, hivyo tunakusudia kuziba pengo hili la kiusomi. Mwisho, hakuna utafiti wa awali juu mada ya kuwepo “kutokuwepo” kwa wahusika wa kike katika fasihi ya Kiswahili, kazi hii itakuwa mchango wa kwanza kwa mada hii.

1.5 Upeo na mipaka ya utafiti.

Utafiti huu kimsingi umechunguza uwasilishwaji wa wahusika wa kike katika *Mbali na Nyumbani*, kwa lengo la kubainisha kuwepo “kutokuwepo” kwao katika mazingira fulani. Ubainishaji huu unalenga kuonyesha sababu za mwandishi kuwawasilisha kwa uwazi au kwa ufinyu katika miktadha fulani na sababu za kutowawasilisha katika miktadha mingine. Japo utafiti huu haukujishughulisha na usawiri wa wahusika wanaume, miktadha wanamopatikana pamoja na majukumu yao vilichangia katika kujadili majukumu ya wanawake. Hii ni kwa sababu, ufanisi wa wanawake au “kutokuwepo” kwake kunafungamana kwa kila hali na kuwepo kwa wanaume. Mazingira na miktadha ambayo wanawake wamehusishwa imechunguzwa ili kujadili kama mwandishi alikusudia kuwanyima hadhi, kuwaonea, kuwadhulumu au kuwatenga. Majukumu ya wanawake yamechunguzwa na kuchanganuliwa kihistoria na kianthropolojia ili kufungamanisha masuala hayo na ukweli wa jamii. Jambo linapochunguzwa kihistoria, madai yalithibitishwa na hivyo tathmini za kihisia na zenye uchukulizi fulani ziliepukwa. Ingawa

kimsingi wahusika ni kipengele cha fani, utafiti huu haukujishughulisha na uchambuzi wa fani katika kazi teule.

1.6 Msingi wa nadharia.

Nadharia tuliyotumia katika utafiti huu ni ya anthropolojia. Anthropolojia ni taaluma inayotafiti tabia na mienendo ya watu kwa lengo la kupata ushahidi wa wazi kuhusu suala linalotafitiwa. Nadharia ya anthropolojia inachunguza na kujibu maswali ya kijamii kwa misingi ya kihistoria na kianthropolojia. Uchunguzi wa masuala kihistoria na kianthropolojia una uwezo wa kuonyesha ukweli na uhalisia wa mambo. Ukweli na uhalisi wa mambo huepusha hisia na chukulizi katika kutathmini masuala ya kijamii. Kimsingi, wanaanthropolojia huchanganua vipengele vya utamaduni ili kuchunguza mifumo pamoja na taratibu zilizomo kwa nia ya kupata ushahidi kuhusu masuala yanayotafitiwa. Lengo la utafiti wa kianthropolojia ni kupata utumikizi jumla kama vile kanuni za kidini, sheria za ndoa na mgao wa majukumu ya wanajamii kama ziliivyojitokeza katika jamii kihistoria. Nadharia ya anthropolojia ina historia ndefu. Waasisi wa nadharia ya anthropolojia ni wenyeji wa mataifa ya Ulaya na Amerika. Baadhi ya waasisi walioiwekea misingi nadharia hii ni Edward B. Taylor aliyeishi kati ya miaka ya 1832-1917 na mwenzake Lewis Henry Taylor aliyeishi kati ya miaka ya 1818-1889. Wanaanthropolojia hawa walianzisha juhudzi za kutafuta nadharia za kutafiti masuala ya kijamii-kianthropolojia. Walijitokeza na mitazamo ya kitamaduni iliyodai kwamba, tamaduni katika jamii hukua sambamba kuititia hatua fulani za kimsingi na kimaendeleo. Walidai pia kuwa utamaduni ulienea kwa njia ya msambao kutokana na maingiliano ya watu. Hata hivyo, nadharia walizojitokeza nazo zilikumbwa na chanagamoto nyingi na ambazo wanaanthropolojia waliofuata walijaribu kuboresha.

Kazi inayochangia pakubwa katika kuiwekea msingi nadharia ya anthropolojia ni ile ilioandikwa na Franz Boas, mwaka wa 1896, *The Limitation of the Comparative Methodologies of Anthropology*. Boas aliishi kati ya miaka ya 1858-1942. Katika kazi yake, alipinga vikali madai ya Taylor na kundi lake na kusema kwamba nadharia za wanaanthropolojia wa awali kama Taylor na kundi lake, zilishindwa kuonyesha tofauti kati ya utamaduni mmoja na mwingine kwa kuwa jamii zilikuwa katika hatua tofauti kimaendeleo. Pili, nadharia hizo zilishindwa kueleza sababu zilizochangia kutoweka kwa tamaduni fulani na kurudi nyuma kwa tamaduni nyingine. Tatu, baadhi ya watu katika tamaduni fulani walifikia hatua ya ustaarabu bila kupitia hatua za ushenzi wa chini na ushenzi wa kati, madai ambayo Taylor na kundi lake walikuwa wamesisitiza kwa kuchukulia kwamba, tamaduni za ulimwengu zilikua na kubadilika kwa hatua sawa. Nne, wanaanthropolojia wa awali walikosa data ya kutosha kuchanganulia masuala yaliyotafitiwa. Tano, walitathmini masuala kwa uchukulizi kwamba, sheria na kanuni zilizotawala tamaduni za ulimwengu zilikuwa za kijumla. Boas alidai kuwa tamaduni za ulimwengu ni tofauti na changamano kwa hivyo, jamii hazipaswi kutathminiwa kwa ujumla na kwa njia sawa au bia.

Jamii zikitathminiwa kwa ujumla, mahitimisho hufanywa kwa hisia na chukulizi fulani. Vinginevyo, Boas alitaka utafiti wa kianthropolojia uepuke tathmini za kihisia na kiuchukulizi. Alipendekeza wanaanthropolojia watathmini masuala ya kitamaduni kwa upekee na kwa kuzingatia kwamba, tamaduni za jamii hufanana na kutofautiana. Alisisitiza ukusanyaji wa data ya kutosha katika ujumlishaji wa tathmini zinazotolewa.

Kulingana na Cara (1976), nadharia ya anthropolojia ina matapo manne yakiwemo; anthropolojia ya kitamaduni, akiolojia, anthropolojia ya vilugha na anthropolojia ya mazingira. Utafiti huu

unajihuisha na anthropolojia ya kiutamaduni ambayo baadhi ya wanaanthropolojia huirejelea kama anthropolojia ya kijamii. Tapo hili la anthropolojia lina mitazamo ifuatayo; mtazamo wa kijamii na kiutamaduni, mtazamo wa upekee wa kihistoria, mtazamo wa kimuundo na mtazamo wa kiuchumi na kisiasa. Mitazamo hii ina mahusiano na masuala ya kimsingi ya utafiti kama tutakavyoeleza kwa kifupi.

i) Mtazamo wa Kijamii au Kiutamaduni.

Mtazamo huu unatambua kwamba, kuna tamaduni nyingi za kilimwengu na tamaduni hizo ni changamano. Kwa misingi hii, utafiti wa kianthropolojia utahitaji kuzingatia hoja hii. Mahusiano kati ya mtazamo wa kiutamaduni na masuala ya kimsingi ya utafiti huu ni kwamba, utamaduni wa jamii ya mwandishi ni changamano, unafanana na kutofautiana na tamaduni nyingine za ulimwengu na kwa hivyo, kuwepo na “kutokuwepo” kwa wahusika wa kike kumechunguzwa kwa upekee wa utamaduni wa mwandishi. Majukumu, tabia, mienendo na mitazamo ya wahusika wa kike katika *Mbali na Nyumbani* vimechunguzwa kwa misingi ya mila na desturi pamoja na mipangilio na taratibu za jamii ya mwandishi.

ii) Mtazamo wa upekee wa Kihistoria.

Mtazamo wa upekee wa kihistoria una madai yake katika kuchunguza ukweli wa mambo kihistoria na kusitiza matokeo yake kuliko uchunguzi wa kisayansi. Kulingana na White (1963:61) data ya kutosha itahitajika kutoa habari za kutosha kuchanganulia masuala kihistoria. Mahusiano kati ya mtazamo wa upekee wa kihistoria na masuala ya kimsingi ya utafiti ni kwamba, masuala kama vile majukumu ya wanawake katika *Mbali na Nyumbani* yamechunguzwa kihistoria na kwa upekee wa jamii ya mwandishi ili tathmini zitakazotolewa

ziepuke hisia na chukulizi fulani. Jambo linapochunguzwa kihistoria, ukweli huweza kujibainisha.

iii) Mtazamo wa Kimuundo.

Muundo wa jamii ni kioo cha jamii husika. Kulingana na White (k.h.j) taasisi za kijamii zapaswa kuchunguzwa kwa uchanya kwa kuwa ni kioo cha jamii. Uhusiano kati ya mtazamo wa kimuundo na masuala ya kimsingi ya utafiti ni kwamba, taasisi za kijamii zinazojitokeza katika *Mbali na Nyumbani* kama vile za kielimu, kisiasa na kidini zimechunguzwa kwa uchanya kwa kuwa zinamulika jinsi jamii ya mwandishi ilivyokuwa kipindi hicho cha kihistoria.

iv) Mtazamo wa Kiuchumi na Kisiasa.

Kila jamii ina mifumo yake ya kiuchumi na kisiasa. Mifumo hiyo inabadilika kwa mpito wa wakati. Mabadiliko yanapotokea huathiri mifumo yote ya kijamii. Miller (1990) anaeleza kwamba ni vigumu kutenga utamaduni na athari zinazotokana na misukumo kama vile ukoloni na ubeberu. Mabadiliko ya mifumo hii huangaliwa kihistoria ili kuonyesha hali ilivyokuwa na ilivyo sasa. Mahusiano kati ya mtazamo wa kiuchumi na kisiasa na masuala ya kimsingi ya utafiti ni kwamba, kuhusishwa au kutohusishwa kwa wanawake katika harakati za kijamii katika *Mbali na Nyumbani* ni uhalisi wa maisha yao yalivyokuwa katika harakati hizo, harakati ambazo zimebadilika kulingana na mpito wa wakati. Majukumu ya wanawake katika mazingira ya kijeshi, kiuchumi, kisiasa, kikazi na kidini yameelezwa kwa kuzingatia jinsi yalivyokuwa na athari zilizotokea kihistoria.

Wanaanthropolojia wanadai kuwa, katika utafiti wa kianthropolojia, kuna miegemeo miwili mikuu; muegemeo wa kiutamaduni na kijamii na ule wa kitaashira au kiishara. Wanaanthropolojia wa kiutamaduni na wa kijamii wanajihuisha na utambulishaji wa vipengele vya utamaduni katika mifumo ya kiuchumi, kisiasa, kidini miongoni mwa vingine. Wanavutiwa na uchunguzi kuhusu mpangilio na utaratibu katika mifumo ya kiuchumi, kidini na kisiasa ili kubainisha ilivyokuwa na ilivyo sasa pamoja na mabadiliko yaliyoipitikia jamii husika. Mahusiano kati ya muegemeo huu na masuala ya kimsingi ya utafiti ni kwamba, sababu za kuwepo na “kutokuwepo” kwa wahusika wa kike katika *Mbali na Nyumbani* kunaakisi uhalisi wa maisha yao katika kipindi hicho cha kihistoria cha mwandishi. Uwasilishwaji wa wanawake katika miktadha fulani na utowasilishwaji wao katika miktadha mingine ni zao la mila na desturi za kijamii. Mipangilio na taratibu za jamii ya mwandishi katika mifumo ya kisiasa, kidini, kielimu inaeleza kwa nini wanawake wamewasilishwa jinsi walivyo katika kazi hii. Majukumu ya wanawake katika jamii ya mwandishi kihistoria, hayalengi kuwadhalilisha, kuwadhulumu au kuwanyima hadhi bali ni uhalisia wa maisha yao kianthropolojia na kihistoria. Muegemeo wa kitaashira au kiishara huhusisha kuchunguza maana ya utamaduni. Kwa mujibu wa Kroeber (1952) utamaduni kimsingi hurejelea sanaa, itikadi, tabia, mitazamo, kaida, malengo na maadili yanayotambulisha asasi za kijamii. Vipengele hivi vya utamaduni huchunguzwa kimaana na kuhusishwa na masuala ya kielimu, kisiasa na kidini kimuktadha. Watafiti wa kundi hili pia huhusisha mbinu zingine mbadala katika utafiti wao kama maelezo ya kisayansi kuhusu mbari, mila, utamaduni na historia awali ya jamii husika. Uhusiano uliopo kati ya muegemeo wa kitaashira na masuala ya kimsingi ya utafiti ni kwamba, tabia za wahusika, itikadi zao za kidini, mitazamo yao kuhusu masuala fulani katika *Mbali na Nyumbani* ni zao la utamaduni kihistoria.

Nadharia ya anthropolojia ya kiutamaduni au kijamii ina madai mbali mbali yakiwemo;

- a) Utoaji wa ushahidi wa kutosha kuhusu maendeleo ya utamaduni wa jamii kwa kukusanya data inayotosha kuchanganuliwa na kujumlisha suala linalotafitiwa.
- b) Utoaji wa maelezo yasiyoegemea uchukulizi au hisia zozote.
- c) Kuchunguza kwa upekee na kimuktadha masuala ya kijamii kama yanavyojitokeza, kwa uelewa kwamba, tamaduni za ulimwengu ni tofauti na changamano.
- d) Kuzingatia ukweli halisi na kutilia shaka pamoja na kupuuza baadhi ya maelezo ya Kisayansi.
- e) Kuchunguza kwa njia chanya taasisi na asasi za kijamii kwa misingi kwamba, mila na desturi za kijamii ni kioo cha kumulika muundo wa ndani wa jamii husika.
- f) Kueleza tabia za watu kwa kutambua sheria zinazofaa kuwepo katika jamii ili kufahamu kwa nini watu wana tabia na mienendo fulani katika jamii.
- g) Kuchunguza mabadiliko ya kijamii, kiuchumi, kisiasa, kielimu na kidini kihistoria ili kuonyesha ukweli na uhalisia wa masuala yanayotafitiwa.

Katika utafiti huu, vipengele vilivyotufaa kuchunguza kuwepo “kutokuwepo” kwa wahusika wa kike katika *Mbali na Nyumbani* ni: ucheleweshwaji na ukimya kwa mujibu wa (Miller 1990), kama inavyodai nadharia ya anthropolojia. Miller (k.h.j), katika *Theories of Africans*, anachunguza sauti na ukimya wa wanawake katika uandishi wa fasihi nchini Senegal kwa kutumia nadharia ya anthropolojia. Katika kazi yake anasema kwamba, wanawake kutohusishwa katika uandishi wa fasihi au kunyimwa kwao nafasi ya kuandika kazi za kifasihi kunafaa kuelezwa kwa kuzingatia mambo mawili. Kwanza, ukimya wa wanawake katika jamii kutegemea jamii yenye kama unavyoelezwa kianthropolojia na pili kunyamazishwa kwa

mwanamke na masuala ya kijinsia kama yanavyojitokeza katika kazi zilizoandikwa na waandishi wa kiume. Kwa upande mwingine, Miller (k.h.j) anaeleza kuwa, kutokuwepo waandishi wanawake wa Kiafrika nchini Senegal hadi kufikia mwaka 1976, kunatokana na kucheleweshwa kuibuka kwao katika uandishi. Miller anaeleza kwamba, uwanja wa fasihi ulimilikiwa na waandishi wa kiume kuanzia mwaka wa 1920 hadi kufikia wakati wa kabla na baada ya ukoloni. Pili, waandishi wa kiume ndio waliandikia masuala ya wanawake. Kwa mujibu wa Miller, kazi ya kwanza inayozungumzia suala la wanawake na iliyandoikwa na mwanamke kwa lugha ya Kifaransa ni “*So Long A Letter*” iliyandoikwa na *Mariama Ba*, mwaka wa 1979. Miller anaonya kwamba, kabla ya kudai kwamba wanawake walikuwa wametengwa au kuzuiliwa wasiandike (kama watafiti wengine wanavyodai), ni muhimu masuala mengine yatathminiwe kama vile kutokuwepo kwa maandishi yaliyoandikwa na wanawake na kwa nini walianza kuandika. Miller anajitokeza na tathmini kwamba, ukimya wa wanawake katika maandishi ya kifasihi ulichangiwa zaidi na wanawake kutojua kusoma na kuandika, ambayo ndio njia kuu ya kukuza na kuijiendeleza kwao katika jamii. Miller anatumia nadharia ya anthropolojia, kumulika historia ya wanawake wa Senegal kuanzia wakati kabla ya ukoloni, jinsi walivyokua hadi mwaka wa 1976 ambapo kazi zilizoandikwa na wanawake zilichapishwa. Aminata Sow Fall aliandika *Le Revenant* (tawasifu za wanawake ambazo hazizungumziwi). Hata hivyo, kazi hii ya kwanza haikuwalhusu wanawake. Kwa kuchunguza kazi ya *So Long A letter*, Miller ameeleza kwa nini wanawake walianza kuandika. Miller (1990:250-251) anasema kwamba, watafiti wachache ambao wamehakiki ukimya wa wanawake katika uandishi wa fasihi nchini Senegal, (ukimya ambao ulichukua nusu karne), wametoa hukumu hasi kwamba wanawake walitengwa katika taasisi za kielimu. Miller anasema kwamba, tathmini kama hizo zinatolewa kwa kuegemea nadharia za kifeministi ambazo zinapuza masuala ya kianthropolojia. Miller anasema kwamba,

elimu kwa wanawake ilicheleweshwa kutokana na itikadi na mifumo pamoja na taasisi mbali mbali katika jamii. Kwa hivyo, ucheleweshwaji wa wanawake katika mifumo na taasisi za kijamii kama vile elimu, siasa, dini na jeshi unapaswa kuchangia pakubwa katika uchanganuzi wa masuala ya wanawake barani Afrika. Miller anapendekeza masuala kuwalusu wanawawake yachunguzwe kianthropolojia, kihistoria pamoja na taasisi na mifumo ili kuepuka tathmini hasi kuwalusu wanawake.

Vinginevyo, Miller (1990:250), anasema kuwa, tunapochunguza masuala ya kifasihi katika miktadha ya Kiafrika tukitumia nadharia za Kimagharibi, ni lazima kila kitu kifikiriwe upya. Sisi tunasema kwamba, mifumo ya Kiafrika iliyokuwepo kabla ya ukoloni haipaswi kulaumiwa na kugandamizwa kwa kuegemezwa kwenye mitazamo ya kigeni. Kwa misingi hii, pana uhusiano mkubwa kati ya anachokisema Miller na masuala ya kimsingi ya utafiti kwamba, matukio katika *Mbali na Nyumbani* yanajikita katika jamii ya Kiafrika kwa hivyo, ukimya wa wanawake pamoja na ucheleweshwaji wao ni chanya bali sio hasi kama inavyoweza kutathminiwa. Kwa hivyo, uchunguzi wa ukimya umechaniganuliwa kulingana na taratibu za jamii husika kama vile fasihi na elimu. Katika muktadha wa Kiafrika, mtafiti hana budi kuonyesha mpaka kati ya suala linalotafitiwa na mifumo ya kisiasa, kiuchumi, kijamii, kielimu, kitamaduni na kidini. Utafiti kuhusu ukimya unapaswa kuchunguzwa kwa kuzingatia masuala kihistoria na kianthropolojia katika jamii husika. Kulingana na Miller, kuna ukimya kama unavyoelezwa kianthropolojia, ukimya kutokana na kazi kuhusu wanawake ambazo zimeandikwa na wanaume na ukimya kama mkakati. Kutokana na ukweli huu, ukimya wapaswa kuchunguzwa kimuktadha. Ukimya kianthropololojia waweza kuhusishwa na jinsia au tabaka fulani kwa hivyo katika kuutathmini haipaswi kupuuza taratibu za jamii husika.Ukimya kama ishara ya dhuluma au mamlaka

hutegemea usemi. Ukimya unaweza kutangulia usemi au kufuata usemi kulingana na matukio au mambo yanayosemwa. Kwa misingi hii, kama anavyooleza Miller, ukimya waweza kuwa mkakati wa kuficha mamlaka ili kukuaminisha kuwa mamlaka yako mahali pengine. Hivyo badala ya kudai ukimya ni kunyimwa mamlaka ni muhimu kuzingatia hoja kwamba, uhusiano wa wenye mamlaka na wasio na mamlaka ni wa kutegemeana. Kwa kuwa utafiti wetu ni wa kianthropolojia, vipengele vya ukimya na ucheleweshwaji kwa mujibu wa Miller (1990) vinatufaa kuchunguza sababu za kuwepo na “kutokuwepo” kwa wahusika wa kike katika *Mbali na Nyumbani*.

Robbins (2000-220) anaelezea kuwa, katika bunilizi za fasihi, usomaji na uhakiki wa masuala ya wanawake unaweza kuwa mgumu na hasa kuhusiana na suala la kutathmini usawiri wa wanawake. Ugumu huu unatokana na ukweli kwamba, tathmini hutegemea uwasilishwaji na uhusishwaji wa wanawake wenyewe. Anaeleza kuwa, ni sawa kuwatathmini wanawake kulingana na uwasilishwaji na uhusishwaji wao lakini pana mambo mengi zaidi ya kuelezwa kuhusu uwasilishwaji wa wanaume pia hasa kwa kueleza kwa nini wamewalishwa jinsi walivyo katika kazi husika. “Kutokuwepo” kwa wahusika wanawake katika kazi inayowahusisha wanaume, kuwepo na wahusika wa kike wenye majukumu ya madogo, “kutokuwepo” kwa usawa wa kijinsia katika masuala ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kitamaduni hakuna maana kwamba wanawake wametengwa au wamebaguliwa. Kulingana na Robbins (k.h.j) tunajifunza mengi kuhusu jinsia ya kiume na ya kike katika kipindi maalumu cha kihistoria kwa kuwa hivyo ndivyo hadithi yenye ilivyowasilishwa. Na kama anavyooleza kutowasilishwa kwa uwazi kwa wanawake katika kazi za kifasihi, hakuna maana kwamba wanawake hawajahusika. Sisi tunasema kwamba, kuwepo au “kutokuwepo” kwa wahusika wa kike katika *Mbali na Nyumbani*

hakuna maana kwamba, wanawake hawajashirikishwa kwa kuwa mwandishi amewawasilisha kihalisa kwani kazi hii sio kazi ya kiubunifu.

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada hii

Masuala kuhusu usawiri wa wanawake katika bunilizi ya Kiswahili yameshughulikiwa kwa mapana na kwa hali mbalimbali. Masuala haya yameshughulikiwa kwa misingi ya taswira ya mwanamke, majukumu na uhalisia wa kiusawiri. Masuala haya yameshughulikiwa zaidi katika tanzu za riwaya, tamthilia na ushairi. Watafiti mbali mbali wametumia nadharia tofauti tofauti kuchunguza maswala ya wanawake. Udurusu wetu umekita katika tafiti zilizofanywa kuanzia miaka ya themanini.

Mbughuni (1982) anatafiti usawiri chanya wa mwanamke katika riwaya bunifu za Kiswahili anasema kuwa, mwanamke ni mhimili mkuu katika asasi ya ndoa. Jambo hili linajitokeza katika majukumu yake ya uzazi na ulezi. Kazi ya Mbughuni imekuwa na manufaa katika utafiti huu kwa kuwa, tumeweza kufahamu majukumu mbali mbali ya mwanamke katika asasi ya ndoa, maoni yatakayotuwezesha kutathmini kuwepo na “kutokuwepo” kwa wahusika wa kike katika *Mbali na Nyumbani*. Hata hivyo, utafiti wa Mbughuni ni tofauti na wetu kwa kuwa yeye ametafiti riwaya za kiubunifu ilhali sisi tunachunguza riwaya ya kitawasifu.

Sirucha (1986) katika tasnifu yake, ‘*Hadhi na Hali ya mwanamke’ katika riwaya za S.A Mohammed*’, anadai kuwa, mwanamke hajapewa nafasi yoyote ya kuonyesha uwezo wake kutokana na misingi ya kitamaduni, kisiasa na kiuchumi. Utafiti wa Sirucha umetuwezesha kufahamu taasisi na mifumo ya kijamii inayodaiwa kumnyima mwanamke nafasi ya kuonyesha

uwezo wake. Madai ya Sirucha kwamba, wanawake wanajiingiza katika ukahaba ili watosheleze mahitaji yanatupa nafasi ya kudadisi upya tabia za wahusika wa kike katika *Mbali na Nyumbani* ambao wamewasilishwa kama makahaba ili tujadili sababu zinazochangia uwasilishwaji wa aina hiyo kwa kutumia nadharia ya anthropolojia. Tofauti kati ya utafiti huu na wa Sirucha ni kwamba, ye ye ametumia nadharia ya kifeministi na sisi tutatumia nadharia ya anthropolojia. Zaidi ya hayo, Sirucha ametafiti riwaya za kiubunifu na utafiti huu unachunguza riwaya ya kitawasifu.

Lugano (1989) ametafiti usawiri wa mwanamke kisiasa, kiuchumi na kielimu katika riwaya za Kiswahili zikiwemo, Rosa Mistika (1971), Kichwa Maji (1975), Gamba la Nyoka (1979) zilizoandikwa miaka ya sabini. Ametumia nadharia ya Umarx na kuhitimisha utafiti wake kwa kusema kuwa, mwanamke ni kiumbe duni, mtegemezi wa mwanamume, chombo cha kumstarehesha mwanamume na chanzo cha maovu yote. Utafiti wa Lugano umetuwezesha kufahamu majukumu ya wanawake katika masuala na shughuli za kisiasa, kiuchumi na kielimu. Tumeweza pia kupata baadhi ya kauli na tathmini ambazo zinaweza kuchunguzwa na kufikiriwa upya kwa kutumia nadharia ya anthropolojia ambayo utafiti huu unatumia.

Moser (1993) katika *Gender Planning And Development* amechunguza mgao wa kazi za kinyumbani kijinsia. Moser amesema kwamba majukumu ya uzazi hujumuisha kuzaa na kulea watoto pamoja na shughuli nyingine ambazo ni za lazima katika kukimu na kuendeleza familia. Majukumu haya huhuishwa na wanawake. Kwa mujibu wa Moser wanawake huhuishwa na kazi zinazohitaji muda mrefu na uvumilivu sababu mara nyingi ni za kurudiarudia tu kama vile kuchota maji, kutafuta kuni, kulea watoto na kupika. Wasichana husaidia mama zao, jambo

linaloendeleza kurithishwa kwa majukumu hayo kwa wasichana kulingana na jamii husika. Kazi ya Moser imetusaidia kuchanganua majukumu ya wanawake katika mazingira na miktadha mbali mbali katika *Mbali na Nyumbani*.

Momanyi (1998) ametafiti *Usawiri wa Mwanamke Muislamu wa jamii ya Waswahili, Utensi wa Mwanakupona*. Kwa mujibu wa Momanyi, mwanamke Muislamu amedunishwa kwa sababu ya dini. Momanyi ametumia nadharia ya ufeministi. Utafiti huu umetusaidia kuelewa jinsi wanawake Waislamu wanavyohusishwa na kushirikishwa katika masuala ya dini. Madai kwamba, dini ya Kiislamu inamduunisha mwanamke ni tathmini ambayo utafiti huu unachukulia kuwa kwa kiasi fulani umetolewa kihisia na kiuchukulizi. Mada ya Momanyi ni tofauti na yetu kwa kuwa imekita katika usawiri wa mwanamke Muislamu ilhali katika kazi hii mazingira na miktadha ya kidini inachunguzwa ili kuonyesha uwasilishwaji wa wanawake.

Katola (2006) ametafiti *Udhalimu Dhidi ya wahusika Wanawake katika tamthilia za Kiswahili*, Hatia (1972), Mama ee (1987), Buriani (1983), Kitumbua Kimeingia Mchanga (2000). Ameorodhesha aina mbalimbali za udhalimu kama kuozwa bila hiari, kudharauliwa, kutawishwa na kukanwa na jamii. Kuozwa bila hiari, kwa mujibu wa Katola ni aina ya udhalimu. Ameelezea historia ya ufeministi wa Kiafrika kwa kusema kwamba ni tapo la ufeministi wa Kimagharibi. Tumeweza kufahamu kwamba, ufeministi wa Kiafrika, japo unatumwiwa kutafiti masuala katika miktadha ya Kiafrika, una misingi yake katika tamaduni za Kimagharibi na kwa misingi hii, utafiti unaokita katika nadharia ya ufeministi wa Kiafrika unaweza kuhitimishwa kwa hisia au chukulizi fulani kutokana na mgongano kati ya tamaduni za Kiafrika na za Kimagharibi. Katola pia ameorodhesha aina za udhalimu kama kuozwa bila hiari, kudharauliwa na kutawishwa,

mambo ambayo utafiti huu unadadisi kianthropolojia ili kuchunguza iwapo tathmini chanya inaweza kutolewa badala ya tathmini hasi. Tofauti kati ya utafiti wetu na wa Katola ni kwamba, ye ye ametumia nadharia ya Ufeministi wa Kiafrika ilhali utafiti huu umetumia anthropolojia ya kiutamaduni. Vile vile, mada yake ni tofauti na yetu.

Nyaosi (2008) anachunguza *taswira ya Asasi ya Ndoa* katika *riwaya ya Kiu ya S.A. Mohammed na Msimu wa Vipepeo ya Wamitila*. Katika utafiti huu, Nyaosi ameshughulikia dhuluma na ukandamizwaji wa wanawake katika asasi ya ndoa. Ameonyesha matatizo yanayowakumba wanawake katika asasi ya ndoa kama kuzaa na kulea watoto. Kulingana na Nyaosi, mwanamume amemwachia mwanamke jukumu la uzazi na ulezi. Utafiti huu umetusaidia kuchunguza majukumu yanayodaiwa kuwadhulumu wanawake katika asasi ya ndoa kama kuzalishwa na kuachiwa jukumu la kulea. Utafiti wa Nyaosi unatupatia msingi wa kuonyesha baadhi ya tathmini hasi kuwahu su wanawake ambazo zinaweza kuchunguzwa na kufikiriwa upya kwa kuzingatia kihistoria maisha ya wanawake.

Mulila (2009) ametafiti *Usawiri Chanya wa Wahusika Wanawake* katika tamthilia za *Zilizala* na *Chamchela*. Utafiti huu unaonyesha jinsi watanzi wa tamthilia hizi mbili wamewapa wahusika kike usawiri chanya. Kazi ya Mulila ni tofauti na yetu kwa sababu ameshughulikia tamthilia ilhali kazi yetu inajihuisha na riwaya ya kitawasifu.

Onyoni (2012) anatafiti *Usawiri wa Wahusika katika Tamthilia za Natala na Mama ee.* anasema kuwa watanzi wa kazi hizi hajawasawiri wanawake kuwa wahusika wakuu. Onyoni pia amedai kuwa mandhari ya usimulizi yanawabagua wahusika wanawake. Kusawiriwa kwa wanawake

katika mazingira ya nyumbani kulingana na Onyoni ni kubaguliwa. Wahusika wa kike kusawiriwa wakiwa wamewabeba watoto ni kudhulumiwa. Utafiti wa Onyoni umetuwezesha kupata tathmini hasi kuhusu mandhari kdaiwa kuwabagua wanawake. Tathmini hii inaweza kuchunguzwa upya kwa kuzingatia kianthropolojia masuala ya wanawake.

Emaita (2014) ametafiti suala la Uhamaji na Uhamiaji kama linavyojitokeza katika *Mbali na Nyumbani*. Ameeleza sababu zinazochangia watu kuhamza, matatizo yanayowakumba wahamaji na wahamiaji, hatua wanazochukua kusuluhiha matatizo hayo na manufaa ya uhamaji na uhamiaji. Utafiti wa Emaita umekuwa nguzo kuu kwetu katika kuchunguza mazingira ya kijiografia na kihistoria ambayo yametumiwa kubainisha kuwepo na “kutokuwepo” kwa wahusika wa kike katika kazi teule. Vile vile, suala la uhamaji na uhamiaji limetuwezesha kutambua sababu za wahusika kuhamza kutoka eneo moja hadi lingine. Utafiti huu umetusaidia kueleza uwepo na ‘utokuwepo’ wa wahusika wa kike katika mazingira ya uhamaji na uhamiaji. Hata hivyo, kazi yake ni tofauti na hii kwa kuwa yeye ametafiti suala la uhamaji na uhamiaji ilhali utafiti huu unahusu sababu za kuwepo na “kutokuwepo” kwa wahusika wa kike katika mazingira ya uhamaji na uhamiaji. Ametumia nadharia ya uhalisia ilhali utafiti huu umetumia nadharia ya anthropolojia.

1.8 Njia za utafiti.

Utafiti wetu kimsingi umefanywa maktabani ili tupate msingi thabiti wa kutafiti mada yetu. Kwanza, tulisoma *Mbali na Nyumbani* kwa kina. Usomaji huu ulituongoza kubainisha majukumu ya wanawake katika mazingira na miktadha ya uwasilishwaji wao. Pili, ulituwezesha kubainisha kuwepo kwa wahusika wa kike katika mazingira na miktadha fulani na kutokuwepo

kwao katika mazingira na miktadha mingine. Kubainisha uwepo wa wanawake katika miktadha na mazingira kimajukumu kulitujengea misingi thabiti ya kujadili sababu za mwandishi kuwawasilisha wanawake katika mazingira na miktadha hiyo. Ubainishaji wa mazingira na miktadha ambamo wanawake hawapo umetujengea misingi ya kujadili sababu za mwandishi kuwawasilisha kwa ufinyu katika mazingira na miktadha fulani na vile vile sababu za kutowawasilisha katika mazingira na miktadha mingine. Tumesoma kazi za wataalamu mbalimbali na tasnifu zinazozungumzia usawiri wa wanawake kimajukumu na jinsi usawiri huo ulivyotathminiwa. Tulilenga kupata baadhi ya tathmini na kauli hasi kuhusu wanawake katika tafiti za awali. Katika utafiti huu tathmini hizo zimechukuliwa kwamba zimehitimisha kwa kukisia au kiuchukulizi, bila kuzingatia historia na maendeleo ya wanawake. Tulidurusu baadhi ya maandishi ya mtandao ili tubaini uwasilishwaji wa wanawake kihistoria na kianthropolojia katika mifumo na taasisi za kijamii, kielimu, kisiasa, kitamaduni, kidini na kijeshi. Historia hii imetuwezesha kutathmini sababu za uwasilishwaji wa wanawake katika *Mbali na Nyumbani* bila hisia au uchukulizi wowote. Suala linapochunguzwa kihistoria ukweli hujitokeza. Majukumu ya wahusika wa kike yamechunguzwa kwa kuyahusisha na yale yanayotekelawa na wahusika wa kiume na tumeonyesha kufanikiwa au kutofanikiwa kwa wanawake katika mazingira na miktadha walimowasilishwa. Majukumu ya wanawake yamejadiliwa kwa misingi ya nadharia ya anthropololojia, tapo la kiutamaduni, kwa lengo la kuonyesha sababu za kuwepo kwao katika mazingira na miktadha fulani na “kutokuwepo” kwao katika mazingira na miktadha mingine.

SURA YA PILI

DHANA YA KUWEPO: UBAINISHAJI WA WAHUSIKA WANAWAKE KATIKA *MBALI NA NYUMBANI*

2.0 Utangulizi

Katika sura hii, tutabainisha kuwepo kwa wahusika wa kike katika mazingira na miktadha mbali mbali kimajukumu katika *Mbali na Nyumbani*. Ubainishaji huu unakusudia kuuwekea msingi mjadala wa utafiti kuhusu sababu za kuwepo kwa wahusika wa kike katika mazingira na miktdha hiyo.

2.1 Dhana ya kuwepo kwa wahusika wa kike

Dhana ya kuwepo katika utafiti huu itatumwa kubainisha mazingira na miktadha ambayo wahusika wa kike wamewasilishwa au kuhuishwa. Kuwepo kwa wanawake katika mazingira na miktadha mbali mbali kunahusiana na majukumu yao. Mahusiano kati ya mazingira na majukumu ya wahusika wa kike na nadharia ya anthropolojia ni kwamba, kuwepo kwao katika mazingira hayo pamoja na majukumu wanayotekeleza ni uhalisia wa maisha yao kihistoria, kianthropolojia na kiuandishi. Kwamba, kuwepo kwao na majukumu yao ni suala la uwasilishwaji kiuhalisia kuliko kiusawiri. Kabla ya kubainisha kuwepo kwa wanawake, tutafafanua dhana na masuala mbali mbali kuhusiana na wahusika ili tuonyeshe uhusiano wao na masuala ya kimsingi ya utafiti.

2.2 Uhusika na wahusika katika fasihi

Katika kazi bunilizi za kifasihi, wahusika huelezwa kama viumbe wanaoumbwa au kubuniwa na mwandishi ili washabihiane na binadamu wa kawaida. Kwa mujibu wa Njogu na Chimera (1999:45), wahusika ni sehemu ya fani. Wahusika husawiriwa kwa sifa za kitabia, kifalsafa, kimaumbile, kiitikadi na kimaadili. Mwandishi huwa na nafasi ya kuwaumba na kuwaumbua jinsi atakavyo. Dhima kuu ya wahusika katika kazi ya fasihi ni kuwasilisha ujumbe wa mwandishi au mtunzi kwa wasomaji au wasikilizaji. Matendo ya wahusika, tabia zao, maumbile yao na majukumu yao huwasilishwa kwa njia mbali mbali. Uwasilishaji waweza kutokana na maelezo ya mwandishi, usimulizi wa mwandishi au kupitia kwa wahusika wengine. Hata hivyo, mwandishi anapowasilia wahusika halisi katika kazi yake, huo ni uwasilishaji wa wahusika katika hali halisi ya maisha, sio usawiri. Mwandishi hana nafasi ya kuwaumba au kuwaumbua wahusika hao apendavyo. Uwasilishwaji wa matendo yao, tabia zao, itikadi na falsafa zao huwa halisi. Wahusika katika kazi bunifu za kifasihi wamechunguzwa na wataalamu mbali mbali. Wataalamu wanaainisha wahusika hao katika makundi kutegemea wadhifa wanaoshikilia katika kazi husika. Kuna wahusika wakuu, wahusika wadogo, wahusika bapa na wahusika duara. Wataalamu hawa hudai kuwa, wahusika wakuu ni wale waliopewa majukumu makuu na hujitokeza zaidi katika hadithi kuliko wale wengine. Wanadai pia kuwa wahusika wadogo na wasaidizi husaidia au humjenga mhusika mkuu ili aendeleze dhamira na maudhui. Hata hivyo, ubainishaji wa wahusika wa kike katika mazingira na miktadha kimajukumu katika *Mbali na Nyumbani* utafanywa kwa kuzingatia uhalsia wa maisha ya wanawake, kihistoria, kianthropolojia na kiuandishi. Sababu kuu ni kwamba, wahusika hao ni watu halisi waliowasilishwa katika mazingira na miktadha halisi ya maisha yao. Hivyo basi, utafiti huu haulengi kuonyesha majukumu ya wahusika wa kike kwa kutegemea wadhifa wao, bali

uonyeshaji wa majukumu utategemea mazingira halisi na uhalisi wa maisha yao. Kila mhusika katika *Mbali na Nyumbani* awe amepewa jukumu kuu au jukumu ndogo, anachukuliwa kuwakilisha uhalisi wa maisha ya wanawake. Kwa misingi hii, uwasilishaji wa wahusika katika tawasifu ya *Mbali na Nyumbani* ni wa kihistoria, kihalisia na kisaikolojia.

2.2.1 Wahusika wa kihistoria

Wahusika wa kihistoria hupatikana katika kazi za kihistoria. Katika kazi za kiubunifu, huchukuliwa kwamba hao ni wahusika walioumbwa kuwakilisha wale wanaohusishwa na matendo katika kazi yenye. Wamitila (2008:390) anaeleza kuwa mhusika wa kihistoria ni mhusika ambaye amesawiriwa katika misingi ya mtu aliyewahi kuishi. Hata hivyo, katika *Mbali na Nyumbani* mwandishi amewawasilisha na kuwahusisha wahusika kihalisia kwa njia ya kusimulia matendo yao, majukumu yao, tabia zao, itikadi zao, mitazamo yao na falsafa zao mionganini mwa mambo mengine. Kwa misingi hii, wahusika hawa japo ni wa kihistoria, hawawezi kutathminiwa kama wahusika katika kazi za kibunilizi za kihistoria, bali ukweli kihalisia ndio msingi mkuu wa kuwatathmini.

Wahusika wa kihistoria wanaowasilishwa na mwandishi wa *Mbali na Nyumbani* ni wengi. Amewahusisha na masuala tofauti tofauti. Kwa mfano, Jomo Kenyatta, Oginga Odinga, Tom Mboya, Dedan Kimathi na Dennis Okumu ni wahusika wa kihistoria ambao mwandishi anaeleza shughuli zao za kisiasa. Kipindi hicho cha mwaka wa 1960, Kenyatta alikuwa amefungwa huko Lodwar na wanasiasa wenzake walikuwa wakidai kuachiliwa kwake. Katika historia ya Kenya, wanasiasa hawa wote waliwahi kuishi na walijihuisha na shughuli za kisiasa kama anavyooleza mwandishi. Ukweli huu unatokana na historia ya siasa za Kenya wakati wa ukoloni. Kwa

kujikita katika upekee wa historia kama mtazamo katika tapo la anthropolojia ya kiutamaduni ni kweli kwamba, wahusika hao tuliowataja walijihuisha na siasa na matukio yanayosimuliwa ni ya kweli.

2.2.2 Wahusika wa kihalisia

Wahusika wa kihalisia ni wahusika ambao, katika kazi za kiubunifu wanasemwa kuwa na sifa nyingi zinazohusishwa na binadamu katika maisha ya kila siku. Wamitila (2008: 387) anasema kwamba mhusika wa kihalisia huainishwa kwa kufuata kanuni ya maisha halisi ikitegemea kanuni ya ushabibi kweli. Hata hivyo, katika kazi za uhalsia kama ilivyo katika *Mbali na nyumbani*, wahusika hawajahusishwa na matendo au sifa za binadamu, wao ni binadamu halisi wanaotekkeleza majukumu halisi katika maisha halisi ya jamii zao. Kwa mfano, katika hali halisi Fatma ni mke wa mwandishi, Laila ni bintiye mwandishi na Shafi ni mwanaye. Kwingineko, Daniel ni rafiki yake mwandishi ambaye alikuwa mwanafunzi katika Chuo Kikuu cha Khartoum. Mwandishi na wenzake wanapokosa mahali pa kulala baada ya kuhangaika muda mrefu, Daniel anawapa nyumba yake waishi hadi watakapopata viza. Wahusika hawa wamehusishwa na sifa na majukumu halisi.

2.2.3 Mhusika wa kisaikolojia

Mhusika wa kisaikolojia ni mhusika ambaye uwasilishwaji wake waweza kuwa wa kimawazo, kindoto au kifikira. Wamitila (2008:387-388) anaeleza kwamba mhusika wa kisaikolojia ni mhusika anayeonyeshwa kwa undani zaidi na labda hata misukumo ya kisaikolojia ya matendo yake kuonyeshwa kwa njia bayana. Kwa mfano, katika *Mbali na Nyumbani*, harakati zote za safari kuanzia wakati mwandishi anapotoroka nyumbani, vikwazo, mivutano na misukumo ya

kisaikolojia na kiakili kuhusu safari kama vile, kukosa pesa, chakula, malazi pamoja na visa vya kukatisha tamaa vyote vimemulikwa kwa undani. Mwandishi anaathiriwa na mambo mengi kimawazo, kifikra, kihisia na katika ndoto. Katika muktadha huu, wahusika fulani wamehusishwa kimajukumu bila kutambulishwa wazi katika maelezo. Athari za wahusika hao ni kubwa na zinachangia nafasi muhimu katika ukuzaji na uendelezaji wa maudhui na dhamira ya mwandishi. Kwa mfano, mwandishi anapouga akiwa kizuizini kule Gulu, anawaza ya laiti angekuwa nyumbani kwao, mama angempikia uji wa mapande uliokolea pilipili manga na mchana angemchemshia ndizi kwenye chukuchuku ya samaki iliyochapukia limao. Katika muktadha huu, mwandishi yuko mbali na mama yake kihalisia lakini kimawazo pana uhusiano wa karibu. Anatamani kuwa karibu na mamake ili amtunze vyema katika ugonjwa wake. Vile vile tunaona ulinganuzi wa chakula alichopewa na kile ambacho mamake angemtengenezea. Majukumu ya ulezi na upishi yanajitokeza kwa undani. Kutokana na mawazo ya mwandishi, tunaweza kuona uwepo wa mama yake ‘usiokuwepo’. Kwa misingi hii tunaweza kudai kwamba, japo mama yake hajawasilishwa katika hali halisi, uhusikaji wake upo na ni muhimu katika kazi hii. Watafiti wanaotathmini usawiri wa wanawake hutilia maanani uhusikaji wazi na kupuza uhusikaji fiche. Kwa kutilia maanani ukweli huu hadithi inapaswa kuchunguzwa kiuwasilishwaji ili kutoa tathmini zisizo za kukisia au za kiuchukulizi.

2.3 Dhana ya mandhari

Dhana ya mandhari ni pana na jumuishi. Ni dhana inayojumlisha mazingira, mwanda na wakati. Gills (1985) anasema kwamba, mandhari sio tu mazingira ya kijiografia kwa sababu pana masuala mengine kama kipindi cha matukio kihistoria na mwanda wa matukio kulingana na utokeaji wake. Matukio katika kazi ya kifasihi hutokana na matendo ya wahusika. Njogu na

Chimera (1999) nao wanasema kwamba, mandhari ni makazi maalum yaliyojengwa na mtunzi ambamo matukio mbali mbali hutokea katika kazi ya kifasihi. Ni mazingira ya wahusika pamoja na matukio, na mahali wahusika wanamoingiliana kijamii, kiuchumi na kitabaka. Kwa kuchunguza mandhari ya wahusika, kijamii, kiuchumi na kitabaka, majukumu yao hujitokeza. Wamitila (2003:210) naye anasema mandhari hutumiwa kuelezea sehemu ambako tendo fulani hutendeka. Neno hili hutumika kwa mapana kuelezea pia mazingira ya kisaikolojia ya tendo fulani. Mandhari huweza kurejelea yale mazingira, wakati na mahali ambapo tendo limetendeka. Katika kazi za kifasihi, mandhari ni kipengele muhimu katika uchunguzi wa wahusika kwa sababu wahusika ndio huendeleza msuko wa hadithi. Mazingira ambapo wahusika hutekekeleza matendo yao huathiri kwa kiasi kikubwa sifa zao, yaani wanaathiriwa kitabia, kimajukumu, kihisia na kisaikolojia. Katika utafiti huu, tunasema mandhari ni dhana inayorejelea wakati kihistoria na mahali kijiografia ambapo wahusika huwasilishwa na mwandishi ili watekeleze majukumu ambayo yanakuza na kuendeleza maudhui na dhamira. Katika muktadha huu, uhusiano uliopo kati ya mandhari na masuala ya kimsingi ya utafiti ni kwamba, mandhari yatachangia pakubwa kubainisha wahusika wa kike katika mazingira na miktadha mbali mbali ili tuonyeshe majukumu yao. Kuna aina tofauti tofauti za mandhari zikiwemo; mandhari ya kijiografia, mandhari ya kihistoria, mandhari ya kidhanifu au kinjozi, mandhari ya kiishara, mandhari ya kidokezi, na mandhari ya kiajinabi. Kwa kizingatia ukweli kwamba, *Mbali na Nyumbani* ni kazi ya kihistoria inayojikita katika uelezaji wa matukio ya kweli, utafiti huu umejihuisha na mandhari ya kijiografia, mandhari ya kihistoria na mandhari ya kidhanifu.

2.3.1 Mandhari ya kijiografia

Mandhari ya kijiografia ni msingi muhimu wa kuibua ukweli hasa katika kutathmini kazi za kihalisia. Matukio, mazingira na maingiliano ya wahusika katika hali halisi huaminika zaidi kwa kurejelea mazingira ya kijiografia. *Mbali na Nyumbani* imeandikiwa katika mazingira ya kijiografia barani Afrika na nchini Ujerumani. Mwandishi hajabuni mazingira au mandhari ambapo matukio yanatokea, kama ifanywavyo katika kazi za fasihi bunifu. Mandhari na mahali maalumu katika kazi hii vinaibua uhalisi wa wahusika na matukio yanayosimuliwa. Mazingira halisi ya kijiografia yanayoelezwa katika kazi hii ni ya kweli. Kwa misingi hii, mahusiano kati ya uwasilishwaji na uhusishwaji wa wanawake katika utafiti huu ni kwamba, mahali, wakati na mandhari yaliyopo yanaakisi ukweli kama unavyosimuliwa. Kwa mfano, mwandishi anaondoka Zanzibar akielekea Kairo kusaka elimu. Katika hali halisi Zanzibar na Kairo ni mazingira halisi ya kijiografia barani Afrika yanayoaminika. Tukio la kuondoka hadi Kairo ili kusaka elimu linaaminika kwa kuwa Zanzibar wakati huo hakukuwepo na Chuo Kikuu. Waafrika walitegemea zaidi Chuo Cha Kairo kwa sababu Misri ilikuwa tayari imepata uhuru, na ndio ilikuwa ngome ya elimu, siasa na uendelezaji wa shughuli za kupigania uhuru barani Afrika (uk 374). Vyama vya kisiasa vilikuwa na ofisi huko Kairo. Huko ndiko wanafunzi walikuwa wakitafutiwa masomo. Matukio yanayosimuliwa katika mazingira hayo ni halisi. Kwa mfano, usafiri katika meli unaofanya katika mto Nili na bahari ya Hindi. Usafiri wa treni kutoka Bungoma hadi Nairobi. Haya ni maeneo ya usafiri ambayo hata sasa yapo na usafiri unaosimuliwa uliendeshwa vivyo hivyo. Mfano, wasafiri wanapongojea kuingia ndani ya meli katika bandari ya Butiaba, wanasukumana na kukwaruzana kila mmoja akitaka kupata nafasi kwa sababu, meli ile ingewaacha wangengojea meli nyingine muda wa wiki nzima. Fauka ya hayo, hapakuwepo na mahali pa kuishi mtu akingoja kusafiri. Waliokuwa wakingojea walilala bandarini huku

wakifanywa chakula cha mbu (uk 77). Tukio hili ni la kihistoria ikizingatiwa kwamba, vyombo vya usafiri kabla na wakati wa ukoloni vilikuwa vichache na viliwekewa wakati maalumu wa kusafirisha abiria.

2.3.2 Mandhari ya kihistoria

Mandhari ya kihistoria huangaliwa kulingana na jinsi usawiri wa mazingira, mahali na wakati vinavyofungamana na kipindi fulani cha kihistoria. Ikiwa dhamira inahusu tukio la kihistoria, mwandishi husawiri wahusika halisi watakaoingiliana katika miktadha ya kihistoria. Tumeshaeleza kwamba, *Mbali na Nyumbani*, si kazi ya kibunilizi bali ni kazi inayoibua ukweli na uhalisi wa wahusika pamoja na dhamira na maudhui yaliyopo. Kwa misingi hii, wahusika hawa ambao baadhi wameshakufa na wengine bado wanaishi, wanawakilisha na kuwasilisha matukio halisi kihistoria. Kwa kuwa mwandishi ametumia mbinu mpya ya kiuandishi mandhari ya kihistoria yamechukuzwa kwa kuhusisha usomaji mbadala. Kwa mfano, tukio la mwandishi kuondoka Zanzibar kwenda Kairo ni tukio la kihistoria lililotokea kama anavyolisimulia. Kwingineko, upigaji kura uliotibuka tarehe 1 Juni 1961, huko Zanzibar, umeelezwa kwa kuonyesha matukio halisi na matendo halisi yaliyotendwa na wapiga kura. Hili ni tukio halisi la kihistoria lililowahi kutokea Zanzibar. Kwamba, Sultani na wakoloni walipanga uchaguzi huu. Mapigano yanayotokea yanarejelewa kihistoria kama Mapinduzi ya Zanzibar.

2.3.3 Mandhari ya kidhanifu/kinjozi

Mandhari ya kidhanifu ni mandhari ambayo hayahusishwi na uhalisia na yanaweza kuhusishwa na njozi katika kazi ya fasihi. Njozi hii inaweza kuwa imeundwa kimakusudi kama ulinganuzi wa uhalisi fulani. Katika hali halisi, wahusika huathiriwa na mambo mbali mbali katika harakati zao za kimaisha. Mhusika anapowaza au anapoota, wahusika wengine huhusishwa katika fikra zake na ndoto zake. Katika *Mbali na Nyumbani*, mwandishi, kuitia ndoto zake, hisia zake, matamanio yake, mawazo yake na fikra zake, amewahusisha wanawake. Huu ni uhusikaji usiokuwepo lakini upo. Uhusishwaji huu, japo ni fiche, una athari kubwa kwa mwandishi. Kwa mfano, mwandishi anapoondoka nyumbani kwa mama Halima, usiku huo anaota ndoto ambayo inahusisha Halima. Mazungumzo kati ya Shafi na Halima yanaonyesha matamanio na hisia kubwa za Shafi kumhusu Halima na hali yake ya shida na upweke. Ndoto hii inamsumbuwa mwandishi sana akiwa njiani kuelekea kazini. Anahisi kana kwamba ni kweli Halima alikwenda chumbani mwake akayaona maisha ya dhiki aliyoishi.

Halima anamwambia;

Hapa ndipo unapoishi?.....Twende zetu.....Popote pale tutakuwa mimi na wewe tu.Peke yetu, pale ambapo walimwengu wengine hawataweza kufika.....
Nyanyuka twende, nifuate (uk 167)

Shafi pia anaota ndoto kuhusu nyumba ya kifahari waliyoahidiwa na Daniel lakini ukweli unaibuka pale keshoye wanapata kuwa ni nyumba ya udongo isiyokuwa na dari (uk 289, 293). Katika ndoto hiyo, Nisreen anamkumbatia huku wote wakiangushana, mara Nisreen akiwa juu na yeche chini. Anakasirishwa na kelele za watu ambao wanakatiza starehe zake. Huu ni ulinganifu kati ya ukweli na ndoto. Haya yanaweza kuchukuliwa kama mandhari ya kidhanifu ili

kuonyesha tofauti ya nyumba halisi na ile ya kijonzi na vile vile hisia na matamanio ya mwandishi juu ya Nisreen. Mwandishi anajenga taswira yake kuhusu Kairo aifikiriayo. Anasema;

.....Jiji lililojaajaa starehe na mabenati wazuri
wanaotumbuiza katika makabare kwa kujinyonga
viuno na kutikisa matiti. Jiji lililoimbwa na waghani
na kusifiwa na washairi mahiri (uk 351)

Maelezo katika mawazo ya mwandishi yanaonyesha matamanio ya mwandishi ya kufika Kairo na maisha anayotarajia kupata huko. Wanawake anaowahusisha katika taswira yake hawapo katika hadithi lakini uwepo wao kimawazo una athari kubwa kwake. Robbins (2000:220) anasema kwamba, kazi za kifasihi zaweza kuonyesha kutokuwepo kwa wanawake katika hadithi inayowahusu wanaume lakini hii haina maana kwamba wanawake hawajahusika. Huu ni uwepo usiokuwepo ambao unapaswa kutathminiwa kwa uchanya. Kupitia mawazo ya mwandishi wanawake wamehusika na majukumu yao kuonyeshwa. Katika hadithi wanaume wanaweza kuwahusisha wanawake katika hadithi kupitia mazungumzo yao. Kwa mfano, mwandishi anapowaezea wenzake shughuli za harusi ya Waswahili anasema kuwa bwana harusi na rafiki zake hukaa kwenye mkeka huku wanawake wakiwaimbia wimbo wa bwana anakula soro, soro na manyamamanyama. Uhusishwaji wa aina hii ni fiche lakini tunaelewa jukumu la wanawake katika sherehe za harusi (uk 322). Tumeweza kufahamu majukumu ya mama yake Shafi kupitia mawazo yake. Kwanza anapougua na pili anapoishiwa na chakula (uk 227 na uk 90). Shafi anawaza jinsi mama yake angemshughulikia akiwa mgonjwa na vyakula ambavyo angempikia. Kwa mujibu wa Robbins (k.h.j) katika kazi ya kifasihi usomaji na uhakiki wa masuala ya wanawake waweza kuwa mgumu kutokana na hali ya kutohusishwa kwao kwa uwazi, kuhusishwa kwa ufinyu, kutopewa majukumu makuu au kupewa majukumu tofauti na yale ya wanaume kwa kuwa kinachotegemewa ni uwasilishwaji na uhusishwaji. Hata hivyo,

uwasilishwaji na uhusishwaji huu unapaswa kuchunguzwa na kueleza kihistoria na kimuktadha. Kwa misingi hii, Shafi amewahusisha wanawake kwa njia fiche kwa hivyo kuna uwepo wa wanawake “usiokuwepo”. Maelezo haya yana mahusiano na masuala ya kimsingi ya utafiti kwamba, “kutokuwepo” kwa wahusika wa kike katika hadithi inayowahusu wanaume, haina maana kwamba wahusika wa kike hawashirikishwi.

2.4 Muhtasari wa *Mbali na Nyumbani*

Japo *Mbali na Nyumbani* ni kazi iliyochapishwa mwaka wa 2013 masimulizi yanajikita katika miaka ya 1960 na kuhusisha matukio ya kihistoria. Mwandishi ndiye mhusika mkuu. Anaondoka Zanzibar akiwa na kiu ya kusaka elimu. Mwandishi alikuwa akilala chumba kimoja na nduguye mdogo Saad, kwa nyanya yao Asha binti Kassim. Anapata nafasi nzuri ya kuondoka bila kuwaaga wazazi wake, jambo linalomsikitisha baadaye. Waliokuwa na habari za kuondoka kwake ni Khamis Mohammed Nura, ambaye wakati huo alikuwa tayari yuko London, Mohammed Said Mohammed, Bilal Gharib na Abdalla Mwinyi Khamis. Abdalla Mwinyi Khamis ndiye alikuwa mwandalizi mkuu wa safari yake na kama anavyoeleza mwandishi, alimwachia jukumu la kuwasaidia wadogo zake. Anapotoka nyumbani anamuaga nduguye akiwa usingizini kwa kumwambia anaenda mandar Chwaka kwani ulikuwa mwezi wa Ramadhani.

Abdalla Mwinyi anampeleka Adam bandarini mwendo wa saa nne asubuhi April, 1960. Anaabiri M.V Ubena meli ya kampuni ya Kijeruman, Deutsh Ost - Afrika Linier. Ilikuwa meli ya kuchukua mizigo. Alipatana na abiria mwingine, kwa jina Ame, ambaye alikuwa akitoka Mkokotoni akielekea Makka kuhiji. Wanasaifiri hadi Tanga kisha Mombasa. Adam anaishiwa na chakula na pesa. Safari ya Aden inachukua wiki mbili na mwandishi anafadhiliwa na Waarabu

wawili ambao walikuwa wakirudi kwao Yemen kwa hofu kwamba, mwaka huo wa 1960, Tanganyika ikipata uhuru yanetokea machafuko makubwa. Meli inapotia nanga bandarini Aden, Adam anashuka kwa matumaini makubwa kwamba ndoto yake ilikuwa inakaribia kutimia. Matumaini ya Adam yanakatizwa na Afisa wa Uhamiaji anapomweleza kwamba, hawezi kushuka Aden mpaka aweke dhamana ya shilingi mia sita. Pesa alizokuwa nazo zilikuwa zimemwishi safarini. Alijaribu kuomba wakala na nahodha wa meli wamlipie lakini hawakumsaidia. Hatima ya Ame ilikuwa hiyo hiyo pia. Ofisini mwa wakala anampata daktari wa meno kutoka Zanzibar, Idarusi Balaawi na kumuomba msaada lakini haikuwezekana kwani alikuwa tayari ameshakabidhiwa kwa wakala wa meli ya kumrudisha Zanzibar.

Meli iliyomsafirisha Adam kutoka Aden ilikuwa na safari ya kuishia Mombasa. Kwa hivyo, aliamua kuishi Mombasa badala ya kurudi kwao Zanzibar kitendo ambacho alikiona kama ishara ya kushindwa. Melini alifahamiana na baharia mmoja, kijana Mwarabu aliyelewa Kingereza. Walielezana matamanio yao, ya mwandishi ya kwenda Ulaya kusoma na ya kijana baharia ya kufanya kazi katika meli kubwa zilizosafiri kutoka Ulaya hadi Marekani. Wanapofika Mombasa, Afisa wa Uhamiaji anakagua pasi yake na kumgongea muhuri wa miezi mitatu. Wakala wa meli, kijana wa Kijerumani anaizulia pasi yake hadi pale atakapopata pesa za kulipia nauji. Anapoingia Mombasa hana pasi ya kusafiria. Mwenzake Ame waliorudishwa pamoja anaingia Mombasa pia na hawaonani tena hadi mwisho wa hadithi.

Mjini Mombasa, Adam hajui pa kwenda na anaishia kutafuta maskani ya mabaharia huko Mwembe Tayari, mahali palipokuwa maarufu wakati huo. Katika maskani haya anatagusana na mabaharia maluuni, walevi, mahashashi na wenye uafriti wa kila aina. Wakazi wa pale walikuwa

vibarua wa bandarini ambao jioni walichanga pesa na kusokota sima iliyoliwa na walioachanga tu. Adam aliishi maisha ya kuomba chakula hadi wakati alipopatana na Mzee Ahmad Said, rafiki ya babake. Baadaye anakutana na Adam Mwakanjuki ambaye anamkaribisha kuishi naye kule Tudor muda wote alioishi Mombasa. Wakati huo Adam Mwakanjuki alikuwa akijishughulisha kikamilifu na harakati za vyama vyaya wafanyakazi hapo Mombasa. Mwandishi anapata nafasi ya kujuana na viongozi wengi maarufu wa vyama vyaya wafanyakazi nya Kenya kama Dennis Okumu, Ben Opar Mboya na wengineo. Wakati huu mwaka 1960, siasa nchini Kenya ilikuwa ikichekka sawasawa. Jomo Kenyatta alikuwa amefungwa Lodwar. Tom Mboya na Oginga Odinga walikuwa wakitembea nchi nzima wakidai uhuru na kudai Jomo Kenyatta aachiliwe. Mau Mau walichukua silaha kupigana na Waingereza. Dedan Kimathi alisakwa na Waingereza na kuuawa. Mwandishi anaelezea harakati zake za kutafuta kibarua bila kufanikiwa. Mara mojamoja alikimbilia meli ya simu bandarini alipofadhiliwa kwa chakula na mpishi aliyeitwa Nuhu. Adam hakuweza kufanya kazi ya kuparamia mameli nyundo mkononi tayari kuyagonga kutu iliyong'ang'anaa kwenye meli hizo kama mabaharia wa pale maskani. Aliiona kama kazi ya watu waliobobe, waliopambana na mawimbi na dhoruba kali, waliohimili vishindo vyaya pepo na mawimbi makali ya miamba. Pamoja na shida zote alizopata, hakuingiwa na wazo la kurudi nyumbani kwani haja yake ilikuwa kwenda Ulaya kutafuta elimu. Hatimaye mwandishi anakutana na Abdalla Juma Bulushi na Abdalla Juma Maharuki. Alisoma skuli moja na Abadalla Juma Bulushi huko nyumbani, Zanzibar. Mpango wa mwandishi kusafiri tena unachanua pale marafiki hawa wanamweleza kwamba walikuwa njiani kuelekea Kairo na pesa walizokuwa nazo zingetosha safari yao na yake pia kama alikuwa tayari.

Mwandishi anaelezea safari yao kutoka Mombasa hadi Nairobi kwa treni. Kabla ya kuondoka, Adam Mwakanjuki anampa anwani ya mwanasiasa mmoja huko Sudan, Abdulkadir- elAmin. Adam anaenda katika ofisi ya wakala wa meli ili kuchukua pasi yake ya usafiri. Anakaribishwa na mwanamke wa Kizungu. Anamdanganya wakala kwamba, shirika la Uhamiaji lilihitaji kumwongezea muda wa kuishi Mombasa, hivyo alihitaji pasi ikagongwe muhuri. Wanaondoka Mombasa kwa treni wakiandamana na Ben Opar Mboya. Mjini Nairobi wanakodisha chumba *Elgon Hotel* bar kule *River Road*. Kesho yake wanasaferi kwa treni hadi Eldoret wanapokaribishwa na Saidi Manywele. Baada ya siku moja wanahamia kwa rafiki za Juma Bulushi, mmoja akitwa Hussein. Baadaye Adam na wenzake wanakutana na Mzee Abdalla Ngazi. Huko wanapokelewa na Bibi Siti, mkewe Abdalla Ngazi. Mzee Abdalla Ngazi alikuwa na kiduka kidogo cha mboga ambapo Adam na wenzake waliketi siku nzima wakizungumza naye huku mkewe akichukua jukumu la kuwapikia chakula kila siku. Waliishi Eldoret kwa muda wa mwezi mmoja, wakila kwa Abdalla Ngazi na kulala kwa kina Hussein. Baada ya kupata pesa kidogo, walisafiri hadi Bungoma kuitia *Broadrick Falls*. Walikuwa wenyeji wa shemeji ya Abdalla Bulushi, Bwana Bakari Ali. Ali alikuwa na biashara ya ya kuuza nyama. Aliishi na Bwana Saidi wa Mwinyi na Bwana Saidi Hamza. Juma Bulushi alipofanikiwa kupata pesa za kutosha nauli yao hadi Kampala kwa treni, wanaondoka baada ya kuishi Bungoma kwa wiki mbili. Mwandishi anapoondoka Bungoma, anahisi kwamba mji huo ulimzoea naye akauzoea ila hakujua ni siri gani ilimfanya ahisi vile. Wanapofika Kampala wanakuwa wenyeji wa Mzee mashuhuri, Suleiman Manoti. Wanapokelewa vizuri na watoto wake kwa kuwa yeye alikuwa ameenda Hijja, huko Makka. Wenyeji hao ni watu waliosoma nao *Comorian School*. Adam na wenzake wanatafuta vibarua injini Kampala bila kufanikiwa. Abdalla Juma Maharuki anatuma barua nyumbani aletewe pesa na anapopata pesa anaamua kurudi nyumbani. Mwandishi anatuma

barua nyumbani akiomba babake pesa ili arudi nyumbani. Babake anamjibu barua na kumwelekeza kwa Bwana Mshangama Beja, mfanyakazi katika *Lake Victoria Hotel*, mjini Entebbe. Anapokea shilingi mia tatu. Yeye na Abdalla Bulushi wanaamua kuendelea na safari.

Mwandishi na rafiki yake wanaondoka Kampala kwa matumaini makubwa. Wanapanda treni ambayo inawapeleka hadi Namasagali. Wanakutana na watu wanaobeba mafurushi ya mizigo, wengine wamewashika watoto wao wakiwaongoza njia nao wanawake wa Kibaganda waliovaa kanzu bwanga bwanga zilizozuiliwa kwa kibwebwe kiunoni, wakipakia mizigo yao ndani ya treni. Wanaingia melini huku wakikaguliwa na walinzi wawili mlangoni. Walisafiri hadi Butiaba na kungoja meli ya kwenda Nimule. Wanawake waliskumana na watu huku wao wakibeba watoto wao, nao wanaume wakijitwisha mafurushi ya mizigo, kila mmoja akipigania nafasi kuingia melini. Askari walijaa langoni wakidai “*omsolo*”‘kodi ya kichwa’ abiria wanadhulumiwa. Ndani ya meli, Adam na mwenzake wanapatana na jasusi ambaye, baadaye anawasaliti kwa askari mpakani Nimule, walipotarajia kuvuka waingie Sudan. Hapo hapo Adam na Abdalla Bulushi wanawekwa chini ya ulinzi wa polisi kwa kosa la kutokuwa na viza ya kuingia Sudan. Wanapelekwa hadi Gulu ambapo wanazuiliwa kama mahabusu kabla ya kurudishwa hadi Bungoma. Wakiwa kizuizini, Adam anaugua Malaria kali. Homa hiyo inamfanya awakumbuke baba, mama na ndugu. Baada ya kuzuiliwa kwa wiki mbili, Mkuu wa Polisi aliyejewa Mzungu aliwashauri warudi Kampala wakapate viza ya kuingia Sudan. Wanapelekwa *Gulu Hotel* na kulipiwa gharama na Idara ya Polisi. Wanasaafiri kwa lori hadi Mbale ambapo wanatafuta malazi katika msikiti. Imamu anawapa malazi. Keshoye wanasaafiri kwa basi hadi Tororo kisha Bungoma, mahali ambapo mwandishi anaselelea kwa miezi sita.

Mwandishi anasimulia maisha yake akiwa Bungoma mahali ambapo anadai kufanya mengi yanayofanywa na kijana wa rika lake na kujifunza mengi. Wanakaribishwa na Bwana Bakari, shemejiye Abdalla Bulushi. Mwandishi anakuwa mkazi na mwenyeji wa Bungoma na kuingiliana na vijana hasa wa Kisomali ambao wazazi wao walimiliki biashara za mikahawa na maduka ya nyama. Alianza kujifunza Kibukusu ili aweze kuelewana nao vizuri zaidi. Ajabu aliyoona ni ya mtindo wa wanawake wa kuvuta sigara huku kaa la moto likiwa ndani ya mdomo badala ya nje ya mdomo. Mwandishi anaelezea jinsi alivyokutana na Abdo mmiliki wa mabasi mawili, moja likiitwa ‘*Mawingo*’ ,lingine likiitwa ‘*Kuiva*’, katika baa ya Mhindi aliyeitwa Noorali Sidi. Abdo anamuajiri kazi ya Ukondakta. Wanapokutana chumbani kwa Abdo, Mariana mpenzi wa Abdo ameketi pembedi akinywa soda. Anapopata kazi hii anahamia katika chumba cha msikiti wa Bungoma uliosimamiwa na Sheikh Noor. Hayo yanakuwa makao yake hadi wakati anapoondoka Bungoma. Mwandishi alikuwa mchoraji mzuri mionganini mwa wengine aliosoma nao wakiwa ni Seif Salim, Abdalla Hemed Jabir na Haji. Alijaribu kuomba kazi ya ualimu katika shule aliosomea mtoto wa Saidi Mwinyi lakini alipata kazi ya ukondakta kabla ya kuonana na mwalimu mkuu. Abdo alimfunza Adam kazi. Wanasa firi kutoka Bungoma hadi Kakamega huku akiangalia jinsi Abdo alivyokagua tiketi. Ndani ya basi, mbele kabisa, Mariana alikuwa amesimama huku ameshika bahasha ya nguo. Aliposhuka Abdo hakushughulika. Adam anafanya kazi hii na kuwekeza pesa ambazo zinamwezesha kupanga safari tena anapokutana na Shaaban Salim, waliokua pamoja.

Mwandishi anaondoka Bungoma akiwa na mwenzake Shaabani. Wanakuwa wenyeji wa Shariff, ambaye anashughulikia upigaji picha na maandalizi yote ya safari yao. Wanapokelewa na Abdalla Juma na Mohammed Saleh Mbamba, waliosoma pamoja *Teacher Training College*.

Walielekezwa wakifika Jinja washuke kisha wachukue teksi iwaveleke hadi Bugembe kwa rafiki ya Shariff, Maalim Idi. Wanapofika Bugembe, wanapokelewa na watoto wawili wa kike wa Maalim kwa heshima kubwa ya kuwapigia magoti na kuwabebea mizigo. Waliwawekea maji wakaoga, wakawapikia chakula kisha wakawewekea magodoro ukumbini wakalala. Maalim aliwashughulikia kwa muda wa wiki nzima huku wakihudumiwa na watoto wake wa kike kwa taa na unyenyekevu. Wanaondoka Bugembe wakiandamana na mwenyeji wao hadi Kampala ambapo anawajulishwa kwa Imamu wa msikiti aliyekuwa Mwarabu kutoka Yemen, ibada inapomalizika. Msafara wote unaandamana hadi viamboni, nje ya jiji hadi kwa Bwana Muhanji Msuo. Kiamboni humo kulikuwa na sherehe kubwa ya kidini iliyoandaliwa. Wanawake waliovaa makanzu ya Kiganda, bwangabwanga na vibwebwe viunoni walikuwa wakizunguka huku na huku wakitayarisha chakula. Waliandaa maandazi, supu, nyama, matoke na chai. Mwandishi, Shaabani na Abdalla walishiriki mazungumzo ya kidini usiku wa tarika ya shadhili. Mwandishi anaeleza jinsi walivyoombewa heri na Sheik-El-Hadadi kabla ya kwenda katika ofisi ya Ubalozi wa Sudan kwenye jengo la “*Amber House*” Wanapokelewa na Binti wa Kisudan aliyezungumza Kiingereza kilichojaa lafudhi ya Kiarabu. Balozi anawapa viza ya kuingia Sudan baada ya kuwahoji na kuwapa fomu za maombi wajaze.

Safari ya treni kutoka Bugembe hadi Namasangali ilichukua usiku kucha. Katika safari hii, wanaume manamba waliofanya kazi katika shamba la miwa la Kakira walikuwemo, wakiandamana na wake na watoto wao labda wakienda likizoni. Baadaye mwandishi anaelezea safari ya meli hadi bandari ya Masindi. Walibebwa na basi la Shirika la Reli na Bandari la Afrika Mashariki kuelekea Butiaba. Butiaba, walikesha katika kibanda hapo stesheni ili kusubiri meli ya asubuhi. Wanaabiri meli hadi bandari ndogo ya Pakwach ambapo wanatiwa mbaroni na maafisa

wa polisi, kinyume na matarajio yao ya kuendelea na safari. Wanapopelekwa katika kituo cha polisi cha Pakwach, wanachunguzwa na kuhamishiwa katika kituo kikubwa cha Arua. Huko wanahojiwa na kuhangaishwa. Adam anavuliwa nguo na Mzungu, mkuu wa kituo hicho akitaka athibitishe si Mkikuyu kutoka Kenya. Baada ya mateso ya muda, anaamuru askari awapeleke hadi Laropi ili waweze kufuata meli iliyowaacha. Baada ya siku mbili wanafika Nimule.

Baada ya kufanikiwa kuingia Khartoum kwa tabu tupu, wanahangaika wakitafuta viza ya kuingia Kairo. Hawana mahali maalum pa kulala, chakula ni shida na pesa hawana Wanaingia Sudan kupitia Juba. Afisa aliyekuwemo ndiye alikuwa Afisa wa Uhamiaji, wa Forodha na Polisi wa zamu. Wanasaifiri hadi Kosti kwa meli waliyoingia kwa adabu na heshima bila ghasia wala vurungu akilinganisha na zile za awali. Meli inapowasili katika kituo cha kwanza kidogo, inavamiwa na wenyeji waliokuja kwa makundi huku wamebeba mikungu ya ndizi na minofu ya nyama ya ng'ombe. Washitiri wa biashara walinunua bidhaa hizo. Hii ilikuwa biashara kubwa katika bandari zote Sudan ya Kusini, bidhaa zikisafirishwa hadi Sudan ya Kaskazini kulikokuwa jangwa. Mwandishi anaelezea kwa mshangao mkubwa utamaduni wa wenyeji. Wake kwa waume kukaa uchi. Wanawake vigori chuchu zimesimama, wazee maziwa yamewaporomoka vifuani. Chini hawakuwa na chochote cha kusetiri sifa ya uke wao. Wanaume makorodani yamening'inia pamoja na uume wao.

Waliondoka kwa safari ya bandari ya Kosti Misri katika meli iliyokuwa na msongamano wa abiria. Karibu na pale waliokaa, palikuwa na mwanamke wa Kinubi aliyemning' iniza mtoto baina ya miguu yake akimpanga. Kitoto hicho kilikuwa uchi, mashonde yakimtoka. Mbele kidogo alikuwepo mtu, mkewe na mtoto wao wa kike. Alikuwa ameketi huku mama akioka

mikate, akisaidiwa na mtoto huyo kigori. Kwa sasa, mwandishi na wenzake walikuwa wameishiwa na chakula. Anatamani kupata mkate na hilo linamkumbusha mama yake. Mwanamke huyo anawafadhili kwa chakula hadi mwisho wa safari. Alikuwa akimtuma yule mtoto wake kuwapelekea mikate mitatu kila siku. Msichana akiitwa Nisreen ambaye hakuwa akizungumza nao hadi wanaibandika mikate hiyo “*rizki bubu*” Mwandishi anadai kuwa Nisreen alibaki kuwa mpenzi wake wa ndoto. Mwandishi anaeleza kupatana kwao na wasafiri wengine Amos na Elly wenyeji wa Kenya, ambao pia walikuwa safarini kwenda kusaka elimu. Kundi likawa la watu watano. Waliingia Khartoum na kufuatana hadi katika Wizara ya Mambo ya Nje baada ya kuusiwa na mwenyeji mmoja mwenye gari aliyezungumza Kiingereza. Wanapofika ofisini wanaitishwa pasi zao kisha baadaye viza ya kuingia Sudan. Mwandishi, Shaabani na Abdalla wanaagizwa waende katika Ubalozi wa Misri huku Amos na Elly wakiwekwa chini ya ulinzi wa polisi mpaka hatima yao ijulikane na Wizara ya Mambo ya Ndani. Wanahifadhiwa katika jengo la Wizara ya Mambo ya Nje kwa muda kisha wanaanza kutafuta mahali pa kulala. Wanaishia kwenda katika Chuo Kikuu cha Khartoum ambapo walitarajia kupata vyumba vyakulala kwa bei nafuu. Wanakosa vyumba lakini mwanafunzi mmoja kwa jina Daniel anawapa nyumba yake waishi hadi pale watakopata viza ya kuingia Misri. Katika Chuo cha Khartoum, wanakutana na Zainabu, mwanafunzi kutoka Zanzibar. Katika hekaheka za kutafuta viza ya kuingia Misri, wanakutana na watu wengine kama Edward na Julius kutoka Kenya ambao tayari walikuwa wamemaliza mwezi mzima wakiingojea viza. Wakiwa katika hali hii ya shida, Adam anakumbuka baba, mama na ndugu. Anasema kwamba alikuwa na hakika kwamba baba na mama walikuwa wakidhani kwamba ameangamia wasikokujua. Hata hivyo alificha unyonge wake. Siku ile wanapotambua kwamba hakuna vyumba vyakulala chuoni, wanaondoka wanyonge na kupata mama la Kinubi limejaa tele pale palikuwa maskani yao kule stesheni ya

treni. Alikuwa amening'iniza mtoto mchanga miguuni huku wengine wawili wakimparamia mabegani naye mumewe ameketi pembedi akivuta sonyo. Stesheni ilijaa watu kila pembe. Wafanyabiashara nao walikuwa wakinadi huku vilio vya watoto waliobebwa na mama zao vikihuzunisha.

Mwandishi na wenzake watano walijuana na Oluoch ambaye alikuwa tayari ameishi Khartoum kwa muda mrefu akitafuta viza. Alikuwa amejuana na watu wengi akiwemo balozi wa Ghana. Wanaamua kumtembelea ofisini. Balozi aliwahutubia na kuwaeleza umuhimu wa Waafrika kuungana na kuwa kitu kimoja katika vita vya kujikomboa na kuikata minyororo ya kikoloni. Aliwapatia kila mmoja gurshi mia moja. Wanafululiza hadi *Bulbul Restaurant* na kushiriki mlo. Baada ya mwandishi kupata pesa anatamani kuuona mji wa Khartoum usiku. Anaelekea katika mtaa uliokuwa ukifanyiwa biashara ya pombe ya kienyeji na ukahaba. Anaingia ndani ya nyumba moja ya pombe na kumpata binti wa Kisudani. Baada ya muda mfupi wanashiriki ukahaba naye baada ya kulipa shilingi ishirini. Baadaye binti huyo anamsindikiza na kumbusu kwa ulaghai shavuni. Mwandishi na wenzake wanafanikiwa kupata viza na vile vile shilingi mia mbili. Safari ya kuingia Misri inaanza. Abiria wanaingia ndani ya treni kwa kupigana vikumbo na kutiana ngwara. Wanaume na mafurushi yao wanawake na watoto migongoni, wakilia na kupiga kelele zilizosikizwa tu na mama zao. Pale Shelal waliona wanaume wameva makanzu nao wanawake mabuibui, dalili ya kuingia Misri. Wanapoingia Misri, wanajiunga na Waafrika wengine ambao walikuwa wakipewa mafunzo ya kijeshi ili wapiganie ukombozi katika nchi zao. Katika mazingira haya, hakuna mwanamke hata mmoja anayehusishwa. Wanafunzwa mbinu za kulipua mabomu na vilipuzi vingine. Wakati wa mafunzo hayo, Luteni Sameer anawatahadharisha

kuhusu vilipuzi hivyo na kuwataka wafuate maagizo yote alio wapa. Mansour anakiuka maagizo hayo na analipuliwa na kuumizwa vibaya sana.

Mwandishi anasimulia kurejea kwake Zanzibar kisiri wakati wa utawala wa Sultani na wakoloni. Anajiunga na kundi lililokuwa likidai haki za wafanyakazi. Anajifunza uandishi wa gazeti. Katika ofisi ya chama cha kupigania haki za wafanyakazi, katibu mkuu ni Khamis Abdalla Ameir na msaidizi wake ni Hasina. Mwandishi ni mhariri wa gazeti la chama hicho lililoitwa '*Kibarua*'. Mwandishi anajuanan na watu wengi wakiwemo wanasiasa. Wakati wa uchaguzi nchini Zanzibar uliopendekezwa na Waingereza, *Juni 1961*, mwandishi anatumwa katika mojawapo ya kituo cha kupigia kura kama mwangalizi wa chama kimoja kilichoshiriki katika uchaguzi huo. Kunatoka machafuko na mwandishi anaelezea matatizo na tabu alizokumbana nazo njiani akirejea ofisini. Watu wanapigana na kuuana kwa mapanga. Wengine wanajeruhiwa vibaya sana (uk 432) Hali haikutulia hadi pale askari wa kigeni walipotuliza fujo hiyo. Mwandishi anasimulia jinsi alivyopata ufadhili wa chama kile cha wafanyakazi, kwenda Ujerumani kusoma. Anaelezea jinsi alivyosafiri hadi Ujerumani akiwa na Hussein na Suleiman. Katika safari yao, wanalala katika hoteli ya *New Stanley* mjini Nairobi. Katika ndege ya Skendinevia, wanapokelewa na mwanamke kisha wanapewa vinywaji na chakula na mabanati wawili, wote wakiwa Wazungu. Katika uwanja wa ndege, wahudumu ni wanaume. Wanapofika Zurich, wanapumzika katika hoteli moja ambapo wahudumu ni wanawake. Ndoto ya mwandishi kuisaka elimu inatimia baada ya kuanza masomo kwa kujifunza Kijerumani. Baadaye anapata elimu kuhusu mambo ya uchumi na kurejea Zanzibar ambako anafungua ukurasa mpya wa maisha yake.

2.5 Uwasilishwaji wa wahusika wa kike katika *Mbali na Nyumbani*

Wahusika wa kike katika *Mbali na Nyumbani* ni watu halisi. Uwasilishwaji na uhusishwaji wao pia ni halisi. Baadhi ya wanawake wametambulishwa kwa majina halisi huku wengine wakitambulishwa kama wanawake kipekee au kimakundi. Mwandishi ametumia zaidi nomino tatu; ‘*mwanamke*’, ‘*wanawake*’ na ‘*binti*’, hasa pale ambapo jina au majina halisi hayatumiwi. Tumebainisha wahusika wa kike kwa kutumia majina hayo kama yalivyotumiwa na mwandishi. Tumewabainisha kwa kujadili majukumu wanayotekeleza katika miktadha ya uwasilishwaji. Uwasilishwaji huu pamoja na uhusishwaji kimajukumu una mahusiano na nadharia ya anthropolojia ya kiutamaduni kwamba, wanawake kihistoria walihuushwa na majukumu ambayo hutekelezwa katika mazingira na miktadha ya kinyumbani huku wanaume wakihuushwa na majukumu nje ya miktadha ya kinyumbani. Utafiti huu umedai tangu mwanzo kwamba kuwepo kwa wanawake katika mazingira na miktadha ya kinyumbani katika *Mbali na Nyumbani*, si kunyimwa hadhi, kuonewa, kudhulumiwa au kudhalilishwa. Ubainishaji wa wanawake umefanywa kwa kufungamanishwa na wanaume. Ufungamanishaji huu unalenga kuonyesha ufanisi au “kutokuwepo” kwa ufanisi wa wanawake. Utafiti huu umebainisha kuwepo kwa wahusika wa kike katika mazingira yafuatayo;

- a) Mazingira ya kijamii.
- b) Mazingira ya kiuchumi
- c) Mazingira ya safari
- d) Mazingira ya kielimu
- e) Mazingira ya kiburudani

2.5.1 Mazingira ya kijamii.

Mahusiano kati ya uhusishwaji wa wanawake katika mazingira ya kijamii na nadharia ya anthropolojia ya kiutamaduni ni kwamba, majukumu yanayohusishwa na wanawake katika miktadha ya kijamii katika kazi hii hayalengi kuwanyima hadhi, kuwaonea au kuwadhulumu, bali ni uhalisia wa maisha yao vile ulivyo. Kuwepo kwa wanawake ni uhalisi unaotokana na mpangilio wa jamii katika mifumo na asasi za kijamii pamoja na tamaduni zao. Mahusiano kati ya uhalisi huu na anthropolojia ya kitamaduni ni kwamba, tamaduni za jamii za ulimwengu hufanana na kutofautiana. Kwa misingi hii, tathmini za masuala ya tamaduni katika jamii ya mwandishi ni za kiupekee na kimuktadha. Hivyo basi, majukumu ya wanawake katika *Mbali na Nyumbani* yanaelezeka kwa misingi ya upekee wa utamaduni kihistoria na kianthropolojia. Kuwepo kwa wanawake pamoja na majukumu yao kunaelezwa kianthropolojia na kihistoria. Katika mazingira ya kijamii uwepo wa wahusika wa kike umejitokeza katika muktadha wa kinyumbani na muktadha wa safari. Miktadha hii imeonyesha kwa uwazi majukumu yanayotekelezwa na wanawake kama itakavyojadiliwa hapa.

2.5.1.1 Muktadha wa kinyumbani

Katika muktadha wa kinyumbani, wanawake waliopo ni wazazi, walezi, wapishi, wapambaji na wapangaji nyumba. Familia ya mwandishi imewasilishwa ukumbini mwa nyumba yake mjini Dar es Salaam, mtaa wa Upanga, Fire. Siku hii ilikuwa ya kusherehekea siku ya kuzaliwa kwa Shafi, mwanawe mwandishi. Katika muktadha huu wanawake wamehusishwa na majukumu ya uzazi, ulezi, upishi na upambaji nyumba. Mwandishi anasema;

Ukumbi wa nyumba yangu ulikuwa umepambika vizuri kwani mke wangu, Fatma, ni hodari wa kuipanga nyumba. Hukiweka kila kitu pale kinapostahili kuwekwa, akavisanifu vikorokoro vidogo vidogo na kuvipeka kwa mpangilio mzuri mpaka mahali pakapendeza, pakamvutia mtu ye yote yule(uk 1)

Maelezo haya yanaonyesha jukumu la Fatma la kuipanga na kuipamba nyumba mpaka ikapendeza na kuvutia. Jukumu la kupanga na kupamba nyumba ambalo linaweza kuchukuliwa kuwa la kumnyima mwanamke hadhi, katika muktadha huu linamkweza mwanamke pale mwandishi analihuisha jukumu hilo na sifa kama ‘*hodari*’.

Laila kwa upande wake ni mpishi. Mwandishi anaeleza;

Tulikuwa tumekaa kwa furaha, mimi, mke wangu Fatma na watoto wangu wawili Shafi na Laila,tukila keki, visheti na biskuti. Vyote hivyo vilipikwa na Laila.Vyakula hivyo vyote tuliviteremsha kooni na sharbatil nzuri ya mabungo aliyoitengeneza mama Shafi (uk 2)

Kulingana na maelezo ya mwandishi, Laila na Fatma ni wapishi. Jukumu la upishi kianthropolojia ni la wanawake. Jamii za Kiafrika kihistoria zilihusisha wanawake na upishi, kazi ambayo ilirithishwa wasichana kutoka kwa mama zao. Upambaji nyumba pia ni jukumu la kinyumbani ambalo wanawake walitekeleza kabla ya mabadiliko yaliyotokana na wageni hasa wakoloni ambao waliathiri mipangilio na tamaduni za kijamii ikawa kwamba, mwanamke anatetea haki na usawa kimajukumu kwa madai kwamba, jinsia zote ni sawa na majukumu ya kinyumbani yanapaswa kuhusisha wanaume pia. Japo wahusika wanaume wapo, hawajahusishwa na upishi. Wao wameketi tu kungoja maandalizi ya chakula yafanywe na wanawake. Uhusishwaji huu katika *Mbali na Nyumbani*, kihalisia unaelezeka kianthropolojia bali haulezeki kiusawiri.

Asha binti Kassim ni nyanyake Adam. Adam na nduguye Saad walikuwa wakilala katika nyumba ya nyanya yao huko Zanzibar. Katika muktadha huu, Asha binti Kassim ni mzazi na mlezi. Rosaldo (1974) anaeleza kwamba, uhusiano uliopo kati ya jukumu la uzazi na shughuli za

kinyumbani si suala la lazima. Majukumu ya wanawake katika miktadha ya kinyumbani ni ya kupangwa na ya kitamaduni kwa kuwa, mwanamke hutambulishwa kilimwengu kwa misingi ya uzazi na majukumu ya kijamii. Uhusiano wa mwandishi na Asha binti Kassim ni wa uzazi kwamba, Asha ni nyanyake. Asha anatambulishwa kwa jukumu la uzazi katika kazi hii. Hata hivyo, katika jamii nyingi za Kiafrika, ilikubaliwa kimila na kidesturi wajukuuu kuishi na babu au nyanya zao ili wawasaidie kazi za kinyumbani. Uhusishwaji wa Asha binti Kassim si wa kuonewa, kudhalilishwa au kunyimwa hadhi, bali ni uhalisia wa utamaduni katika jamii ya mwandishi.

Mzee Abdalla Ngazi ni mkazi wa Eldoret. Yeye na mkewe, Biti Siti wanawakaribisha mwandishi na wenzake nyumbani kwao kule Eldoret. Biti Siti ni mwanamke mpole, mkarimu na mwenye mapenzi ya mzazi. Kazi yake ilikuwa kuwapikia Adam na wenzake huku mumewe akishughulika katika biashara. Mwandishi anaeleza hivi;

Tulipofika kwake, tulipokelewa na mke wake, Bibi Siti, aliyejkuwa mpole, mwangi wa huruma na aliyetupenda kama watoto aliowazaa mwenyewe. Ilipofika saa ya kula, Biti Siti hakuchoka hata siku moja kutuandalia chakula na sisi tukala kadiri ya kutosheleza njaa yetu (uk 57).

Biti Siti ni mama, mlezi na bibi. Jukumu kuu alilopewa ni upishi. Mzee Abdalla naye ni mfanyakia biashara. Mwandishi anaeleza kwamba, Mzee Abdalla alikuwa na kiduka cha mboga. Hapo ndipo aliketi kutwa akiuza bidhaa ili apate riziki ya kukimu familia yake (uk 57). Uhusikaji huu ni uhalisia wa maisha ya wanawake yalivyokuwa. Wanawake hawakuhusishwa na utafutaji wa riziki. Wao walizaa na kulea watoto kwa kutegemea waume zao. Moser (1993) anasema kwamba, wanawake kwa kawaida huhusishwa na kazi ambazo zinahitaji muda mrefu na

uvumilivu sababu mara nyingi ni za kurudiarudia tu, kama kuchota maji, kutafuta kuni, kulea watoto na kupika. Biti Siti amewapikia wageni wake kwa muda wa mwezi mmoja bila kuchoka. Katika muktadha huu wa upishi, Biti Siti anaonyesha uhalisi wa jukumu hili. Mwandishi hajamdunisha wala kumnyima hadhi. Ni ukweli kianthropolojia na kihistoria.

Mama Halima ni mwanamke Msomali, mkazi wa Bungoma. Ana binti mmoja kwa jina Halima. Mama Halima alijuana na mwandishi katika safari zake za Bungoma na Kakamega wakati mwandishi alikuwa kondakta wa basi. Vile vile, nyumba ya Mama Halima ilikuwa karibu na msikiwa Bungoma ambapo mwandishi alikuwa ameomba chumba cha kuishi. Mama Halima alimkaribisha mwandishi nyumbani kwake na kuagiza Halima kutayarishia Adam chai. Katika mazungumzo yao, Mama Halima anamhadithia mwandishi kuhusu waume wake watatu alioishi nao kwa zamu kama ilivyo mila na desturi za Wasomali. Uwasilishwaji huu katika muktadha wa kinyumbani na uhusishwaji wa jukumu la upishi ni suala la kitamaduni kwamba, wasichana hurithishwa majukumu ya kunyumbani na mama zao. Mama Halima anapomwagiza Halima alete chai inaeleweka wazi kwamba, japo Halima ni msichana mdogo amefunzwa upishi na mamake. Moser (k.h.j) anasema kwamba, wasichana husaidia mama zao katika kazi za kinyumbani na hii huwa njia ya kuendeleza na kurithisha majukumu hayo kwa wasichana kulingana na taratibu katika jamii. Mwandishi hajamwasilisha Mama Halima kama Malaya kwa kueleza alivyoishi na waume watatu, kama inavyoweza kuhitimishwa na watafiti ambao hupuuza masuala ya kianthropolojia. Huu ni utamaduni katika jamii ya Wasomali.

Watoto wa kike wa Maalim kule Bugembe, walikaribisha mwandishi na wenzake kwa kuwapigia magoti na kuwabebea mizigo. Wanawawekea maji ya kuoga na kuwapikia chakula kisha

kuwaandalia mahali pa kulala. Majukumu yanayohusishwa na watoto hao wa kike ni ya kinyumbani kama kupika, kutayarisha maji ya kuoga na kutayarisha malazi. Muktadha wa kitamaduni unajitokeza pia. Kupiga magoti na kuwabebea wageni mizigo ni utamaduni wa Waganda. Mila na desturi zao huwataka wanawake kuwapokea wageni kwa kufanya hivyo kama njia ya kuonyesha heshima. Mahusiano kati ya upigaji magoti na nadharia ya anthropolojia ni kwamba, kupiga magoti, kuwabebea wageni mizigo, kuwaandalia chakula na malazi si kuwadhalilisha bali ni utamaduni wa Waganda amba hata sasa baadhi ya Waganda huenzi na kuheshimu.

Asha, mkewe Ali na Nuru, mkewe Adam, walipokea mwandishi na wenzake huko Kairo.

Mwandishi anatoa maelezo yafuatayo;

Asha na Nuru walitupokea vizuri. Walituonyesha chumba chetu. Kama waliojua tulikuwa na njaa, walituandalia chai nzito na mayai ya kukaanga na mkate wa fimbo. Siku nyingi hatukula chakula kama kile, kwa hivyo hatukula bali tulifakamia (uk 372).

Maelezo haya yanaonyesha kuwa Asha na Nuru mbali na upokezi wa wageni ni wapishi.

Baadaye mwandishi anaeleza vile hamu yake ya kuoga ilisadifu kana kwamba Nuru aliyasoma mawazo yake, anaeleza;

Nilikuwa nikiwaza jinsi ya kuwaambia wenyeji wangu juu ya haja yangu ya kuoga ndipo alipokuja Nuru akasimama mbele ya mlango wa chumba chetu na kitumbo chake cha ujauzito. Mkononi alikuwa amekamata taulo na sabuni. “Nendeni mkaoge, alitwambia (uk 372).

Uwasilishwaji wa Nuru kama mjamzito unaonyesha jukumu la uzazi. Vile vile, Asha ni mzazi na mlezi kwani tunaelezwa kwamba, Ali alipoingia chumbani mwake alitoka akiwa amembeba mtoto wake mchanga, Raisa, na kuanza kucheza naye. Kipindi cha kula kilipowadia, Ali alimwita Asha amchukue Raisa ili aweze kushiriki mlo na wageni wake (uk 384). Jukumu la ulezi linapewa Asha wakati wa chakula kwa kuwa, mwanamke ndiye mlezi wakati wowote.

Mamake Adam amewasilishwa nyumbani kwao Zanzibar akiwa ameketi juu ya mkeka huku amepakata watoto wawili mapacha amba ni ndugu zake mwandishi. Huu ni wakati Adam aliporejea Zanzibar kisiri baada ya kupata mafunzo ya kivita huko Kairo kwa lengo la kutayarishwa kupigania uhuru wa nchi yake. Watoto hao ni Fatma na Zawadi.

Mwandishi anaeleza;

Nilipofika nyumbani nilimkuta mama yangu amejifunga kanga kifuani. Alikuwa amekaa juu ya mkeka amepakata watoto wawili wachanga. Mmoja alimpakata mkono wake wa kulia mwengine mkono wake wa kushoto. Aliponiona alishtuka. Alinitumbulia macho. “Maskini mwanangu! ”alisema kwa sauti ya hisia za mama aliyepotelewa na mwanawe akakata tamaa ya kumwona tena (uk 422).

Mamake Adam ni mzazi na mlezi. Watoto wale wanaelezwa kuwa wamelala usingizi mikononi mwa mama yao. Mama haonyeshi kuchoshwa nao. Anavumilia uzito wa watoto wawili mikononi mwake. Baba yake Shafi hahusishwi na ulezi. Ameshaenda kwenye sherehe za maziko.

Kule Kampala, nyumbani kwa Bwana Muhanji Msuo, Bwana Msuo alikuwa ameandaa dhifa kubwa ya Kidini. Palikuwa na wageni wengi sana wakiwemo Adam na wenzake. Kundi la

wanawake limehusishwa katika maandalizi ya vyakula mbalimbali kama maandazi, kuku, matoke, mchuzi wa nyama na chai. Mwandishi anaeleza hivi;

Wanawake waliova makanzu ya Kiganda, bwangabwanga na vibwebwe viunoni walikuwa wakizunguka huku na huku. Huyu kabeba mwiko, huyu alikuwa na upawa mkononi. Upishi huo ulikuwa uwanjani nje ya vijumba vyia kiamboni pale. Karai kubwa ilikuwa juu ya mafiga. Mafuta yalikuwa yakinokota tokotoko. Moto mkali ulikuwa umechanua chini yake, umetawanya ndimi zake, maandazi yakiiva taratibu. Mwanamke mmoja alikuwa amesimama pembeni ya karai akiyageuzeza maandazi(uk 185).

Katika maelezo haya wanawake hawa ni wapishi. Kila mmoja alishika jukumu lake na kulitekeleza dhidi ya changamoto zilizoko. Wanawake hawa wanaonyesha uvumilivu katika kazi ya upishi kwani mwandishi anaeleza kwamba, moshi uliokuwa umechanganyika na harufu ya mafuta ulikuwa ukiwapalia machoni na kuwashasha puan. Waandalizi uwanjani walihangaika na sahani za matoke na mabakuli ya mchuzi mikononi wakiwaandikia wageni. Uhusishwaji huu wa kimakundi una mahusiano na nadharia ya anthropolojia kwamba, utamaduni wa jamii za Kiafrika kabla ya kuathiriwa na majilio ya wageni ulikuwa hivyo. Ushirikiano wa wanawake katika upishi lilikuwa jambo la kawaida. Mgao wa majukumu umeonyeshwa kihalisia kwamba, kuna wale walipika vyakula fulani na kuna waandalizi walihangaika kuwapa wageni chakula. Kila mtu alikuwa na jukumu lake alilotakiwa kutekeleza katika sherehe hiyo. Kutohusisha wanaume katika upishi huu kunachukuliwa kuwa suala la kianthropolojia kwamba, hili ni jukumu la wanawake, na wala si kuwadhalilisha.

2.5.1.2 Muktadha wa safari

Katika muktadha wa safari, mwandishi amewahusisha wanawake na jukumu la uzazi, ulezi, upishi. Japo ni miktadha ya safari majukumu haya yanaonekana kuwa ndio makuu kwa wanawake. Wanaume wamehusishwa na majukumu tofauti kabisa na ya wanawake katika miktadha hii hii. Carol (1990) anaeleza kwamba, katika jamii nyingi ulimwenguni, majukumu fulani hupewa wanaume huku mengine yakipewa wanawake. Kwa mfano, katika mataifa ya Ulaya na Amerika, wanaume ndio walikuwa mihimili ya jamii huku wanawake wakiwa wategemezi. Majukumu ya wanawake yalikuwa kulea watoto pamoja na kazi zote zinazofanywa ili kukimu na kuendeleza familia. Uhusishwaji wa wanawake katika ulezi na uzazi katika miktadha ya safari unaashiria kwamba, jukumu la ulezi na uzazi humuandama mwanamke popote pale. Rosaldo (1974) anasema kwamba, watoto wachanga hukaa na kuingiliana muda mrefu na mama zao kuliko baba zao na kwa hivyo, hili ni jukumu la kimsingi la wanawake. Baadhi ya wanawake ambao wamehusishwa kama wazazi na walezi katika safari wanapatikana katika maelezo ya mwandishi kama ifuatavyo;

Hapo stesheni palikuwa zahama ya watu, wakienda na kurudi, wengine wamebeba mafurushi ya mizigo, wengine wamewashika watoto wao wakiwaongoza njia. Wanawake wa Kibaganda waliovaa kanzu bwanga bwanga zilizozuiliwa kwa kibwebwe kiunoni, wakipakia mizigo yao ndani ya treni (uk 68).

Uhusishwaji huu unaonyesha uhalisi wa jukumu la uzazi na ulezi. Mwanamke anaonekana kuandamana na watoto hata safarini na ijapokuwa katika miktadha hii ya usafiri wapo wanaume, mwandishi hawahuishi kabisa na jukumu la ulezi. Thibitisho linajitokeza katika maelezo ya mwandishi kwamba;

Wanawake waliwabeba watoto wao, wanaume walijitwisha mafurushi ya mizigo. Kila mmoja alitaka awe mbele katika foleni (uk 74).

Kwininge, katika (uk 77) mwandishi anaeleza kuwa vilio vyatoto waliobebwa na mama zao vilisikika tu na mama zao. Wanaume hawakujali vilio vile kwa kuwa walikuwa wakipigania kuingia melini, wakiwabinya watoto hao. Mwandishi anatuonyesha wazi kwamba, shughuli zote kuhusu mahitaji ya watoto humlenga mwanamke, kwamba, wanaume kianthropolojia hawakuhusishwa na ulezi wa watoto. Katika safari hii hii ya kuelekea Nimule kupitia mto Nili, wanawake waliowasilishwa mbali na kuwatunza watoto wao, wanawapikia chakula na kuwafuta kinyesi kwa makaratasi na matambara. Harufu ya kinyesi inaonekana kumkera mwandishi anapoeleza kwamba, ingawa harufu mbaya ya vikwapa vyatoto binadamu ilipuliza, ilizidi kukirihisha ilipochanganyika na ile ya kinyesi cha watoto waliokuwa wakienda haja kubwa na ndogo papo hapo. Shughuli hii ya kuwapangusa watoto mashonde inajitokeza pia (uk 226) mwandishi anapoeleza kwamba, mama wa Kinubi alikuwa amening' iniza mtoto wake mdogo baina ya miguu huku mashonde yakimtoka mtoto bila habari ya karaha alyokuwa akiifanya. Katika meli hiyo pia, wanawake wamewasilishwa kama wapishi. Mwandishi anaeleza;

Mbele yetu walikuwa watu walioonekana kama wa ukoo mmoja. Baba, mama na mtoto wao wa kike.....Baba alikaa mkao wa kuisuka miguu yake. Mkewe alikuwa amejizonga ushungi mweupe, ameshughulika akichoma mikate kwa jiko la mafuta taa. Mtoto wao kigori, maziwa ndo kwanza yanamchipuka, alikuwa anamsaidia mama yake kugeuza mikate uliokuwa ndani ya chuma cha kuchomea mikate (uk 226).

Kama inavyodhihirika, upishi ni jukumu la kimsingi la mwanamke na hulitekeleza mahali popote. Baba hashughuliki na upishi. Tendo la msichana kumsaidia mama yake laweza kuchukuliwa kama njia ya kumrithisha jukumu la upishi. Huku si kunyimwa hadhi bali ni uhalisia wa kihistoria na kitamaduni.

Katika stesheni ya treni, mjini Khartuom mwanamke amewasilishwa kama mzazi na mlezi. Mwandishi anaeleza kwamba, mama la Kinubi lilikuwa limechukua nafasi yao waliyozoea kutandika makaratasi na kulala kwa kuwa hawakuwa na mahali pa kulala (uk 279) Mwanamke huyo alikuwa na watoto watatu. Yule mchanga alikuwa amening'inia katikati ya miguu huku wawili wadogo wakimparamia mama yao mabegani. Baba yao alikuwa amekaa pembedi akivuta sonyo. Mama huyu ni mzazi na mlezi. Kutohusisha baba na jukumu lolote hakumaanishi kumdhulumu mke wake bali ni suala la kianthroplojia kwamba, wanaume hawakushiriki katika ulezi. Baba anaonekana kustarehe na hajishughuliki na ulezi wa watoto. Kwingineko, wanaume manamba waliofanya kazi katika shamba la miwa la Kakira walikuwa wameandamana na wake zao na watoto wao, labda wakienda likizoni. Wanawake hao walikuwa wamebeba watoto wao. Uhusishwaji huu unaonyesha mama kama mzazi na baba kama mfanyakazi. Uhusishwaji huu hauna maana kwamba wanawake wamenyimwa nafasi ya kufanya kazi katika shamba la miwa wala haina maana kwamba mwandishi amewadhalilisha bali ameonyesha ukweli wa majukumu kijinsia, kianthropolojia na kihistoria.

2.5.2 Mazingira ya kiuchumi

Uwasilishwaji wa wanawake katika mazingira ya kiuchumi umejitokeza kianthropoljia na kihistoria. Mazingira ya kiuchumi katika utafiti huu yamehusishwa na muktadha wa kikazi na muktadha wa kibashara. Wanawake katika mazingira haya hawajahusishwa bali wamehusika. Baadhi ni wapokezi na wahudumu katika ndege, mahoteli na ofisi. Katika miktadha hii wanaume wamehusishwa pia. Wanawake wanaonekana kupewa majukumu ya kisaidizi yakilinganishwa na yale ya wanaume. Mahusiano kati ya wanawake kupewa kazi za kisaidizi katika mazingira ya kiuchumi na nadharia ya anthropoljia ni kwamba, wanawake hawakuhusishwa na masuala ya

kiuchumi kwa kuwa walikuwa wategemezi kwa wanaume. Wanaume ndio walikuwa mihimili huku wanawake wakiwa wasaidizi tu. Hii ndio sababu uwasilishwaji huu unaonyesha idadi ndogo ya wahusika wa kike pamoja na uhusika wao kama wasaidizi tu. Utafiti huu umedai tangu mwanzo kwamba, tathmini za watafiti wa awali zinazohitimisha kwa madai kuwa, kutohusishwa kwa wanawake kwa wingi katika mifumo ya kiuchumi ni kutengwa au ni utegemezi zinaweza kufikiriwa upya ili kuwapa wanawake tathmini chanya kwa kuzingatia historia na maendeleo ya wanawake katika mifumo ya kiuchumi.

2.5.2.1 Muktadha wa kikazi

Katika muktadha wa kikazi, wanawake wamehusika katika kazi mbali mbali. Kazi wanazofanya wanawake hawa ni tofauti na zile zinazofanywa na wanaume katika mazingira yayo hayo. Wanawake katika mazingira ya kikazi wamewasilishwa kama wahudumu na wapokezi hasa ofisini na hotelini. Vile vile uwasilishwaji wa wanawake umeonyesha mwuguzi, mwalimu, katibu muhtasi, watafsiri na wafagizi. Kwa mfano, katika hoteli ya *New Stanley*, mjini Nairobi, pana mpokezi wa kike ambaye ni mwanamke wa asili ya Kizungu. Aliwapokea Adam na wenzake bila mlahaka mzuri. Anaelezwa kuwa mnafiki na mwenye kiburi. Haya yamejitokeza wakati anapowaelekeza Adam na wenzake katika vyumba vyao (uk 445). Katika hoteli hii hii, pana mhudumu wa kiume aliyevalia nadhifu. Anaelezwa kuwa aliwapokea kwa heshima kwa kujipinda kabla ya kuwaelekeza kwenye meza. Kwingineko, katika ndege ya Skendinevia, Adam na wenzake walipokuwa wakielekea Ujerumani, walipokelewa na mwanamke Mzungu, mrefu, mwenye nywele za dhahabu, aliyevalia sare ya buluu. Baada ya ndege kupaa angani, mwandishi anaeleza kwamba waliandaliwa vinywaji na mabenati wawili waliokuwa wapole. Uandalizi wa kinywaji ni shughuli ya kiupishi. Mwandishi ameonyesha ukweli kwamba jukumu la upishi ni la

kimsingi kwa wanawake. Rubani wa ndege ni mwanamume. Uhusikaji huu unaonyesha tofauti kati ya kazi za wanawake na za wanaume. Mwanamume anaonekana kupewa kazi muhimu naye mwanamke akihusishwa na kazi za kisaidizi. Uhusishwaji huu unaonyesha uhalisi wa kazi za wanawake kihistoria. Uendeshaji ndege kimsingi ulihuhsishwa zaidi na wanaume. Ilikuwa adimu kupata mwanamke rubani katika kipindi hicho kihistoria. Wanawake walajiriwa kama wahudumu tu na ilikuwa vigumu kupata wahudumu wanaume katika usafiri wa ndege.

Mifano mingine ya uhusishwaji wa wanawake katika muktadha wa kikazi inajitokeza katika ofisi ya wakala wa meli mjini Mombasa (uk 39). Mwandishi amemwasilisha mwanamke Mzungu ambaye ni mpokezi. Wakala wa meli ambaye alikuwa Mjerumani alizuilia pasipoti yake hadi wakati angelipa nauli ya meli. Haya yanatukia baada ya Adam kurudishwa hadi Mombasa kutoka Aden. Katika ofisi hii hii, bawabu wa mlango alikuwa mwanamume. Kazi ya uwakala inaonekana muhimu na inayompa mwanamume hadhi ya juu ikilinganishwa na ya upokezi ambayo inatekelezwa na mwanamke. Tunaona pia kazi ya kulinda lango imehusishwa na wanaume. Kihistoria wanawake walipoanza kufanya kazi za kiofisi, walihuhsishwa na kazi zisizohitaji nguvu nyingi. Kwa misingi hii, uhusishwaji huu ni wa kihistoria na kianthropolojia na mwandishi hajampa mwanamke mpokezi hadhi ya chini wala kumnyima nafasi ya kuwa wakala au bawabu.

Katika ofisi ya Ubalozi wa Sudan, mjini Kampala (uk 190), mpokezi ni Mwfrika, Binti wa Kisudan aliyekuwa akizungumza Kiingereza kilichojaa lahaja ya Kiarabu. Uhusishwaji huu unaonyesha uhalisi wa maisha ya wanawake kielimu. Vinginevyo, Binti wa Kisudan ni mwakilishi wa wanawake wachache wa kiafrika ambao walikuwa wafanyakazi katika ofisi

wakati wa ukoloni. Wapokezi hawa wawili, Mwafrika na Mzungu, ni wawakilishi wa wanawake waliofanya kazi za kisaidizi katika ofisi tofauti tofauti kama kuwapokea wageni. Uhusishwaji huu ni uhalisi wa wanawake kikazi katika kipindi hicho kihistoria.

Uhusikaji wa mwuguzi, mwalimu na katibu muhtasi ni wa kiuwakilishi. Mwuguzi Mwafrika katika hospitali ya Hindu Mandal, kule Zanzibar ndiye alimjulisha mwandishi kwamba Abdalla Juma alikuwa ameaga dunia (uk 479) Kihistoria, wanawake walikuwa wauguzi huku udaktari ukihuishwa na wanaume. Kuwepo kwa mwanamke mmoja mwuguzi kunathibitisha hali ya wanawake kihistoria katika miktadha ya kikazi kwamba, kutokuwepo kwao kwa wingi sio kunyimwa nafasi bali ni hali halisi ilivyokuwa kipindi hicho cha mwandishi. Mwanamke anayehusika kama mwalimu wa lugha ya Kijerumani katika Chuo Cha Bernau pia tunaweza kudai kwamba ni mwakilishi wa wanawake waliokuwa walimu. Kwa upande wake, Hasina aliyekuwa Katibu muhtasi wa Katibu Mkuu wa chama cha wafanyakazi huko Zanzibar, anawakilisha wanawake Waafrika waliobahatika kupata elimu na kujiunga na kazi za kiofisi. Hata hivyo, kazi hii ni ya kisaidizi pia. Mwandishi vil vile amewahuishwa wanawake wawili na kazi ya utafsiri. Wanawake hawa ndio wanaotafsiri hotuba ya mkuu wa Chuo Cha Bernau, Ujerumani ambapo Adam alikuwa akisomea. Mmoja wao alitafsiri kwa Kiingereza na mwingine kwa Kifaransa (uk 472). Wanawake hawa ni wasaidizi wa Mkuu wa Chuo hicho. Kazi ya kusimamia Chuo Kikuu inayohusishwa na mwanamume inaonekana kumpa hadhi mwanamume huku kazi ya kutafsiri ikimpa mwanamke hadhi ya chini. Kianthropolojia na kihistoria, wasimamizi wa taasisi za kielimu walikuwa wanaume. Kwa misingi hii, mwandishi amewawasilisha wanaume na wanawake katika hali yao ya uhalisi katika kipindi hicho kihistoria.

Mwandishi amewawasilisha wanawake wa Kigorolana kama wafagizi (uk 421). Wafagizi hawa wamesimama nje ya maghala ya vyakula wakisubiri wachukuzi wamalize kutoa magunia yao wafagie. Katika muktadha huu, wachukuzi wamewasilishwa matumbo yakiwa wazi, wakitokwa na jasho kutokana na kazi ya kuburura marikwama yaliyosheheni magunia. Kazi ya kufagia si nzito kama ilivyo ya kuvuta marikwama. Kwa misingi hii, wanawake kuhusishwa na ufagizi huku wanaume wakihuhsishwa na uvutaji marikwama, ni uhalisia wa maisha kwamba, wanawake kutokana na hali zao kimaumbile, huhusishwa na kazi zisizohitaji nguvu kama za wanaume. Hata hivyo, katika kuchunguza kazi za wahusika hawa wa kike, ni za kiusaidizi tu. Katika miktadha hii, daktari ana hadhi na mamlaka kuliko mwuguzi, mkuu wa Chuo ana hadhi kuliko watafsiri naye katibu mkuu wa chama cha wafanyakazi kule Zanzibar ana cheo na mamlaka juu ya katibu muhtasi. Huku si kuwanyima wanawake hadhi au kuwaonea, bali ni uhalisi wa maisha yao kihistoria na kianthropolojia.

2.5.2.2 Muktadha wa kibiashara

Katika muktadha huu, mwandishi amewahuhsisha wanawake kwa ufinyu na biashara. Kwanza, katika safari ya kuelekea Kosti, wanaume na wanawake wamehusishwa na biashara ya ndizi mbichi. Biashara hii inafanyika kijijini katika kituo kidogo cha meli. Wanawake hao wamewasilishwa kihalisi. Wanaiza bidhaa kwa wasafiri (uk 224) Uhusishwaji huu ni uhalisi wa maisha ya wanawake kiuchumi. Kihistoria, katika vituo vya treni na bandari, walikuwepo wauza bidhaa hasa vyakula vilivyo tayari kuliwa ikizingatiwa kwamba, wasafiri walichukua muda mrefu katika safari hizo. Kwa mfano, meli hii ilipokuwa ikielekea Kosti, ilichukua siku tatu kufika katika kituo cha kwanza. Wasafiri walihitaji kupumzika. Waliokuwa wameishiwa na chakula walihitaji kununua vyakula vingine. Bidhaa zilizokuwa zikiuzwa na wanawake hao

zilitoka mashambani kwao. Wanawake wamehusishwa na biashara ndogo ndogo zinazofanyiwa katika mazingira ya kijijini. Suala hili lina mahusiano na nadharia ya anthropopolojia kwamba, wanawake kihistoria walihusishwa na kazi ndogo ndogo zilizofanyiwa katika mazingira kinyumbani kwa kuwa, wana majukumu ya kimsingi kama kulea watoto ambayo yanawazuia kufanya biashara nje ya miktadha ya kinyumbani.

Binti wa Kisudan ni mkazi wa Khartoum ambaye anafanya biashara ya kuuza pombe ya kienyeji na ukahaba. Katika mazingira haya mwandishi ameonyesha mandhari ya ulevini. Mtu wa kwanza ambaye mwandishi anakutana naye alikuwa mlevi. Mlevi huyo alikuwa akiyumbayumba nje ya nyumba ya udongo. Ndani ya chumba hicho, palikuwa na Binti wa Kisudan aliyekuwa akiwauzia walevi pombe ya kienyeji. Adam alipoingia binti yule alimshika mkono na kumuongoza hadi chumbani. Adam alilipa shilingi ishirini kisha akashiriki ngono na binti huyo kabla ya kuondoka na kurejea katika makao yao ya muda, nje ya mji wa Khartoum (uk 331). Mandhari haya yanayofanyiwa biashara ya ukahaba na uuzaji wa pombe ya kienyeji yanaonyesha hali za kiuchumi za wakazi wake. Nyumba ni za udongo. Moshi unavuka kwa kuwa upishi wao unatumia kuni. Wakazi wanaelezwa kama vibarua wanaotafuta riziki mchana kutwa. Kwa upande wa kulia, pana nyumba nzuri ambazo mwandishi anasema ni za watu waliotulia kwa starehe na raha, kinyume na upande wa kushoto ambapo maisha yalionekana kama yanayochemka.

Katika muktadha wa kibiashara tunaweza kumweka Mariana pia. Mariana alikuwa mpenzi wa Abdo. Abdo alikuwa mmiliki wa mabasi mawili, basi moja likiitwa *Mawingo* ambapo Adam alipata kazi kama kondakta, na la pili liitwa *Kuiva*. Adam alipatana na Mariana mara ya kwanza

chumbani mwa Abdo. Mara ya pili alipatana naye katika baa akiwa na Abdo. Alikuwa amejifunga kitambaa cha feruzi kichwani na alivalia kanzu chafu ya manjano (uk 126) Mwandishi anaeleza kwamba, Mariana hakuwa mkazi wa pale Bungoma. Mara ya tatu alipomwona Mariana ndani ya basi asubuhi akiwa jinsi alivyokuwa usiku uliotangulia. Hii ina maana kwamba, Mariana alikesha katika baa. Basi lilikuwa likielekea Kakamega. Mariana alishuka katika kijiji kimoja.

Mwandishi anaeleza;

Pale basi liliposimama tulikuwa kama tuliomezwa na pori la miti mirefu iliyozinguka kijiji kile. Kijiji chenyewe kilikuwa na vibanda vichache vyta misonge, kimoja hapa kingine kule (uk 131).

Kutokana na maelezo haya inaeleweka kwamba, Mariana hakuwa mkazi wa mjini. Alikuwa akiingia mjini kutafuta riziki kwa kufanya ukahaba kutokana na hali yake ya kiuchumi. Kijiji anakotokea kimewasilishwa kama cha watu maskini. Mariana alipokutana na Adam kituoni Kakamega, mavazi aliyovaa yalimbadilisha kiasi kwamba, Adam hamtambui. Kinyume na ile kanzu chafu, siku hiyo alivaa kanzu iliyowacha maziwa nje, iliyombana kiunoni sawasawa na mkanda mwekundu. Alionekana kama nguva. Nywele zilichanwa kwa mbele na kuwekwa shore kubwa juu ya paji lake. Alikuwa ameurashia uso wake poda iliyoufanya ung'are. Midomo alipaka rangi nyekundu. Alivalia viatu vyeusi vyta visigino badala ya vile vyta mipira ya gari alivyovaa awali. Alibeba mkoba mweusi ulioning'inia kwenye nyonga. Alipozungumza na Adam, alimweleza wazi kwamba, hakuwa ameolewa, hakuwa na mtoto wala hakuwa na haja ya mume, alichotaka ni mwanamume.

Uhusikaji wa Binti wa Kisudan na Mariana waweza kuelezwa kihistoria ili kuafiki uhalisi wa maisha kiuchumi wakati wa ukoloni. Wanawake waliojihuisha na uuzaji wa pombe ya kienyeji na ukahaba ni wale waliokumbwa na umaskini. Umaskini ulisababisha hali duni za kiuchumi. Kulikuwa pia na ukosefu wa ajira katika nchi nyingi Afrika Mashariki, kabla ya uhuru. Watu walihamia mijini ili waboreshe maisha yao. Walikumbana na changamoto kama kugharamia chakula, ulipaji nyumba na matibabu mionganoni mwa nyingine. Kwa misingi hii, mwandishi amemwasilisha mhusika huyu ili kuakisi ukweli kihistoria na uhalisi wa maisha ya wanawake. Hali za kiuchumi na mabadiliko kutokana na ukoloni yamechangia pakubwa uwasilishwaji wao kitabia. Kwa misingi hii, Mariana na Binti wa Kisudan sio makahaba, sio chanzo cha maovu yote wala sio vyombo vyta kuwastarehesha wanaume, kama baadhi ya watafiti wa awali walivyowatathmini wanawake katika mazingira ya ulevi na starehe.

2.5.3 Mazingira ya Kielimu

Wanawake waliowasilishwa katika mazingira ya kutafuta elimu ni wachache. Pana wanafunzi wawili, mwalimu mmoja na watafsiri wawili. Zainabu ni mwanafunzi wa Zanzibar, anayesomea katika Chuo Kikuu cha Khartoum. Naajat ni Suriama, (baba ni Mzungu na mama ni Mmisri) anasomea katika Chuo Kikuu cha Kairo. Pana mwanamke Mjerumani ambaye alikuwa mwalimu wa lugha ya Kijerumani katika chuo cha Bernau, huko Ujerumani. Zainabu na Naajat ndio wanawake pekee wanaohusishwa na elimu ya Chuo Kikuu. Wanafunzi wengine wote waliosawiriwa ni wanaume. Zainabu anajuanana na Adam na wenzake wakiwa katika harakati za kutafuta malazi huko Chuoni. Uhusikaji wa Zainabu unaakisi ukweli kwamba, wakati huu idadi ya wanawake katika vyuo ilikuwa ndogo sana. Zainabu anawakilisha wanawake wachache wa Kiafrika ambao walikuwa katika taasisi za kielimu. Mahusiano kati ya uhusikaji wa Zainabu

katika taasisi ya kielimu na nadharia ya anthropolojia ni kwamba, elimu kwa wanawake Waafrika haikutiliwa mkazo kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na hata miaka kadhaa baada ya ukoloni. Kuhusika kwa Zainabu kama mwanamke wa pekee katika Chuo ni suala la kihistoria. Miller (1990:255) anaeleza kwamba elimu kwa wanawake barani Afrika ilicheleweshwa kutokana na itikadi na mifumo pamoja na asasi mbali mbali za kijamii. Itikadi iliyokuwepo katika jamii nyingi za Kiafrika ni kwamba, elimu ya mwanamke haikuwa na faida kwani waliishia kuolewa. Tamaduni nyingi zilimtayarisha mwanamke kuwa bibi, mzazi na mlezi, bali si mchuma riziki. Kwa misingi hii elimu ya wanawake ilipuuzwa. Mwandishi ameibua ukweli huu kihalisia anapohusisha idadi ndogo ya wanawake katika muktadha wa wanafunzi. Uhusikaji wa mwalimu wa lugha ya Kijerumani na utafsiri ni uhalisi kwamba, kazi hizi zilihusishwa na wanawake zaidi kuliko wanaume. Wanaume hawakuhusishwa na kazi ya ualimu. Walihuushwa na kazi zilizochukuliwa kuwa na hadhi ya juu kama marubani, madaktari mionganini mwa nyagine. Kwa misingi hii, mwandishi katika *Mbali na Nyumbani* hajawatenga wanawake katika miktadha ya elimu, bali ni uhalisi kianthropolojia na kihistoria.

2.5.4 Mazingira ya Kiburudani

Mazingira ya kiburudani katika *Mbali na Nyumbani* yamejitokeza katika hoteli na baa. Wahusika wamewasilishwa katika mazingira hayo kwa njia ya starehe na burudani. Katika (uk 114) baa ya Noorali Sidi, mfanyabiashara wa Kihindi, palikuwa na kijana aliyekuwa akipiga gitaa na kuimba nyimbo za Jean Mwenda Bosco na Edward Masengo. Kijana huyo alikuwa kivutio kikubwa kwa wateja. Mwandishi anaeleza jinsi wanawake na wanaume walivyokuwa wakijiburudisha kwa vinywaji na muziki. Mwandishi anasema kwamba, aliingia katika baa hiyo usiku ili aweze kuyapa kisogo maonyo ya Bwana Bakari kwamba kwamba, akishazoea mji wa Bungoma

hataweza kuondoka, ataselelea kwa kuwa ulikuwa mji wa raha. Mwandishi anasema hakuwa mnywaji wa pombe lakini alifurahia kuona watu wakicheza na kutimka ili wasahau dhiki zao na waburudishe roho zao. Mwandishi anaeleza kwamba, katika baa hiyo, wapenzi waliokwishachukuliwa na nishai za ulevi walikuwa wakikumbatiana na kubusiana jaraha. Abdo mmiliki wa la *Mawingo* alikuwa akitafuna mirungi na kuvuta sigara.

Kwingineko, katika klabu ya wanafunzi, chuoni Khartoum, mwandishi amemwasilisha Zainabu. Anaeleza kwamba Zainabu hakuwa na mazoea ya kuingia kilabuni humo. Wahusika waliomo humo ni wanaume ambao wanajiburudisha kwa muziki na vinywaji (uk 227) Mhusika mwingine amejitokeza katika hoteli ya *New Stanley* akiwa na mpenzi wake aliyezungusha mkono wake kiunoni huku wakibusiana midomo kama nyuni (uk 447). Vile vile hotelini Zurich, wapenzi walioonekana kunogewa na mahaba walionekana wamekaribiana huku wakigusananisha pua zao. Muziki wa bashraf ulikuwa ukisikika kwa mbali. Kuwepo kwa wahusika wa kike katika mazingira ya kiburudani kunaelezeka kihalisia kwamba, katika maeneo ya mijini ilikuwa kawaida kupata wanawake na wapenzi wao katika baa wakicheza na kusikiza muziki kama ilivyo hata sasa. Kuwahuisha wanawake na wanaume ni uhalisia kwamba, kukamilika kwa mapenzi kunahuisha jinsia zote. Kwa misingi hii, wanawake hawa sio makahaba kama inavyoweza kutathminiwa na baadhi ya watafiti.

2.6 Hitimisho

Katika sura hii muhtasari wa *Mbali na Nyumbani* umetolewa na suala la wahusika na mandhari limeshughulikiwa ili kuiwekea misingi mijadala ya utafiti. Aina za wahusika katika fasihi zimeangazwa. Wahusika wa kihistoria, kihalisia na kisaikolojia wamemejadiliwa kwa kuwa hizo

ndizo kategoria za wahusika zinazojitokeza katika *Mbali na Nyumbani*. Wahusika wa kihistoria ni pamoja na Jomo Kenyatta, Oginga Odinga, Tom Mboya na Dedan Kimathi. Wahusika halisi ni pamoja na Shafi Adam Shafi, mwandishi wa *Mbali na Nyumbani*, Fatma (mkewe) Laila (bintiye) mionganoni mwa wengine. Wahusika wa kisaikolojia wamehusishwa katika fikra, ndoto na mawazo ya wahusika wengine. Mfano mzuri ni mama yake Shafi. Shafi anapouqua anamwaza mama yake jinsi angemwuuguza. Katika ndoto zake, Shafi, katika ndoto zake anawahusisha baadhi ya wanawake kama, Nisreen na Halima. Hisia na matamanio yake yanaonyesha uhusikaji muhimu wa wanawake kisaikolojia.

Mandhari yanayojitokeza katika *Mbali na Nyumbani* ni ya Kijiografia, kihistoria na kidhanifu. Mwandishi anatoka Zanzibar na kuelekea Kairo. Anafika Aden na kurudishwa hadi Mombasa. Zanzibar, Kairo, Aden na Mombasa ni mandhari halisi ya kijiografia katika bara la Afrika. Matukio yanatokea katika mandhari halisi ya kihistoria kama mafunzo ya kijeshi ambayo Adam na wenzake wanapata huko Kairo. Mandhari ya kidhanifu yanajitokeza katika fikra na ndoto za wahusika na hata kuitia mazungumzo yao. Kwa mfano, Adam anajenga picha ya Kairo anayoitamani kabla ya kufika huko na kuonyesha hisia na matamanio yake.

Wahusika wamebainishwa katika mazingira na miktadha mbali mbali. Katika mazingira ya kijamii, wanawake wamewasilishwa katika muktadha ya kinyumbani na muktadha wa usafiri. Majukumu ya kimsingi wanayotekeleza katika miktadha hiyo miwili ni uzazi, ulezi na upishi. Wanaume waliowasilishwa katika muktadha wa kinyumbani na safari hawatekelezi majukumu yanayoteklezwa na wanawake.

Katika mazingira ya kiuchumi, wanawake wamewasilishwa kaatika muktadha wa kikazi na muktadha wa kibiashara. Wanawake katika miktadha hiyo ni wahudumu na wapokezi katika ofisi na hoteli. Kazi zao ni za kiusaidizi tu. Wanaume katika miktadha ya kikazi ni marubani, mabalozi, madaktari, wasimamizi wa vyuo na mawakala wa meli. Wanaume wamehusishwa na kazi ya kuburura marukwama katika bandari huku wanawake wakiwa wafagizi tu. Tumeona kwamba huu ni uhalisia wa maisha ya wanawake kihistoria.

Katika mazingira ya kielimu, wanawake wamewasilishwa kwa ufinyu katika elimu ya Vyuo Vikuu. Uwasilishwaji huu ni uhalisi wa maisha ya wanawake katika shughuli za kielimu. Kutokuwepo kwa wanawake katika elimu ya msingi na ya sekondari katika *Mbali na Nyumbani* kumetokana na ukweli kwamba, elimu ya Kimagharibi ilipokelewa kwa kupeزوا kwa wasichana na kuhimizwa kwa wavulana kujiunga na taasisi za kielimu.

Katika mazingira ya kiburudani, wanawake wamewasilishwa kihalsia katika baa wakinywa pombe na kujiburudisha na wapenzi wao. Ukweli ni kwamba, wapo na walikuwepo wanawake wa aina hiyo walioingia katika mazingira ya kiburudani jioni baada ya kazi za mchana ili kujiburudisha na pengine kuchuma hela kutoka kwa wapenzi wao.

Imebainika kwamba wanawake wamewasilishwa zaidi kwa majukumu ya kinyumbani ambayo baadhi ya watafiti hudai ni kuwadunisha, kuwaonea, kuwadhulamu na kuwanyima hadhi na nafasi wanawake au kuwatenga.

SURA YA TATU

DHANA YA UTOKUWEPO: KUBAINISHA MAZINGIRA NA MIKTADHA AMBAMO

WAHUSIKA WA KIKE HAWAPO KATIKA *MBALI NA NYUMBANI*.

3.0 Utangulizi

Katika sura ya pili, tulibainisha kuwepo kwa wahusika wa kike katika mazingira na miktadha mbali mbali kimajukumu. Katika sura hii, tutabainisha kutokuwepo kwa wahusika wa kike katika mazingira na miktadha fulani kama inavyojitokeza katika *Mbali na Nyumbani*. Ubainishaji huu unalenga kuuwekea msingi mjadala wa utafiti kuhusu sababu za kutokuwepo kwao katika mazingira na miktadha hiyo. Kutokuwepo kwa wahusika wa kike kwa ufinyu katika mazingira na miktadha fulani pamoja na kutokuwepo kwao katika miktadha mingine kunahusiana na anthropolojia ya kiutamaduni kwamba, uwasilishwaji wao kwa ufinyu ni matokeo ya ucheleweshwaji wa kujumuishwa katika harakati za kijamii na sio kunyimwa nafasi, ilhali kutokuwepo kwao kabisa katika miktadha mingine ni ukimya unaoweza kuashiria kuwepo kwao na sio kutengwa kimakusudi.

3.1 Dhana ya kutokuwepo kwa wahusika wa kike

Dhana ya kutokuwepo katika utafiti huu itatumwa kuelezea mazingira na miktadha fulani ambamo wahusika wa kike wamewasilishwa kwa ufinyu na miktadha mingine ambamo hawajawasilishwa kabisa. Kwamba, matukio, shughuli, majukumu na mambo yote katika mazingira na miktadha fulani yamehusishwa zaidi na wanaume kuliko jinsi wanawake walivyohusishwa. Kwa upande mwengine matukio, shughuli, majukumu na mambo yote katika miktadha mingine yamehusishwa na wanaume bila kuwahuisha wanawake. Kuwepo kwa

wanawake kwa ufinyu katika mazingira na miktadha fulani kunahusiana na majukumu waliyopewa katika tawasifu. Kutokuwepo kwao kabisa katika mazingira na miktadha mingine kunahusiana na majukumu yaliyopewa wahusika wa kiume. Mahusiano kati kutokuwepo kwa wanawake katika mazingira na miktadha hiyo na masuala ya kimsingi ya utafiti ni kwamba kianthropolojia, uwasilishwaji wa wanawake kwa ufinyu ni matokeo ya ucheleweshwaji kwa maana ya kutojumuishwa au kutoshirikishwa katika harakati za kijamii, ilhali kutowasilishwa kwao katika miktadha mingine ni ukimya, lakini ukimya ambao si lazima uwe na athari hasi. Utokuwepo wa wahusika wa kike umejitokeza katika mazingira ya kijeshi, mazingira ya kisiasa, mazingira ya kidini, miktadha ya uhamaji na miktadha ya kikazi.

3.2 Mazingira ya kijeshi

Jeshi ni jumla ya askari wanaaoajiriwa kulinda nchi, wananchi na mali yao. Laweza kuwa jeshi la ulinzi, jeshi la polisi, jeshi la anga, jeshi la wanamaji miongoni mwa mengine. Shughuli zinazofanywa na wanajeshi huchukuliwa kuwa ngumu na zinazohitaji nguvu nydingi, uvumilivu na tajriba pana. Kabla ya majilio ya wakoloni, jamii nydingi za Kiafrika ziliwu na mifumo yao ya kitawala. Jamii hizi ziliwu na mipangilio yao ya ulinzi ambayo kwa kiasi kikubwa iliwashirikisha wanaume. Wanawake hawakuhusika katika shughuli za ulinzi. Wanaume walipitishwa katika hatua fulani za kimafunzo kabla ya kutawazwa kama walinzi wa jamii zao. Mbali na jukumu la ulinzi, wanaume pia walihitajika kuvamia jamii jirani kwa madhumuni ya kuwashika majirani zao mateka na kuwanyang'anya mali zao kama njia ya kilimbikizia utajiri hasa wa mifugo. Wanawake katika jamii nydingi walihitajika kukaa nyumbani, mahali ambapo palionekana salama kwao. Vinginevyo, wanawake walichukuliwa kuwa jinsia dhaifu isiyoweza kuvumilia matatizo wala kukabiliana na hatari za kivita. Vile vile, jukumu la uzazi na malezi

lilionekana la kimsingi kwao. Hawakukubaliwa kwenda vitani au hata kushiriki katika mapigano dhidi ya adui. Jamii nyingi ziliwateua wanaume ambao wangebaki nyumbani wakiilinda jamii yao wakati wenzao walipokwenda vitani. Katika *Mbali na Nyumbani*, kuna mazingira na miktadha tofauti tofauti ya kijeshi. Katika miktadha hiyo, wahusika wa kike hawajahusishwa. Mahusiano kati ya kutokuwepo kwa wahusika wa kike katika mazingira na miktadha ya kijeshi na nadharia ya anthropololojia ni kwamba, wanawake katika kipindi hicho cha kihistoria, (kipindi kinachoangaziwa na mwandishi) hawakukubaliwa kushiriki katika shughuli zilizokuwa ngumu na zilizofanyiwa katika mazingira yasiyo salama kama ya kivita. Kwa misingi hii, mwandishi hajawawasilisha wahusika wa kike katika mazingira ya kijeshi kama askari polisi, askari jeshi na wapiganiaji uhuru. Huo ndio uliokuwa uhalisia wa kihistoria na masimulizi ya mwandishi yanaakisi uhalisia huo.

3.2.1 Askari polisi.

Askari polisi na askari jeshi katika *Mbali na Nyumbani* wamepewa majukumu mbalimbali. Askari polisi wamehusishwa na majukumu ambayo hayahitaji bunduki. Wao wanatumia marungu au fimbo kulinda usalama katika mazingira yao ya kikazi. Askari jeshi wamehusishwa na majukumu yanayohitaji bunduki. Katika mazingira na shughuli zao wao wamebeba bunduki na silaha nyinginezo za kivita au kiulinzi. Katika (uk 75 na 201) askari waliokagua stakabadhi za malipo ya *kodi ya kichwa* wanaelezwa kushuka kutoka kwa karadinga kwa kishindo. Askari hao walikuwa wamebeba rungu kila mmoja akiwa tayari kuwaadhibu wasafiri ambao hawakuwa wamelipa kodi ya kichwa. Mbali na kudhulumiwa kwa abiria, walitusiwa na kupigwa makofi mbele ya wake zao na watoto wao huku wakifungwa kamba mikononi na miguuni kama watumwa wanaopelekwa mnadani. Waliwazuilia wale ambao hawakuwa wamelipa na

kuwaruhusu tu wale waliokuwa wamelipa waendelee na safari. Askari hawa hawakuwa na utu hata kidogo. Kazi ya kukagua kodi ya kichwa kwa wasafiri waliokuwa wakiingia melini inaonyeshwa kuwa ngumu. Kwanza, kulingana na maelezo ya mwandishi, meli ilikuwa imejaa tele (uk 79) Walipofika Pakwach, wasafiri waliongezeka. Kukagua stakabadhi ya kila msafiri haikuwa kazi rahisi. Kachero anayehusika na kazi ya kuwasaka waliokuwa wakitaka kuvuka mpaka kwa njia ya magendo anajifanya kuwasaidia kisha baadaye anawasaliti kwa askari wa mpakani kuingia Sudan (uk 85). Hii ni kazi inayohitaji ukakamavu na ujasiri. Iliwahitaji makachero wazungumze na wasafiri na kuwafuata hadi mwisho wa safari yao ndipo wawakamate. Kutokuwepo kwa wahusika wa kike ambao ni askari wa kukagua kodi kunaweza kuelezwa kuwa ni uhalisi wa kihistoria na kianthropolojia.

Katika kituo cha kuvuka mpaka cha Nimule, kuingilia Sudan, mwandishi na mwenzake wanakutana na askari polisi wawili. Walikuwa wamevalia sare ya polisi wa Sudan, suruali ya kipande ya kaki na shati la kaki la mikono mifupi. Kofia walizovaa zilikuwa za pama zimepindwa mkono wa kulia na kuchomekwa ua jeusi la plastiki pembeni. Mkuu wa kituo anawataka waonyeshe pasipoti na viza zao. Walikuwa na pasipoti lakini hawakuwa na viza. Mkuu wa kituo aliwatia mbaroni na kuwaweka chini ya ulinzi wa polisi hadi kituo cha Gulu. Kachero aliyewasaliti aliandamana nao hadi Gulu. Kachero huyo aliwasukuma wakishuka basini na kuwatanguliza hadi kituoni. Kituoni palikuwa na askari wawili. Waliwaamrisha waketi sakafuni mbele ya meza ya mapokezi baada ya kunyang'anywa pasipoti zao. Ndani ya kituo palikuwa na mahabusu, wezi na wahalifu waliokuwa chini ya ulinzi mkali.

Mwandishi anaeleza;

Tulikaa tu tukiangalia vioja vya watu waliokuwa wakiletwa kituoni pale. Wengine walikuwa wamepigana mapanga huko walikotoka, wezi wa ng'ombe au walevi. Hapo palikuwa mahali pa kelele, vurugu na shari tupu. Tulikesha pale katika hali ile ya mtafaruku na wasiwasi mpaka kulipokucha. Usiku wote usingizi wetu ulikuwa ukikatika katika ijapokuwa tulikuwa tumechoka taabani (uk 88)

Maeleo haya yanadhihirisha kwamba, kazi ya askari ni ngumu na inahitaji nguvu na ukakamavu. Askari katika kituo hicho walikuwa wakiwalinda mahabusu ambao kwa njia moja au nyingine wangkuwa hatari kwa usalama wao. Kazi hiyo waliifanya kwa zamu. Askari wote katika kituo kile walikuwa wanaume. Mkuu wa Kituo alikuwa mzungu (uk 94) Kama wanavyomwita, Bwana Mkubwa aliamrisha wapelekwe Hotelini Gulu wakae mpaka wakati watakapopata safari ya kurudi Kampala wakatafute viza ya kuingia Sudan. Katika kituo kidogo cha polisi, lango la kuingia Juba, palikuwa na askari mmoja ambaye alikuwa na majukumu matatu. Alikuwa ndiye Afisa wa Uhamiaji, Afisa wa Forodha na polisi wa zamu. Baada ya kuwataka waeleze kama walikuwa na pesa za kutosha kuwakimu muda wataoishi Sudan, alikagua pasi zao na kuwatakia mema. Kazi hizi ni ngumu kufanywa na mtu mmoja ikizingatiwa kwamba wasafiri waliotaka kuvuka mpaka wangkuwa wengi wakati mwingine na vile vile kituo hicho kilitumiwa mchana kutwa usiku kucha.

Kwingineko, safari ya meli iliyotoka Wadi Halfa kwenda Shellal, abiria waliingia melini huku askari watatu wa bandarini walioshika fimbo mikononi wakihakikisha kwamba hakuna ye yote aliyevunja foleni. Walikuwa wakali kwa ye yote aliyefanya hivyo. Askari hao walikuwa wanaume. Mwandishi anapopitia Gulu kwa mara ya pili, aliwapata askari na makachero katika kituo cha polisi. Askari hao hakuva sare ya askari. Walikuwa katika kikosi maalum cha

makachero waliokuwa wakishughulikia usalama wa utawala wa Malkia (uk 209) Katika miktadha hii hapakuwa na askari wanawake. Kutokuwepo kwao kunaakisi ukweli kihistoria kwa kuwa hivyo ndivyo ilivyokuwa hali ya maisha yao katika jamii ya mwandishi.

Kwenye basi la '*Kuiva*', ambako mwandishi alikuwa kondakta, mionganoni mwa abiria palikuwa na askari wa magereza aliyefuatana na mahabusu huku wote wawili wakiwa wamejifunga kikuku kimoja mkono wa kushoto. Sababu ya kujifunga ikiwa kwamba, askari hakutaka mahabusu yule atoroke. Hii ni hatari kubwa sana kwa askari mwenyewe kwani kwa bahati mbaya mahabusu akivunja vikuku, itabidi askari akimbizane naye. Hii ni kazi ngumu na yenyе hatari kubwa. Katika muktadha wa askari wa magereza, hakuna wahusika wa kike. Kutokuwepo kwao kunaelezeka kihalisia kuwa, huu ni uwasilishaji wa wahusika wa kweli kihistoria kuliko wahusika wa kuelezeka kiusawiri.

3.2.2 Askari Jeshi

Katika jengo la Wizara ya Mambo ya Nje, Khartoum, mwandishi anaeleza kwamba, jengo lile likiliwa na askari jeshi waliojizatiti kwa mirau mizitomizito. Yeye na wenzake hawakuwa na hofu wala shaka kulala nje ya jengo hilo kwa kuwa usalama wa kutosha ulikuwepo (uk 241). Anaeleza kwamba, walipotakiwa na afisa wa Ubalozi wa Sudan wapeleke pasi zao, waliziendea katika jengo hilo la Wizara ya Mambo ya Nje. Waliwakuta askari jeshi waliobeba bunduki mabegani kama kawaida yao, wakiwa makini na tayari kukabiliana na yejote aliyeingia kule. Walikuwa askari wasiotaka mzaha wala masihara (uk345) Ofisi za Wizara ya Mambo ya Nje kawaida huwa na shughuli nyingi kama kupokea wageni, kutoa msaada kwa wageni na kutatua shida za wageni hasa kuhusu uhamiaji na shughuli nyingine za kiserikali. Jengo hili pia

liliwa na ofisi ya uhasibu. Baada ya mwandishi na wenzake kurudishiwa pasi zao, waliagizwa kwenda kwa mhasibu ili wapewe pesa za kugaramia safari yao. Walipopanda kwenye ghorofa ya kwanza, walipata askari jeshi wawili waliokuwa na bunduki katika eneo la mapokezi (uk 348) Kubeba bunduki kila wakati mchana kutwa, usiku kucha ni kazi inayohitaji mtu mwenye nguvu, mvumilivu na jasiri kukabiliana na hatari yoyote. Mwandishi hajawasilisha wahusika wanawake katika muktadha huu. Katika kipindi hicho cha kihistoria, wanawake hawakuruhusiwa kushiriki katika kazi zilizohitaji silaha au zilizokuwa katika mazingira ya hatari. Kutokuwepo kwa askari wanawake katika muktadha huu kunaakisi ukweli huu na hakupaswi kueleze ka kiusawiri.

3.2.3 Wapiganiaji uhuru

Dedan Kimathi, kiongozi wa Mau Mau alikuwa akipigana na Waingereza kwa silaha anuai. Mau Mau ni kundi ambalo liliwa limechoshwa na mazungumzo kuhusu upiganiaji uhuru na likaamua kuingia vichakani na kutumia silaha ili kupigana na Waingereza. Waingereza waliliita kundi hilo magaidi lakini wananchi waliwaita wapiganiaji uhuru. Mwandishi anaeleza jinsi watu walioshukiwa kuhusika na Mau Mau walivyokamatwa na kuwekwa katika kambi maalum za mateso. Hakuna wanawake katika muktadha huu.

Mwandishi na wenzake walipofanikiwa kuingia Kairo, nchini Misri, waliingia kambini kupata mafunzo ya kijeshi ili waweze kupigania uhuru katika nchi zao. Mafunzo haya yanafanywa kisiri. Walijiunga kambini wakiwa tisa; Shafi, Abdalla, Hemedi, Mansour, Shaaban, Ali Sultani, Nassoro, Mohammed na Ahmed. Gari lililowabeba liliendeshwa na kijana aliyevalia sare za kijeshi (uk 389). Kulingana na maelezo ya mwandishi, kijana huyu alikuwa kurutu. Kambi ya kijeshi ilikuwa jangwani mbali na jiji la Kairo. Iliwachukua takriban saa nzima kufika kule.

Walifika mahali palipokuwa na kizuizi kilicholindwa na askari wawili walioning'iniza bunduki mabegani. Kambi ilikuwa na mabanda ya mabati ambayo yalitumika kama makazi. Katika moja ya mabanda yale walikaribishwa na mwanaume aliyevalia kijeshi. Mahali walipokuwa wamesimama palikuwa na upemo wa baridi uliomfanya Shaaban alalamike. Amri jeshi alitokeza katika banda na kuwataka waingie ndani. Walitahadharishwa kuwa pale palikuwa ni eneo la kijeshi. Utaratibu wa maisha ya kambini kama kutii amri zinazotolewa na wakubwa ulisisitizwa. Walionya kwamba yule angepinga amri ya mkubwa angeiona dunia juu chini, chini juu. Luteni Sameer alipewa jukumu la kuwafunza. Alianza kwa kuwaeleza utaratibu wa pale kambini. Kuamka saa kumi na moja. Kuingia katika mazoezi. Kunywa chai na baadaye kuingia mafunzoni.

Mafunzo yalianza hapo hapo. Walijipanga mstari mmoja na kukaza miguu huku wakifuatana sanjari kwa kubandika na kubandua miguu, kushoto na kulia. Baada ya kupewa sare waliruhusiwa kupumzika. Waliagizwa kusafisha banda lao ila hawakupewa ufagio na hawakujuwa wangeomba nani na wapi. Mwandishi anaeleza;

Kambi ile haikuwa kambi ya makazi ya wanajeshi ambayo tungelikuwa na ujirani wa majirani kuazimana kinu, mchi, chungio au ufagio. Hiyo ilikuwa ni kambi ya kivita, maskani ya wapiganaji tu. Kwa hivyo hatukuwa na jirani ambaye tungekwenda kwake kuazima chochote (uk 397)

Maelezo haya yanaashiria maisha magumu ambayo mwandishi na wenzake walikumbana nayo katika kambi ya mafunzo ya upiganiaji uhuru. Fauka ya hayo, eneo la kambi lilikuwa ni jangwa. Kawaida ya jangwa huwa na upemo wa baridi na joto kali sana. Mbali na hayo, chakula walichopewa kilikuwa ni mikate na maharagwe tu. Walipoingia katika mafunzo ya vitendo, Mansour alijeruhiwa kwa kukosa kutii amri (uk 409) Katika muktadha huu, mwandishi

hajawasilisha wahusika wa kike. Haya ni mazingira ambayo kihistoria na kianthropolojia yalikuwa bado hayajawatambua wala kuwahusisha wanawake.

Tarehe 19 Agosti, 1960, mwandishi, Hussein na Suleiman walifika katika uwanja wa ndege wa *Shonefeld* Ujerumani. Walilakiwa na mwenyeji kwa gari lililowapeleka chuongi, Bernau. Siku hiyo dunia ilikuwa katika hali ya wasiwasi kutokana na vita baridi kati ya Wamerikani na Warusi. Mwandishi anaeleza kwamba katika jiji la Berlin, vifaruh ya Wamerikani vilikuwa vimekabiliana uso kwa uso na vifaruh ya Warusi. Vya Wamerikani vilikuwa upande mmoja na vya Warusi vilikuwa upande mwingine wa Lango la *Brandenburg*, katika barabara ya *Unter den Linden*. Vita baridi vilikuwa si baridi tena. Wakazi wa jiji la Berlin walilala wakiliacha jiji likiwa moja na kuamka kulipata jiji limegawika upande wa Mashariki wenyeji wakiwa ndani nao wa upande wa Magharibi wakiwa nje ya ukuta. Ukuta huu ulichukua umaarufu mkubwa kutokana na muda wa usiku mmoja wa kuujenga (uk 463) Mwandishi na wenzake walishangaa kusikia masimulizi ya mwenyeji wao. Katika Chuo chao, Bernau, nje ya uwanja, hawakuona dalili ya wanafunzi walioshika vitabu na makabrasa kwapani. Mwandishi anaeleza;

Walikuwa vijana wakakamavu waliovaa sare za kijeshi za rangi ya kijani kibichi. Walikuwa wamebeba mirau mabegani huku wakicheza gwaride, wakiimba kwa jazba na hamasa (uk 464)

Mwandishi alishangaa kwamba, wafadhili wake walikuwa wamemlaghai na kumrudisha katika mafunzo ya kijeshi. Hussein na Suleimani nao pia walitazamana kwa mshangao. Mwenyeji wao aliwatoa hofu kwa kuwaeleza kwamba, hicho kilikuwa chuo cha kutoa mafunzo kwa wanamgambo. Chuo hicho kilikuwa cha wafanyakazi, tabaka lililokuwa likitawala nchi ile. Wote waliokuwapo walikuwa wanafunzi ambao wakati ule walikuwa wakipokea mafunzo ya mgambo

ili wawekwe tayari kupigania nchi yao ambayo ilikuwa katika hali mbaya ya kisiasa. Katika muktadha huu, hakuna wanawake wanaohusika kama wanamgambo. Kutokuwepo kwao katika miktadha hii ni uhalisia wa kihistoria na kianthropolojia na ambao unaweza kufasiriwa kuwa ukimya, kwa maana kwamba kufikia wakati huu, wanawake hawajatambuliwa wala kushirikishwa katika harakati za aina hii.

Mwishoni mwa tawasifu, mwandishi amesimulia maisha ya marafiki zake wawili, Abdalla na Shaaban. Mwandishi anaeleza vile mwezi wa Mei mwaka wa 2007, alipata habari za kuugua kwa Abdalla na kwenda hospitalini, Hindu Mandal, Tanzania ambapo alipata kwamba ameshaaga dunia. Mwandishi alieleza kwamba, yeye na Abdalla waliporudi Zanzibar, Abdalla alienda Cuba kupata mafunzo zaidi ya kijeshi. Baadaye alirudi Zanzibar na kujiunga na harakati za kisiasa. Mapinduzi yalipotokea Zanzibar mwaka wa 1964, yeye na watu wengine walianzisha Jeshi la Ukombozi wa Zanzibar. Baada ya kuungana kwa Zanzibar na Tanganyika, majeshi yote yaliungana na Abdalla akawa Afisa katika jeshi hilo. Alikwenda Urusi na kupata mafunzo zaidi. Alirudi Zanzibar na kufanya kazi Nachingwea, Monduli na Dar es Salaam. Rais wa Zanzibar, Abeid Karume alipouliwa, Abdalla alikamatwa na kutiwa jela kwa muda mrefu. Baada ya kuachiliwa, aliachishwa kazi jeshini. Mwandishi alieleza kwamba, mwaka 2009, Shaaban Salim alikuwa bado mtu mwenye afya (uk 480) Shaaban naye alipata mafunzo ya kijeshi Kairo, Cuba na Urusi. Alifanya kazi kwa cheo cha Luteni kabla ya kukamatwa na kufungwa kwa muda mrefu kama Abdalla baada ya kuuawa kwa Abeid Karume. Baada ya kuachiliwa huru alifanya kazi kama Mkuu wa Nidhamu katika Chuo cha Kilimo Kizimbani. Wakati wa kuandikwa kwa tawasifu Shaaban bado yuko na anaishi Mkunazini. Katika muktadha wa wahusika kutoka nje ya nchi zao ili wakapate mafunzo zaidi ya kijeshi nje ya nchi zao, hakuna wahuska wa kike.

Kutokuwepo kwao katika muktadha wa mafunzo ya kijeshi na vyeo katika majeshi kwaweza kuelezeka kihistoria na kianthropolojia kuwa ni ukimya kwa maana ya kutohusishwa au kutoshirikishwa.

3.3 Mazingira ya kisiasa

Siasa ni itikadi ambapo kundi la watu au wanajamii hufuata kwa kuaminishwa na viongozi wao na ambayo huwa ndio msingi wa kuendesha mifumo ya uchumi, utamaduni na maisha ya kijamii. Masula ya kisisasa huweza kuendeshwa na taasisi mbali mbali za kijamii. Masuala na matukio mengi ya kisiasa katika *Mbali na Nyumbani* yamewasilishwa katika miktadha mbalimbali kihistoria. Wahusika ni watu halisi waliowahi kuishi na wengine bado wanaishi. Matukio ya kisiasa pia ni mambo ya kweli yaliyotokea katika mazingira halisi. Kihistoria, kipindi cha miaka ya sitini, ni kipindi kinachojulikana kama cha kupigania uhuru barani Afrika. Nchi za Afrika zilikuwa zikitawaliwa na wakoloni kutoka nchi za kigeni. Utawala wa kikoloni uliwanyima Waafrika uhuru wao katika mifumo na taasisi mbalimbali. Utawala huu ulikuwa ukiwadhulumu Waafrika kwa njia tofauti tofauti. Matatizo yaliyopelekea Waafrika kupigania uhuru yalikuwa; unyakuzi wa mashamba yao, kulazimishwa kufanya kazi katika mashamba ya wabeberu na ulipaji wa kodi mionganini mwa mengine. Hali hii iliwachosha na kuwaudhi Waafrika. Kila nchi ilianzisha mipango kabambe ya kupigania uhuru wao. Baadhi ya nchi zilitumia njia ya mazungumzo huku zingine zikitumia silaha ili kunyakua uhuru wao kutoka kwa wakoloni. Mapambano hayo yalifanywa kuititia vyama vya wafanyakazi na vile vya kisiasa. Vyama hivi vilikuwa na viongozi waliochaguliwa ili kujadili mapendekezo yao na serikali za kikoloni. Mazungumzo yalipogonga mwamba, baadhi ya nchi zilianzisha harakati za vita ili kuwashinikiza Wakoloni wawape uhuru wao. Kihali halisi, vyama vya kutetea wafanyakazi

ndivyo vilizaa vyama vya kisiasa. Mapambano yalikuwa yamepamba moto kila mahali hasa nchi za Afrika Mashariki, mahali pa jamii ya mwandishi.

Katika (uk 15) mwandishi anaeleza jinsi mapambano ya kupigania uhuru wa Tanganyika yalikuwa yamepamba moto mwaka wa 1960. Wakati huu mwandishi alikuwa safarini kuelekea Kairo. Katika meli ya *M.V. Ubena*, walikuwemo Waarabu wawili waliokuwa wakirudi kwao Yemen kutoka Tanga. Hofu yao ilikuwa kwamba, Tanganyika ikipata uhuru, yangetokea machafuko makubwa (uk 16). Machafuko yaliyodhaniwa kutokea yalitokea baadaye, tarehe I Juni 1960, baada ya upigaji kura uliotibuka Zanzibar. Kuna miktadha miwili ya kisiasa katika *Mbali na Nyumbani*; muktadha wa vyama vya wafanyakazi na muktadha wa wanasiaya.

3.3.1 Vyama vya wafanyakazi na vyama kisiasa

Tumeshataja kwamba, vyama vya wafanyakazi ndivyo vilivyozaa vyama vya kisiasa. Vyama hivi vilianzishwa na vikundi vya watu ambao walikuwa wakifanya kazi katika serikali ya wakoloni pamoja na wale waliofanya kazi katika viwanda na mashamba ya Wazungu. Vyama hivi vililalamikia masuala kama yale ya malipo duni, hali mbaya za makazi, kazi nzito, ulipaji kodi miiongoni mwa masuala mengine. Vyama hivyo viliongozwa na watu ambao baadhi walichukua uongozi wa nchi zao baada ya kunyakua uhuru. Mwandishi ameeleza harakati za baadhi ya vyama vya wafanyakazi na kuhusisha viongozi mbali mbali walioshughulika katika upiganiaji uhuru. Mwandishi mwenyewe aliporejea Zanzibar, alijiunga na kundi mojawapo lililokuwa likidai haki za wafanyakazi. Baadaye alijiingiza katika siasa na waandishi wa magazeti aliokutana nao walimfunza jinsi ya kuandika magazeti. Wakati huu machafuko yanapotokea, ye ye alikuwa mwangalizi wa chama cha kisiasa kilichoshiriki katika uchaguzi huo, katika kituo

cha Mahonda (uk 425). Baadaye mwandishi alipata kazi ya kuhariri gazeti lililoitwa ‘*Kibarua*’. Gazeti hili lilikuwa la chama cha wafanyikazi ambacho Katibu Mkuu alikuwa Khamis Abdalla Ameir, naye Katibu Muhtasi akiwa Hasina. Chama hiki cha wafanyikazi ndicho baadaye kilimthamini mwandishi katika masomo yake kule Ujerumani. Mwandishi anaelezea jinsi watu walipigana, wakachinjana na kuuana katika vituo vyta kupigia kura. Ilibidi askari wa kigeni watulize fujo hiyo (uk 432) Mapigano haya yalisababishwa na jazba za kisiasa huku watu wakigawanyika wakawa hawasemezani, hawatembeleani, hawazikani, kila mmoja akivutia upande wake (uk 423) Katika muktadha huu wa vyama vyta wafanyikazi, mhusika wa kike ni mmoja tu, Hasina, ambaye ni Katibu Muhtasi wa Katibu Mkuu. Kuwepo kwa ufinyu kwa wanawake katika muktadha wa vyama vyta wafanyikazi na vyta kisiasa nchini Zanzibar, kwaweza kuelezwa kihistoria kuwa ni ucheleweshwaji wa wanawake katika kutambuliwa na kushirikishwa katika shughuli za kimsingi za kijamii.

Kipindi cha mwaka wa 1960, mwandishi anakieleza kama kipindi ambacho siasa nchini Kenya zilikuwa zimepamba moto sawasawa. Mwandishi anaeleza;

Siasa nchini Kenya ilikuwa i-moto na harakati za vyama vyta wafanyikazi zilikuwa zimechanganyika na harakati za kisiasa. Kenya nzima ikifukuta moto wa makumbi (uk 30)

Ni wakati huu wa moto wa siasa nchini Kenya ndipo mwandishi anafika Mombasa baada ya safari yake kukatizwa kule Aden aliposhindwa kulipa dhamana ya shilingi mia sita (uk 19). Kule Mombasa, anakutana na Adam Mwakanjuki ambaye alijishughulisha kikamilifu na harakati za vyama vyta wafanyakazi. Adam Mwakanjuki anamjulisha kwa viongozi wengi maarufu wa vyama vyta wafanyikazi kama, Dennis Okumu na Ben Opar Mboya kutoka Kenya, mionganoni

mwa wengine (uk 30) Ben Opar Mboya alikuwa kiongozi wa Shirikisho la Vyama vyatia Wafanyikazi tawi la Mombasa. Katika muktadha huu wa vyama vyatia wafanyikazi nchini Kenya hakuna wanawake wanaohusishwa. Kutokuwepo kwao katika harakati za kudai haki za wafanyikazi kunaelezeka kihistoria kwamba hivyo ndivyo mambo yalivyokuwa, na kwa hivyo kuibuka kwa ukimya wa wanawake ni kutokuwepo katika harakati hizi.

3.3.2 Wanasiasa

Viongozi wa kisiasa ambao mwandishi amerejelea ni Jomo kenyatta aliyekuwa amefungwa huko Lodwar. Oginga Odinga na Tom Mboya walikuwa mstari wa mbele wakidai kuachiliwa kwa Kenyatta huku wakidai uhuru. Katika muktadha wa wanasiasa Kenya, wanawake hawajahusishwa. Kutokuwepo kwa wanawake katika siasa kunaelezeka kihistoria na kianthropolojia kama ukimya wa wanawake katika harakati za kisiasa.

Wanasiasa wengine waliotajwa na mwandishi ni pamoja na Abdulkadir-el-Amin wa Sudan. Mwandishi alipokuwa akiondoka Mombasa, Adam Mwakanjuki alimpa anwani ya mwanasiasa huyu ili akifika Khartoum amtafute. Dokta Banda, mwanasiasa kutoka Nyasaland amehusishwa kimasimulizi. Mwandishi na wenzake walipopelekwa kituo cha polisi cha Pakwach, masanduku yao yalisasambuliwa na askari na picha ya Dokta Banda ikapatikana katika sanduku la Abdalla. Banda alikuwa akihutubia mkuutano wa hadhara katika kiwanja cha Mnazi Mmoja, Unguja. Alikuwa ametumwa na PAFMECA kusuluuhisha ugomvi wa kisiasa kati ya vyama vyatia kisiasa katika nchi hiyo. Dokta Banda alikuwa mpiganiaji uhuru mashuhuri, hasimu mkubwa wa wakoloni wa Kiingereza (uk 204)

Mwandishi mwenyewe ameeleza historia ya mapambano ya kupigania uhuru nchini Sudan. Katika maelezo yake anasema kwamba, mwaka huo 1960, Sudan ilikuwa nchi huru baada ya kupata uhuru mwaka 1956. Mapambano ya kupigania uhuru yalianza mwaka 1881 chini ya kiongozi shupavu, Mohammed Ahmad ibn as-Sayyid baada ya kijitangaza kuwa Mahdi. Aliongoza mapigano makali ya mtutu wa bunduki kati ya wapiganiaji uhuru wa Kisudan na majeshi ya pamoja ya wakoloni wa Kiingereza na Wamisri walioongozwa na C.G.Gordon. Katika mapigano hayo Mahdi alishinda na Gordon akaawa mnamo mwaka wa 1884, huko Khartoum (uk 222) Katika nchi ya Sudan mnamo mwaka 1960, serikali ilikuwa chini ya utawala wa kijeshi ikiongozwa na Jenerali Ibrahim Aboud, aliyeniyakua madaraka kwa nguvu mwaka 1958. Kwingineko, mwandishi amesimulia tukio la kihistoria kuhusu mji wa Omdurman uliokuwa kaskazini mwa Khartoum. Kihistoria, hapo ndipo palikuwa makao makuu ya Mohammed Ahmed ibn as Sayyid, aliyepigana na Waingereza na Wamisri (uk 268) Viongozi wote wanaotajwa katika muktadha huu ni wanaume ambao mbali na kuwa wanasiasa, ni wapiganiaji uhuru. Hakuna wanawake. Kutokuwepo kwa wahusika wanawake katika muktadha huu wa wanasiasa wapiganiaji uhuru ni ukimya wa wanawake kihistoriakatika harakati za kupigania uhuru.

Katika Chuo Kikuu cha Khartoum, Daniel ambaye ni mwanafunzi anasimulia historia ya Kongo katika upiganiaji uhuru. Anaeleza mapigano ya Wakongo dhidi ya Wabelgiji na hatimaye kuuawa kwa Patrice Lumumba, kiongozi na wanasiasa maarufu. Anasimulia pia mapambano ya watu wa Sudan ya Kusini na mapigano ya watu wa Afrika Mashariki dhidi ya ukoloni (uk 273 -274) Dokta Kwame Nkurumah anarejelewa kama simba wa Afrika. Alikuwa wanasiasa na kiongozi mashuhuri barani Afrika. Aliongoza nchi ya Ghana katika mapigano dhidi ya Wazungu.

Kundi la Waafrika lililokuwa likitafuta viza lilitembelea Ubalozi wa Ghana mjini Khartoum na kuhutubiwa kabla ya kupewa ufadhili wa shilingi mia tatu kila mmoja. Aliwaeleza umuhimu wa Waafrika kuwa kitu kimoja katika vita vya kujikomboa na kuikata minyororo ya kikoloni. Wanaohutubiwa ni wanaume kutoka Kenya, Uganda, Zanzibar na Nyasaland. Baadaye katika Jengo la Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, Abdul-Aziz anawasimulia historia ya nchi ya Sudan na mapambano yake dhidi ya mkoloni, kabla ya kuwapa pasi zao alizozuilia hadi watakapopata viza ya kuingia Misri. Kutokuwepo kwa wahusika wa kike ni suala la ukimya kianthropolojia na kihistoria.

Baada ya kupata viza ya kuingia Misri, mwandishi, Abdalla na Shaaban wanajiunga na Waafrika wenzao mjini Kairo. Wanaishi barabara ya Ahmed Hishmet, Mtaa wa Zamalek, nyumba nambari kumi na tano. Mwandishi anaeleza kwamba hapo ndipo palikuwa na shughuli za kisiasa pamoja na matayarisho ya upiganiaji uhuru wa Nchi za Afrika, kila nchi ikiwa na ofisi. Kairo ilikuwa ngome ya wapigania uhuru na vyama vingi vya kupigania uhuru vilikuwa vikikusanyika pamoja katika nyumba ile. Katika ofisi hizo, wanafunzi kutoka nchi mbalimbali za Kiafrika walikuwa wakitafutiwa masomo. Hata hivyo, katika nyumba hiyo, wengi waliokuwamo walikuwa wanaharakati wa kupigania uhuru. Lugha iliyokuwamo ilikuwa ukombozi. Majina ya wanasiaya yaliyokuwa yakinajwa pale yalikuwa, Jomo Kenyatta wa Kenya, Amilca Cabral wa Guinea Bissau na Cape Verde, Edward Mondelane wa Msumbiji, Ben Bella wa Algeria, Augustino Neto wa Angola na wengineo. Katika muktadha huu wa viongozi wa kisiasa, hakuna wahusika wa kike. Wanaotajwa ni viongozi ambao kwa kweli walipigania uhuru katika nchi zao na hata wengine wakawa marais wa kwanza katika nchi zao baada ya kunyakua uhuru kama Jomo Kenyatta wa Kenya (uk 382) Viongozi wote wanaotajwa katika muktadha huu ni wanaume. Wao

ni wapiganiaji uhuru na wanasiasa maarufu. Kutokuwepo kwa wahusika wa kike kunaelezeka kihistoria kama ukimya.

Mazungumzo yanayofanywa katika nyumba ya Ali wakati wa chakula ni ya kisiasa. Nuru na Asha hawahusishwi katika mazungumzo hayo. Wao waliwaandalia chakula tu. Ali anawaambia wenzake kwamba, katika mapambano dhidi ya wakoloni, vijana ndio walipaswa kuwa mstari wa mbele (uk 384) Baada ya chakula walihamia ofisini ambapo hoja ya kujiunga na kundi la wapiganiaji uhuru iliibuliwa. Baada ya kufikiri kwa muda wa siku kadhaa, wote waliamua kuingia kambini ili wapate mafunzo ya kijeshi na baadaye waweze kuzikomboa nchi zao. Wanapojiunga na kambi ya kijeshi wanawake hawahusishwi pia.

Mwandishi anapoondoka Zanzibar kwenda Ujerumani kusoma, anaandamana na Hussein na Suleiman. Hussein alikuwa mwenyeji wa Pemba. Alikuwa akijishughulisha na harakati za kisiasa. Anawaeleza wenzake kwamba, aliwahi kuhudhuria Mkutano wa Nchi za Kiafrika kule Ghana. Suleiman alitokea Unguja. Kabla ya kuingia katika harakati za kudai haki za wafanyakazi, alikuwa akifanya kazi serikalini. Shafi, Hussein na Suleiman walikuwa wakienda kusomea masuala ya kisiasa. Kutokuwepo kwa wanawake ambao walisafiri hadi nchi za Ng'ambo ili kupata taaluma katika masuala ya kisiasa kunaelezeka kihalisia kama ukimya wa wanawake bali hakuelezeki kiusawiri.

3.4 Mazingira ya kidini

Dini ni mfumo fulani wa imani ya watu na njia ya kuabudu, kusali, kuheshimu au kumtii muumba wao. Baadhi ya dini ni Ukristo, Uislamu, Uyahudi, Uhindu, Ubudha mionganoni mwa

zingine. Kila dini huwa na imani zake ambazo zimejenjeka katika itikadi fulani. Waumini wa dini fulani hushikilia na kuendeleza imani zao kupitia viongozi wa kidini. Baadhi ya masuala ya kidini huhusisha kusali, kusifu, kutoa zaka na sadaka, miongoni mwa mengine. Katika *Mbali na Nyumbani* dini zinazohusika ni dini ya Kiislamu na dini za Kienyeji.

3.4.1 Dini ya Kiislamu

Uislamu ni dini ambayo msingi wake ni Kurani Tukufu na inafuata imani ya kuwa Mungu anayepaswa kuabudiwa ni mmoja tu na Mtume Muhammad ni mjumbe wake. Mwandishi amewawasilisha wahusika halisi katika mazingira halisi ya kidini kama misikitini na sherehe za kidini zinazofanywa nje ya muktadha wa misikiti. Vile vile, kuna maelezo na masimulizi kuhusu dini ya Kiislamu. Mwandishi amejitambulisha kama Muislamu anapoeleza;

Nilikuwa sikujiandaa kwa chakula nikiwa safarini. Nilitegemea kuomba chakula mumo humo melini. Siku moja nilipokwenda kuomba mkate nilimkuta mpishi akitoa jichwa la nguruwe kwenye ‘oven’. Nilisema moyoni mwangu, “Mama yangu we!” Mimi Muislamu, sili nguruwe na inaonesha nguruwe nd’o kilichokuwa chakula chenyewe melini mle. Nilisema, “Potelea mbali, msafiri kafiri,hata huyo nguruwe nikimpata nitaml.”(uk 16)

Maelezo haya yanaonyesha itikadi ya Waislamu kutoruhusiwa kula nguruwe. Mwandishi analazimika kula nguruwe kutokana na hali ya kuishiwa na chakula. Huku ni kukufuru imani ya dini yake. Kwingineko, mwandishi amehusika katika miktadha ya kidini. Kwanza, katika safari yake ya kwanza kurudishwa Zanzibar, yeye na Abdalla waliomba malazi katika Msikiti wa Mbale kwa kuwa walifika kule usiku. Mwandishi anaeleza kwamba, misikiti mingi ya Uganda na Kenya ilikuwa na vyumba maalumu vya kupokea wageni vilivyoitwa “*Musafir Khana*”

Imamu wa Msikiti ule aliposikia mngurumo wa lori, alitoka nje kwani alijua fika kwamba alikuwa na wageni (uk 99).

Kulingana na mwandishi, imamu yule alikuwa ameshika dini sawasawa. Shafi anaeleza;

Alikuwa na pandikizi la sijida usoni na sura ya mtu Rahimu. Alionesha alikuwa bado hakulala, labda alikuwa amezama katika nyiradi za usiku. (uk 100)

Mwandishi alipokuwa akiishi Bungoma, mwenyeji wake Bwana Bakari alimtaka atafute mahali pengine pa kuishi. Shafi alimwendea Sheikh Noor, msimamizi wa ujenzi wa msikiti wa Bungoma ili amwombe makazi katika chumba cha msikiti. Shafi anaeleza kwamba, Sheikh Noor alikuwa mzee wa Kisomali aliyejitlea kumcha Mungu maisha yake yote. Yeye ndiye alisimamia ujenzi wa msikiti wa pekee wakati huo huko Bungoma. Alisafiri hadi Kenya akichangisha shilingi moja moja kutoka kwa Waislamu ili agharamie ujenzi huo. Sheikh Noor alienda msiktini kila wakati na mwandishi anampata pale wakati wa swala ya adhuhuri huku akiomba kwa tashbih yake. Shafi alijadiliana na Sheikh Noor ndipo akamkulalia ombi lake (uk 120-123). Maeleo hayo yanatuonyesha majukumu ya Sheikh katika dini ya Kiislamu. Kwanza, kusafiri kutoka Uganda hadi Kenya akichangisha pesa za kujenga msikiti. Pili, kusimamia ujenzi. Tatu, kwenda msikitini kila wakati. Katika muktadha huu wanawake hawatambuliwi wala kuhusishwa.

Katika mji Bungoma, mwandishi anaeleza jinsi wafanyibiashara walishughulika kidini. Anaeleza;

Duka la nyama lilikuwa limefungwakwa kuwa ulikuwa wakati wa swala ya magharibi (uk 108)

Duka lililokuwa limefungwa likikuwa la Bwana Bakari, Mjomba wa Abdalla ambaye aliwakimu kule Bungoma. Wengine wanaohusishwa na swala ni Mzee Suleiman Manoti. Wakati mwandishi na Abdalla wanafika kwake kule Kampala, wanaelezwa kuwa Manoti alikuwa ameenda safari ya Hijja huko Makka (uk 62) Ame pia alikuwa akienda Makka kuhijji wakati anapokutana na Shafi katika meli ya *M.V Ubena*. Katika mji wa Bugembe, mwandishi na Abdalla waliingia katika msikiti ili wapate kujulishwa kwa Maalim Idi. Msikitini walimpata mtu mmoja aliyeonekana mcha Mungu. Anawapeleka kwa Maalim Idi kwa kuwa nyumba yake haikuwa mbali na msikiti. Maalim pia alikuwa Muislamu. Alivalia kanzu, koti na tarbushi vazi lake la kawaida. Baada ya kupumzika, Maalim anajuliana hali na wageni wake. Wanapomweleza kwamba safari yao ilikuwa ya Kairo kusoma, anainua viganja vyake vyakonon na kuwaombea dua ili Mungu afanikishe safari yao. Mwandishi na mwenzake nao waliinua mikono yao na kuitikia.

“Mwende safari yenu salama” .“Amina.” “Mfanikiwe katika haja zenu zote za kheri” .“Amina” (uk 181- 182)

Mwandishi anaeleza kwamba pale walikuwa mionganoni mwa wacha Mungu na hivyo iliwabidi pia wasipitwe na kipindi hata kimoja. Maalim anawapeleka katika msikiti mkuu wa Ijumaa wa Kampala. Kule msikitini, walipata Waislamu wakikusanyika kwa swala ya Ijumaa. Walikuwa wamevalia nguo zao za mtungini ili kutimiza suna ya kuvaahivyo kwa swala hiyo. Walivaa kanzu nadhifu nyeupe, wengine, kofia na wengine vilemba. Msikiti ulikuwa umejaa mpaka nje. Watu walikaa kwa safu juu ya mabusati wote wakielekea kibla. Imamu wa msikiti alikuwa Mwarabu kutoka Yemen. Alipanda kwenye mimbar na kusoma hotuba ya swala ya Ijumaa huku watu wakimsikiliza alipotaja majina ya maimamu wa dini ya Kiislamu. Baada ya swala ya Ijumaa. Katika muktadha huu wa Ibada Misikitini, wanawake hawatambuliwi wala kuhusishwa na kushirikishwa.

Bwana Muhanji Msuo aliishi nje ya jiji la Kampala. Maalim Idi, Shafi na wenzake walihudhuria sherehe za kidini kiamboni (uk 184-185. Katika sherehe hii, wanawake wamehusika katika upishi na uandalizi wa chakula. Kundi la wanawake waliovaa magwanda ya Kiganda walionekana wakihangaika kwa maandalizi ya upishi. Wengine walikuwa wakiwaandalia wageni chakula huku wakizunguka na sahani za matoke na mabakuli ya mchuzi. Usiku ulipoingia wanaume walishiriki katika mazungumzo ya kidini. Wanawake hawakuhusika katika mazungumzo hayo. Ulikuwa usiku wa dhikiri ya tarika ya shadhili iliyօendelea usiku kucha. Alfajiri ilipofika wanawake wale waliwaandalia wageni chai na maandazi. Kutohusika kwa wanawake katika mazungumzo ya kidini kunaweza kuelezeka kihalisia kama ukimya.

Mwandishi na wenzake walikaa siku mbili kwa Bwana Muhanji Msuo. Siku ya tatu waliandamana na Malim Idi hadi kwa Sheikh El-Hadadi, imamu wa msikit wa Ijumaa. Walimkuta peke yake amekaa penye kibla akisoma Kur'an. Baada ya mazungumzo yao kuhusu safari ya Sudan, Sheikh aliinua viganja vyake vya mikono na kuwaombea dua huku wakiitikia Sheikh EL-Hadadi alikuwa tayari amezungumza na Balozi wa Sudan ili akubali maombi yao ya viza (uk 189) Mwandishi na wenzake walifurahi kupata viza. Sheikh alipiga *Fat -ha* na kuwaombea safari njema.

Mwandishi aliporejea nyumbani kutoka Kairo, alimpata mama yake ameketi juu ya mkeka ameshika watoto wawili wa kike, Zawadi na Fatma. Baada ya kujuliana hali, mamake anamjulisha kifo cha Maalim Said Omar kisha anamwambia; “Nenda ukamzike baba yako mwanangu. (uk 422)”

Mwandishi anafululiza hadi Msikiti wa Miembeni ambapo maiti ya Maalim Said Omar ilikuwa imeletwa. Kati ya umati wa watu uliohuduria maziko alikuwemo baba yake. Mwandishi anasema kwamba, alipewa heshima ya kushuka kaburini ili amlaze baba yake mdogo kwenye mwanandani. Mama yake mwandishi hahusiki katika sherehe za kuzika Maalim Idi. Uombolezaji wa kifo cha Maalim Said Omar uliendelea kwa siku tatu kisha siku ya nne wakaondoa tanga. Kutokuwepo kwa wanawake katika sherehe za mazishi ya Bwana Said Omar kwaweza kueleza kihalisia kuwa ukimya kianthropolojia kwamba, katika muktadha wa dini ya Kiislamu, japo wanawake wanahuishwa na miktadha ya mazishi, hawakubaliwi kuchanganyika na wanaume. Kwa misingi hii, yawezekana kuwa, mwandishi ameleezea hali ilivyo kuwa katika mazishi aliyohuduria. Aliweza kutagusana na wanaume kama vile baba yake na huu ni uhalisi anaosimulia katika kazi yake. Wanaume wamehusishwa na shughuli na vyeo mbali mbali. Shughuli hizo ni kama, kuswalisha kujenga misikiti, kukaribisha wageni misikitini na kuzika waumini wa dini yao. Nyadhifa ambazo zimejitokeza ni kama Shehe na Imam. Wanaume katika miktadha yote ya dini hii ndio viongozi katika misikiti. Hakuna mhusika wa kike hata mmoja. Kutokuwepo kwa wanawake katika usimamizi wa misikiti ni ukimya halisi kianthropolojia.

3.4.2 Dini za Kienyeji

Mara ya kwanza mwandishi anapofika Bungoma anaishi kwa muda wa wiki moja. Yeye na Abdalla Juma Bulushi walipitia pale na kuishi kwa mjomba wa Juma, Bwana Bakari. Wakati wanapoondoka mwandishi anasema kwamba alihisi kuwa Bungoma ni mahali alipopazoea napo pakamzoea ila hakujuu ni kwa nini alihisi hivyo. Anaeleza;

Ijapokuwa kuwepo kwangu katika mji ule kulikuwa kwa muda mfupi tu, sikujua mji ule ulikuwa na siri gani iliyonifanya nihisi hivyo (uk 59)

Baada ya safari ya mwandishi kukatika kwa mara ya pili, aliamua kurudi Bungoma badala ya kwenda Zanzibar. Alirudi kwa Bwana Bakari na kujuana na vijana wengi wa Kisomali na Wabukusu. Alipenda sana kuuangalia Mlima Elgon. Aliuona wenye matumaini hasa kwa sababu matumaini yake ya kwenda Ulaya kusoma yalikatizwa na mitafaruku mbali mbali. Anaeleza kwamba, Wabukusu waliuheshimu Mlima Elgon kwa imani kwamba, kilele cha mlima ule ndiko alikoishi Elijah Masinde, kiongozi wa ‘*Dini ya Msambwa*’. Kama anavyoeleza, dini hiyo ilitangaza vita dhidi ya ukoloni wa Wazungu. Imani yao ilikuwa kwamba, ukombozi ulitegemea mlima ule. Mwandishi anaeleza;

Ikiwa Mlima Elgon uliweza kuwapa Wabukusu matumaini ya ukombozi kwa vile ulivyosimama imara na kumhifadhi kiongozi wao Elijah Masinde, kwa nini usiwe alama ya matumaini kwangu? (uk 112)

Kiongozi wa “*Dini ya Msambwa*” ni mwanamume. Kutowahusisha wanawake katika uongozi wa dini hii kunafungamana na masuala ya kimsingi ya utafiti kwamba, wanawake kihistoria hawakushiriki katika masuala ya kidini. Kutokuwepo kwa wahusika wa kike katika muktadha huu basi, kwaweza kuelezeza kianthropolojia na kihistoria kama ukimya.

3.5 Mazingira ya kuhama na uhamiaji

Uhamaji ni hali ya mtu au watu kuondoka mahali na kwenda kuishi mahali pengine. Uhamaji unahusisha kutoka sehemu fulani katika nchi fulani hadi sehemu nyingine katika nchi hiyo bila kuvuka mipaka. Kwa upande wake, uhamiaji ni hali ya mtu au watu kutoka au kuingia nchi fulani kwa shughuli fulani. Uhamaji na uhamiaji katika *Mbali na Nyumbani* umejitokeza katika miktadha mbalimbali. Mhusika mkuu Adam, amehusishwa na uhamaji na uhamiaji kwa kiwango

kikubwa. Katika uhamaji na uhamiaji wake, kuna wahusika wengine ambao wameandamana naye. Katika sehemu hii, tunakusudia kubainisha kutokuwepo kwa wahusika wa kike katika miktadha ya uhamaji na uhamiaji. Lengo la kubainisha kutokuwepo kwao ni kuiwekea misingi mijadala ya utafiti hasa kuhusu sababu za kutokuwepo kwao katika miktadha hiyo ya uhamaji. Sababu za uhamaji na uhamiaji katika tawasifu hii zinatokana na shughuli mbali mbali za wahusika, hasa mhusika mkuu, Shafi. Mahusiano kati ya uhamaji na uhamiaji na masuala ya kimsingi ya utafiti ni kwamba, katika kipindi hicho cha kihistoria, kulikuwa na ubanifu wa uhamaji na uhamiaji wa wanawake ambao unaelezeka kianthropolojia na kihistoria. Tutajadili uhamaji na uhamiaji kwa kuhusisha sababu zinazochochea uhamaji na uhamiaji huo. Sababu hizo zinachangia pakubwa kuonyesha kwa nini wanawake hawapo au hawahusishwi.

3.5.1 Kuhama kutoka Zanzibar hadi Aden

Mwandishi anapoondoka nyumbani kwao Zanzibar mwezi wa Aprili 1960, lengo lake ni kuhamia Ulaya ili akapate elimu. Safari ya mwandishi kuondoka Zanzibar ilikuwa siri kubwa. Waliojua kuhusu safari hii walikuwa marafiki wachache waliomsaidia kwa pesa kidogo kama Khamis Mohammed Nura, aliyekuwa London wakati huo na Abdalla Mwinyi. Abdalla Mwinyi ndiye aliyemsindikiza hadi bandarini alipoabiri meli iliyoitwa M.V.Ubena. Meli hii haikuwa ya abiria, bali ilikuwa ya kubebia mizigo (uk 13) Melini alipatana na abiria watatu. Ame, alikuwa akitoka Mkokotoni akielekea Aden kisha baadaye Makka kwa nia ya kuhiji. Palikuwa pia na Waarabu wawili ambao walikuwa wakiishi Tanga. Walikuwa wakirudi kwao Yemen wakihofia kwamba kungekuwa na machafuko Tanganyika baada ya uhuru mwaka huo, 1960. Mwandishi na Ame walipofika Aden, hawakuruhusiwa kuendelea na safari. Walikosa pesa za kulipa dhamana ya shilingi mia sita. Katika ofisi ya wakala wa meli, palikuwa na daktari wa meno

kutoka Zanzibar. Aliitwa Dokta Idarusi Baalawi. Yeye pia alikuwa mhamiaji Aden kutoka Zanzibar (uk 22) Sababu za uhamiaji huu ni za kielimu, kidini kisasa na kikazi. Katika muktadha huu, hakuna wahusika wa kike. Kutokuwepo kwao kwaweza kuelezeza kihalisia kuwa kufikia wakati huu wanawake walikuwa hawakushirikishwa katika shughuli za kuhamia mataifa ya nje kwa nia ya kupata elimu, dini, siasa na kazi.

3.5.2 Kuhama kutoka Mombasa hadi Bungoma

Mwandishi aliporudi Mombasa baada ya kukatika kwa safari yake, alihangaika na kutaabika kwa sababu hakujuu angeishi wapi na vipi. Aliamua kuishi katika maskani ya mabaharia kule Mwembe Tayari. Alikutana na rafiki ya babake Mzee Ahmada Saidi na Adam Mwakanjuki. Adam Mwakanjuki alikuwa akiishi Tudor na alimpa msaada mkubwa wa malazi na chakula. Adam Mwakanjuki alimjulisha Shafi kwa viongozi wa vyama vyta kupigania haki za wafanyikazi. Mwandishi alikutana na Abdalla Juma Bulushi na Abdalla Juma Maharuki. Waliamua kuanza safari ya Kairo. Safari hii ilianza kwa treni iliyowasafirisha hadi Nairobi, wakiandamana na Ben Opar Mboya, kiongozi wa Shirikisho la Vyama vyta Wafanyikazi tawi la Mombasa. Kule Nairobi walilala *Elgon Hotel* katikati ya mtaa wa *River Road*. Walihamia Eldoret na kukaribishwa na Saidi Manywele. Abdalla Bulushi alitafuta pesa za kutosha nauli ya kuwafikisha Bungoma kwa mjomba wake Bwana Bakari. Uhamaji huu ulifanywa nchini Kenya kwa lengo la kutafuta pesa za kugharamia safari ya Kairo. Katika muktadha huu wa kuhama kwa nia ya kutafuta vibarua, mwandishi hajawalusisha wanawake. Kutokuwepo kwa wahusika wa kike katika muktadha huu wa kuhamia mijini kwa nia ya kupata vibarua unaelezeka kama ubanifu wa wanawake katika uhamaji mijini.

3.5.3 Kuhamia hadi Kampala

Kule mjini Bungoma, Shafi alifanya kazi ya ukondakta. Aliwekeza pesa za kutosha kugharamia safari hadi Kairo. Anaeleza;

Nilichelewesha safari ya basi makusudi ili nipaye muda wa kwenda benki kuchukua pesa zangu nilizokuwa nikiweka akiba. Nilikwenda nikazitoa pesa zote nilizoziweka. Zilikuwa shilingi elfu tatu na u-shei. Baada ya kuzitia kibindoni, nilimshauri Shaabani tufuatane tukatembee Kakamega (uk 169)

Mwandishi na wenzake walipohamia Kampala kutoka Bungoma, walitarajia kuishi kwa Mzee Suleiman Manoti kule Kibuli, kabla ya kuendelea na safari yao. Walipofika kule, waliwapata vijana wengine kutoka Zanzibar ambao walikuwa wamewatangulia. Vijana hao, Abdalla Elyas na nduguye Kassim walikuwa wakisoma nao ‘*Comorian School.*’ Abdalla Juma Maharuki aliamua kurudi nyumbani kutokana na ugumu na matatizo ya safari. Kwa hivyo uhamiaji hadi Kairo ulifanywa na Shafi na Abdalla Juma Bulushi. Waliipanga safari yao kwa kutumia “*The National Geographic Magazine*”. Waliondoka kwa treni hadi Namasagali. Katika treni hiyo, palikuwa na abiria wengi sana. Wanawake waliokuwamo walikuwa wamewashika watoto wao mikono huku wakipakia mizigo ndani ya treni. Meli hiyo ilipitia Bandari ya Masindi kabla ya kutia nanga Butiaba. Kutoka Butiaba walisafiri hadi Nimule ili wavuke mpaka waingie Sudan. Wanawake waliokuwamo melini walikuwa wakishuka katika bandari na vituo vidogo vidogo. Mwandishi na wenzake waliitishwa viza ya kuingia Sudan. Kwa kuwa hawakuwa nazo, iliwabidi warudishwe Kampala ili wakaombe viza ya kuingia Sudan. Kabla ya kurudishwa walihamishiwa katika kituo cha polisi cha Gulu. Mkuu wa polisi aliwaambia;

“Lazima sasa narudi Kampala, Napata viza, halafu ndiyo naingia Sudan, Naelewa sawasawa?”

Badala ya kurudi Kampala, mwandishi na wenzake walirudi Bungoma. Abdalla Bulushi alihamia Nakuru na kumuacha Shafi huko Bungoma kwa matumaini kwamba akifanikiwa kupata kibarua angemjulisha amfuate kule. Baada ya Shafi kuishi Bungoma kwa miezi sita, alihamia Nakuru akiwa na Shaaban Salim ili wamfuate Abdalla Juma Bulushi aliyejewa akiwangojea kule. Walikaa Nakuru siku mbili kabla ya kuhamia Bugembe. Walipokewa na Maalim Idi. Aliwapeleka Kampala kisha wakahamia katika kijiji kimoja nje ya mji wa Kampala. Uhamaji kutoka Bugembe hadi Kampala ulikuwa wa kidini. Walitembelea msikiti wa Ijumaa kisha wakahamia kwa Bwana Muhanji Msuo kusherehekeea dhikiri ya tarika ya shadhili.

Uhamiaji Kampala mara ya pili unafanywa kwa kupitia Nakuru ambako Abdalla Bulushi alikuwa amehamia ili kutafuta kibarua. Shaabani na Shafi wanahamia Nakuru kwa treni na kufika kwa Shariff. Shariff anawahusia wasiende moja kwa moja hadi Kampala wapitie Bugembe kwanza kwa Maalim Idi. Wanahamia Bugembe ili wapate usaidizi wa viza kutoka kwa Maalim Idi.

Mwandishi anasema;

Nilirudi tena Kampala kuisaka viza ya kuingia Sudan. Hiyo ingelitoa uamuzi juu ya kufanikiwa au kutofanikiwa kwa safari yetu ya Misri.....Sikujua Maalim alikuwa na satuwa gani ya pale Kampala Kampala ya kutuwezesha sisi kuipata viza hiyo (uk 183)

Walisaidiwa kupata viza na Sheikh El-Hadadi, imamu wa Msikiti wa Ijumaa Kampala. Uhamiaji huu ulifanywa na wahusika wa kiume kutoka Zanzibar hadi Kampala. Mbali na Shafi, Abdalla na Shaabani, walikuwepo vijana wengine waliohamia Kampala. Hao ni Elyas na Kassim walioishi kwa Mzee Manoti. Kutokuwepo kwa wahusika wa kike kunaelezeka kihistoria kwamba viza inayowafanya wahusika wahangaike ingewawezesha kuingia Sudan ili wakapate

elimu, jambo ambalo liliwa nadra kwa wanawake. Suala nzima la uhamaji ni suala linaloweza kuhusishwa na ukweli kwamba katika kipindi hiki cha kihistoria, mwanamke bado alikuwa hajawa kiumbe wa kiuchumi, kwa maana ya kuhitajika kujichumia na kuchumia jamii. Hali kadhalika suala zima la utafutaji elimu laweza kuangaliwa kama ujenzi wa mikakati ya kujihakikishia uwezo wa kujichumia kibinafsi na kuchumia jamii. Hii ndio mojawapo ya sababu inayoweza kutolewa ni kwa nini kutokuwepo kwa wanawake katika harakati za uhamaji, ambazo pia ni harakati za utafutaji na uchumaji, ni ukimya wa kihistoria na kianthropolojia.

3.5.4 Uhamiaji Sudan

Baada ya Shafi na wenzake wawili kupata viza, wanaanza safari ya uhamiaji Sudan. Walisafiri kwa treni kutoka Kampala hadi Namasagali. Ndani ya treni hiyo walikuwepo manamba wafanyakazi katika shamba la miwa la Kakira amba walikuwa wameandamana na wake na watoto wao wakienda likizoni (uk 195-196). Walipitia Bandari ya Masindi na kuelekea bandari ndogo ya Pakwach. Katika kituo cha polisi, walihojiwa na askari wa kituoni pale na masanduku yao kupekuliwa. Abdalla alipatikana na picha ya Dokta Banda na hivyo ikawafanya kuonekana kama wanasiasa. Baadaye walihamishiwa kituo cha polisi Arua. Huko walifungiwa na kuhojiwa siku iliyofuata. Mwandishi alidhulumiwa kwa kushukiwa kuwa Mkikuyu kutoka Kenya. Alivuliwa nguo zote na Mzungu aliyekuwa Mkuu wa Kituo hicho. Baada ya mateso hayo, wanasindikizwa na askari hadi Laropi ili waiwahi meli iliyokuwa imeewaachwa siku iliyotangulia. Wanafanikiwa kuiwahi meli ambayo inawapeleka hadi Sudan. Katika meli hiyo, wanakutana na vijana wawili kutoka Kenya, Elly na Amos. Wanajenga usuhuba mkubwa. Wao pia walikuwa katika safari ya uhamiaji hadi Kairo kwa nia ya kusoma. Wanaingia Sudan wakiwa kundi la vijana watano. Wanahangaika wakitafuta viza ya kuingia Misri. Katika Ubalozi wa

Misri, wanakutana na vijana wengine kutoka Kenya. Vijana hao walikuwa wahamiaji huko Sudan na walikusudia kupata viza ya Misri ili wakasome. Hao ni pamoja na; Julius, Edward (uk256)

Edward aliwaeleza kwamba, kwa kuwa hakuwa na mahali maalum pa kulala, wangeenda katika Chuo cha Khartoum ili wapate vyumba vyta kulala kwa bei nafuu. Kwa wakati huu walikuwa wakilala kwa maboksi katika stesheni ya treni mjini Khartoum. Wakiwa Khartoum walitembelea mji mdogo wa Omduraman ili wakajiliwaze kwa kuona yaliyokuwa makao makuu ya Mohammed ibn as-Sayyid na pale mito ya Nile Mweupe na Nile Buluu inakutania. Mwandishi anasema;

Muda ambao tulidhania ungelipotea bure pale mjini Khartoum ulipita kwa haraka pale Omduraman. Ziara yetu katika mji ule ulikuwa kama maliwazo yaliyoniliwaza maradhi yangu ya kitoto kufikiri nyumbani (uk 270)

Wahamiaji katika muktadha huu walikuwa wanaume. Kutokuwepo kwa wanawake wahamiaji katika miktadha ya kupata elimu kunaelezeka kianthropoljia na kihistoria kwamba, katika kipindi hicho cha kihistoria wanawake wanaume ndio walihuushwa na masuala ya kutafuta elimu ya nje. Wanawake bado hakuwa wametambua umuhimu wa kuitafuta elimu nje ya miktadha ya jamii zao. Uwasilishwaji wa vijana wanaotafuta viza ya kuingia Misri ili wakasome ni uhalisi kihistoria.

Katika Chuo Kikuu cha Khartoum, mwandishi alimpata mwanamke kutoka Zanzibar aliyeitwa Zainabu. Zainabu alikuwa amehamia Khartoum kwa nia ya masomo (uk 276) Chuo hicho kilikuwa na wanafunzi kutoka sehemu mbali mbali za Afrika. Zainabu ndiyе mwanamke pekee aliyehusishwa na uhamiaji kwa nia ya kupata masomo. Kuwepo kwake kunaelezeka kihistoria

kama ucheleweshwaji wa wanawake katika upataji wa elimu ya chuo kikuu kipindi hicho. Mwandishi na wenzake walipokosa vyumba katika Chuo Kikuu cha Khartoum, Daniel aliwapa nyumba yake iliyokuwa nje ya mji wa Khartoum. Walihamza kwa madhumuni ya kutafuta makao bora. Mwandishi anaeleza kwamba nyumba ya Daniel waliyoihamia ilikuwa ya udongo mtupu, tokea msingi mpaka dari. Daniel alikuwa amewatahadharisha kwamba haikuwa nyumba nzuri. Anawaambia; “*Nyumba yenye si nyumba ya kuitwa nyumba, ni boma tu, labda la kuishi ng’ombe au mbuzi...* (uk 289) Katika muktadha huu, lengo la wahamaji hawa ni kutafuta malazi. Hakuna wahusika wa kike. Kutokuwepo kwao kunaeleweka kwamba, hii ni safari ya vijana walio katika harakati za kutafuta elimu, suala linaloelezeka kianthropolojia na kihistoria kwamba, katika kipindi hicho cha kihistoria, wanawake walikuwa bado hawajashirikishwa na kuhusika kwao katika masuala ya kielimu kulikuwa kwa pemberi mno. Huu kwa hivyo, unaweza kuelezwa kwamba ni ucheleweshwaji wa wanawake katika miktadha ya kielimu, na uwasilishaji unaofanywa na mwandishi unaakisi hali halisi kihistoria.

3.5.5 Kuhamia Kairo

Mwandishi, Shaaban na Abdalla hatimaye walifanikiwa kuingia Kairo. Uhamiaji wao ulianzia Khartoum wakapitia Wadihalfa kisha Shellal mahali pa kuvukia mpaka kuingia Misri. Baada ya kujaza fomu za uhamiaji waliingia Kairo. Walitafuta mahali palipoitwa Zamalek, Barabara ya Ahmed Hishmet, nyumba nambari kumi na tano. Sababu kuu ilikuwa kutafutiwa masomo katika nchi yoyote ile. Baada ya kupokewa katika nyumba ya Ali, walihamia mtaa wa Munira mbali kidogo na Zamalek. Kule waliwapata vijana wengine wahamiaji kutoka Zanzibar ambao walikuwa wanafunzi katika vyuo mbali mbali kule Kairo (uk 373) Baada ya kuhamasishwa kuhusu kupigania uhuru, waliamua kujunga na kambi ya mafunzo ya kijeshi iliyokuwa

jangwani, mahali penye upopo wa baridi na joto kali. Wanaojiunga na mafunzo hayo ni; Shafi, Abdalla, Shaabani, Hemedi, Suleiman, Nassor, Ali, Mansour na Mohammed. Baada ya kuhitimu mafunzo ya kijeshi, mwandishi alihamia Zanzibar kisiri akiwa na Abdalla. Lengo lao lilikuwa kupigania uhuru kwa kutumia silaha kama bunduki, vilipuzi na mabomu. Katika muktadha huu wa kuhamia kambini kwa ajili ya mafunzo ya kijeshi hakuna wahusika wa kike. Kutokuwepo kwao kwaweza kuelezeza kianthropolojia na kihistoria.

3.5.6 Kuhamia Ujerumani.

Mwandishi anaporejea nyumbani Zanzibar kutoka Kairo alipopata mafunzo ya kijeshi, alijunga na chama cha kudai haki za wafanyakazi kule Zanzibar. Baada ya machafuko yaliyotokea baada ya uchaguzi wa tarehe 1 June 1961 Zanzibar, mwandishi anapata ufadhili wa chama chao cha kudai haki za wafanyakazi aende Ujerumani kusomea mambo ya uchumi katika Chuo cha Wafanyakazi kwa muda wa miaka miwili (uk 434) Uhamiaji huu ulihuisha Shafi, Suleiman Hemed na Hussein Mbarouk. Suleimani alikuwa mwenyeji wa Unguja. Alikuwa akishughulika na harakati za vyama vya wafanyakazi baada ya kuacha kazi katika serikali ya ukoloni. Hussein naye alikuwa mwenyeji wa Pemba. Alikuwa mwanasiasa aliywahi kuhudhuria Mkutano wa nchi za Kiafrika kule Ghana. Uhamiaji katika nchi ya Ujerumani ulilenga elimu. Fauka ya hayo, wahamiaji hao walikuwa wanaume ambao nia yao ilikuwa kupata elimu ya juu kuhusu masuala ya kisiasa. Walipofika katika chuo cha Bernau, walikutana na wahamiaji wengine kutoka mataifa mbali mbali ya ulimwengu kama Anwar kutoka Uingereza (uk 467) na Ram kutoka Cylon (uk 470) Katika muktadha huu wa uhamiaji Ujerumani, hakuna wahusika wa kike. Kutokuwepo kwao kunaelezeka kihistoria na kianthropolojia.

3.5.7 Kuhama kwa Abdalla na Shaabani

Mwishoni mwa tawasifu hii, mwandishi ameелеzea maisha ya baadaye ya marafiki zake wawili, Abdalla na Shaabani. Wao, baada ya kuhamia tena Zanzibar kutoka Kairo, walipopata mafunzo ya kijeshi, walifanya uhamiaji mwingine nchi za Cuba na Urusi ambapo walipata mafunzo zaidi ya kijeshi. Wote walirejea Zanzibar na kupata vyeo vya juu katika majeshi ya nchi hadi kufikia kuuawa kwa Rais Abed Karume. Wote walikamatwa na kufungwa kwa muda mrefu baada ya kuachishwa kazi. Katika muktadha wa uhamiaji Cuba na Urusi, hakuna wahusika wanawake. Kutokuwepo kwao kunaelezeka kihistoria na kianthropoljia.

3.6 Mazingira ya kazi

Mazingira ya kikazi katika *Mbali na Nyumbani* yamejitokeza kwa njia mbali mbali. Mwandishi amewasilisha wahusika mbali mbali katika miktadha ya kikazi kihalisia. Pana miktadha fulani ya kikazi ambapo wahusika wa kike hawapo, wahusika wanaume ndio wapo. Mahusiano kati ya kutokuwepo kwa wahusika wa kike katika miktadha ya kazi za wanaume ni kwamba, uelezwaji wake ni wa uhalisia kuliko ule wa kiusawiri. Baadhi ya kazi ni ngumu na zinafanyiwa katika mazingira yasiyo salama kwa wanawake.

3.6.1 Kazi katika usafiri

Usafiri katika *Mbali na Nyumbani* ni wa aina nne; usafiri barabarani, usafiri majini, usafiri wa reli na usafiri wa ndege. Wasafiri walitumia aina hizi za usafiri kuhama na kuhamia sehemu mbali mbali za nchi za Afrika Mashariki, Sudan, Kairo na Ujerumani. Vyombo walivyotumia katika usafiri vilikuwa skuta, mabasi, malori, meli, mashua, motaboti, treni na ndege. Wafanyakazi katika vyombo hivyo wana shughuli mbali mbali. Tumebainisha kazi hizi kwa lengo la

kuonyesha mazingira ambayo wahusika wa kike hawako. Mahusiano ya kutokuwepo kwa wanawake katika miktadha hiyo na nadharia ya anthroplojia ni kwamba, wanawake walihusishwa na kazi fulani na kutohusishwa na nyingine katika kipindi hicho cha kihistoria. Tumebainisha kazi katika usafiri barabarani, usafiri majini, usafiri wa treni na usafiri wa ndege.

3.6.1.1 Usafiri wa barabarani

Usafiri barabarani umehusisha magari kama skuta, malori, teksi na mabasi. Katika vyombo hivi kuna madereva, makondakta, utingo, wapiga debe na washawishi. Katika muktadha huu wa usafiri, hapakuwepo na wanawake. Basi la Kampuni ya OMP ambalo mwandishi na wenzake walisafiria kutoka Mbale hadi Tororo, lilikuwa na kondakta na utingo ambao walikuwa wanaume. Wameelezwa kuwa watu wasiokuwa na insafu. Kondakta alishughulika kuwakatia watu tiketi. Yeye na utingo hawakujali kubanana kwa abiria kwa kuwa kama anavyosema mwandishi, hiyo ilikuwa ni siku njema iliyokuwa na baraka na biashara nzuri (uk 101). Mabasi mengine yalimilikiwa na Abdo, mwajiri wa Shafi. Basi moja liliitwa ‘*Kuiva*’ na lile lingine *Mawingo*. Mabasi hayo yalisafirisha abiria kati ya mji wa Kakamega na Bungoma. Dereva wa basi lililoitwa ‘*Mawingo*’ alikuwa akiitwa Simiyu, naye utingo alikuwa akiitwa Kabichi. Dereva wa basi la ‘*Kuiva*’ aliiitwa Kassim na utingo akiitwa Wilson. Shafi alikuwa kondakta wa basi la ‘*Kuiva*’. Shafi anaeleza kwamba, kazi ya ukondakta ilikuwa ngumu sana. Kwanza, ilibidi aamke alfajiri kuliko kawaida yake aingie katika baridi ya umande ulionyonyota usiku kucha kutoka Mlima Elgon. Pili, kunyanya magunia mengi ya abiria na baiskeli na kuyapandisha juu ya chanja ya gari. Tatu, kubishana na abiria wakorofi ambao walitaka kulipa nauli ya chini. Nne, hakuelewa vyema lugha ya Kibukusu na abiria wengi hawakufahamu lugha ya Kiswahili. Tano, ilibidi achukue hadhari kubwa asije akanaswa na askari kwa kukosa PSV. Hofu yake kuu ilikuwa

wakati wa kuvuka daraja la Nzoia wakati wa kwenda na kurudi. Daraja hilo lilikuwa limejengwa kiholela na lilikuwa hatari hivi kwamba, kila abiria alikuwa na hofu ya kufa kwa kutumbukia mto Nzoia. (uk 138) Ameeleza kwamba, madalali, makondakta na utingo wa mabasi kituoni walipaswa kuwa wahuni, wachepe na walaghai, sifa ambazo hakuwa nazo. Kulingana na mwandishi kazi ya ukondakta ilikuwa ngumu sana. Hata hivyo, Kabichi utingo wa basi la ‘*Mawingo*’ alijua kazi yake vyema. Mwandishi anaeleza;

Makondakta walikuwa wakienda mbio huku na huku na vitabu vyao vya tiketi mikononi tayari kumkatia abiria tiketi haraka haraka kabla hakukatiwa na kondakta mwingine. Kondakta wa Mawingo hakuwa na haja ya kufanya hivyo. Kazi hiyo alimwachia Kabichi aliyekuwa mwamba kituoni pale. Aliyeweza kumbeba abiria mzima mzima, akamvurumisha ndani ya basi yeeye na mizigo yake (uk 134)

Maeleo haya ya mwandishi yanaonyesha changamoto za kazi ya usafirishaji. Katika muktadha huu, hakuna wahusika wa kike hata kidogo. Kutokuwepo kwao kwaweza kuelezwaa kianthropolojia na kihistoria. Mbali na wanaume kuwa madereva wa mabasi, wao pia ni madereva wa teksi (uk 173,183,441,458) Katika ukurasa wa 441, dereva wa teksi alienda kuchukua Shafi na wenzake katika Hoteli ya *New Stanley* ili awapeleke katika uwanja wa ndege wa Nairobi. Hii ina maana kwamba, madereva wa teksi hufanya kazi wakati wowote, iwe mchana au usiku. Kutokuwepo kwa wahusika wanawake amba ni madereva wa teksi kunaelezeka kianthropolojia na kihistoria kama ukimya.

3.6.1.2 Usafiri wa majini

Vyombo vinavyohusika katika usafiri wa majini ni meli, mashua na motaboti. Katika usafiri huu zipo kazi kadhaa zinazojitokeza. Kuna manahodha, marubani, makuli, mabaharia, wachukuzi,

walinzi na wapishi. Katika miktadha na mazingira yote, hakuna mhusika wa kike hata mmoja. Usafiri wa majini ni wa polepole. Safari za meli kutoka bandari moja hadi nyingine zilichukua muda mrefu. Kutoka Aden hadi Mombasa meli iliyoitwa *El Nasser*, ilichukua usiku kucha kufika Mkalla kisha siku mbili kutoka Mkalla hadi Mombasa, mwandishi anaeleza kwamba ilikuwa safari ndefu (uk 26) . Kwingineko, meli iliyowasafirisha Shafi kutoka Bandari ya Butiaba hadi Pakwach ilichukua siku tatu. Mwandishi anasema;

Mwendo wa meli ulikuwa wa taratibu mno na sisi, kwa pupa kubwa ya safari tuliyokuwa nayo, tulihisi kama kwamba meli ile ilikuwa ikituchelewesha. Siku ya kwanza ilipita, na ya pili nayo ikapita. Siku ya tatu, saa kumi juu ya alama meli ilifunga gati kwenye bandari ndogo ya Pakwach (uk 202)

Maelezo haya yanaonyesha kwamba, safari za meli ni za taratibu na wafanyikazi hukaa muda mrefu majini. Manahodha walipambana na mawimbi na dhoruba mchana kutwa usiku kucha kwa siku kadhaa, wiki kadhaa au hata miezi kadhaa. Manahodha, mabaharia, makuli, wauza tiketi, wapishi na walinzi katika meli wote ni wanaume. Kazi zinazofanywa na mabaharia ni ngumu na hatari. Kazi ya kuparamia mameli na kuyagonga kutu iliyong'ang'anaa. Walifanya hivyo kwa kuning'inia kwenye kamba kutoka asubuhi mpaka jioni huku wameshika nyundo mkononi kuondoa kutu kwenye chuma cha meli. Maelezo haya yanaonyesha jinsi kazi katika mazingira ya usafiri zilizo ngumu. Mbali na kazi hii, makuli na makarani walikuwa wakipakia na kupakua mizigo melini. Vile vile kulikuwa na wachukuzi ambao walibeba mafurushi ya mizigo. Kwa mfano mwandishi alipowasili bandarini Unguja alipata watu wengi wakishughulika na kazi pale bandarini. Anaeleza;

Wachukuzi walikuwa matumbo wazi, miili yao ikinyekenyajasho lililokuwa likiwatiririka. Walikuwa wakiburura marikwama yaliyokuwa yamesheheni magunia (uk 421)

Wachukuzi wanaotajwa walikuwa wanaume. Katika bandari hii pia mwandishi anaeleza kwamba walikuwepo wanawake wa Kigorolana ambao walikuwa wamesimama nje ya maghala ya vyakula ili wafagie baada ya wachukuzi hao kutoa magunia yao. Kutohusisha wanawake na kazi ya uchukuzi na kuwahusisha na ufagizi kunaelezeka kiathropolojia na kihistoria.

Mwandishi pia anaeleza kwamba, wauza tiketi walikuwa bandarini kila wakati, kidirishani wakiuzia wasafiri tiketi hasa za siku iliyofuatia (uk 223). Ilibidi wawepo bandarini mchana kutwa, usiku kucha ikizingatiwa kwamba safari za meli zilifanywa mchana na usiku. Ilikuwa ni lazima abiria wapange foleni. Meli zilisafiri kulingana na wakati maalumu uliokuwa umetengwa. Wasafiri waliogopa kukosa nafasi kwani meli ilipoondoka, wangengojea siku kadhaa irudi kubeba abiria wengine. Kwa misingi hii kulikuwa na misongamano ya wasafiri bandarini. Walinzi katika safari za meli walikuwa na jukumu la kuhakikisha kwamba palikuwa na utaratibu wakati wa kuingia melini. Meli zilibeba abiria wengi kupita kiasi. Ilibidi pawe na walinzi wa kuhakikisha usalama wa safari. Walinzi hao walikesha bandarini kwani meli zingewasili na kuondoka wakati wowote ule. Kazi ya wauza tiketi na walinzi imehusishwa na wanaume. Kutokuwepo kwa wahusika wa kike kunaelezeka kianthropolojia na kihistoria.

Kazi ya upishi katika meli imejitokeza pale mwandishi anawawasilisha wanaume wawili mmoja akiitwa Nuhu, mpishi katika meli ya Simu bandarini Mombasa. Alikuwa mkarimu na alikuwa akimpa Shafi chakula alipofika pale (uk 31). Mpishi mwingine wa kiume ni yule alikuwa katika meli ya *M.V Ubena*, ambayo Shafi anasafiria kutoka Zanzibar hadi Aden mara ya kwanza. Alipoishiwa na chakula alianza kuomba mpishi yule. Alishangaa siku moja kumpata mpishi akitoa jichwa la nguruwe kwenye *oven*. Kama Muislamu hakuwa na la kufanya ila kula chakula

cha mpishi yule (uk 16). Katika muktadha wa usafiri melini kuna wapishi wa kike katika muktadha wa kinyumbani ila si wa kikazi. Kutokuwepo kwa wanawake katika miktadha ya kazi ya upishi safarini kunaelezeka kianthropolojia na kihistoria.

3.6.1.3 Usafiri wa treni

Treni ni chombo kinachosafiri kwenye reli kinachotumia injini ya kuburura mabehewa kadhaa ya mizigo au ya kubeba abiria. Katika *Mbali na Nyumbani*, usafiri wa treni umejitokeza katika uhalisia wa kipindi hicho kihistoria. Mwandishi na wenzake walisafiri katikati ya miji ya Afrika Mashariki na hata nje ya eneo hilo kwa kutumia treni. Kazi zinazojitokeza katika mazingira ya usafiri wa treni ni walinzi,wakagua tiketi. Walinzi walikuwa na jukumu la kutuliza zogo na ghasia za wasafiri wakati wa kuingia melini. Wakaguzi walizunguka ndani ya mabehewa yote wakikagua tiketi za usafiri. Wasafiri ambao hawakuwa na tiketi walihangaika na kujificha katikati ya wasafiri wenzao kwa kuwa wangepatikana wangeshushwa na kuadhibiwa vikali. Hii ilikuwa kazi ngumu kwa wakaguzi ikizingatiwa kwamba, wasafiri walikuwa wengi sana. Mwandishi anaeleza kwamba walipokuwa wakitoka Bungoma, alikuwa amelala wakati aliamshwa na mkagua tiketi. Mwandishi anaeleza;

Alikuwa singasinga mtu mzima aliyejizonga lemba kichwani.
Tita la sharafa ya ndevu zilizokolea mvi lilikuwa limemzunguka
usoni. Alinichokoa kwa gongo kule nilikojipachika akanipigia
kelele kwa hasira, “Tiket” (uk 172)

Maeleo haya yanaonyesha jinsi kazi ya kukagua tiketi za wasafiri ilivyokuwa ngumu. Ilibidi mkaguzi awaamshe abiria waliokuwa usingizini mbali na kuwatafuta wale walikuwa wakikwepa kulipa nauli. Mwandishi hajawasilisha wahusika wa kike katika muktadha huu. Kutokuwepo kwao kunaweza kuelezeaka kianthropoljia na kihistoria kuliko kiusawiri.

3.6.1.4 Usafiri wa ndege

Katika usafiri wa ndege, wahusika wanaume ni marubani, wahudumu na makarani. Shafi, Hussein Mborouk na Suleiman Hemedi wanaondoka uwanja wa ndege wa Kiembesamaki, Unguja, kwa ndege ya Shirika la Ndege la Afrika Mashariki, aina ya ‘Dakota’. Katika ndege hiyo rubani na mhudumu ni wanaume. Mwandishi anatoa maelezo ya mhudumu kwa kusema;

Alikuwa kijana barobaro, aliyeavaa shati jeupe na suruali nyeusi. Alikuwa amekaza tai ya kahawia shingoni. Alibeba sinia iliyokuwa imejaa keki na alimpitishia kila abiria achukue..... (uk 439)

Katika uwanja wa ndege wa Nairobi, palikuwa na makarani Wazungu, wa Idara ya Uhamiaji waliokuwa wakikagua vyeti vya kusafiria. Mwandishi na wenzake wanapopanda Ndege la Skendinevia kusafiri hadi Ujerumanini wanapanga foleni ili wakaguliwe. Ilipofika zamu ya mwandishi, kijana wa Kiingereza aliyeokuwa na tambo la wastani alichukua pasi yake na kuikagua sababu ilikuwa imechorwa mstari mwekundu. Alimweleza kwa nini alikuwa amezuiliwa kuingia Sudan kabla ya kuruhusiwa kupanda ndege (uk 452) Ilikuwa saa mbili usiku. Kazi hizi zote katika uwanja wa ndege, Nairobi zilifanywa wakati wa usiku. Wafanyakazi katika uwanja huo walikuwa wameavaa makoti mazito ili kujikinga na baridi iliyokuwa ikizizima usiku ule. Maelezo haya yanaonyesha changamoto zilizoandamana na kazi katika usafiri wa ndege. Kule Zurich, katika uwanja wa ndege, palikuwa na wahudumu wa Shirika la Ndege la *Interflug* kuelekea Berlin. Mhudumu mmoja mwanamume alikuwa akilipisha kodi ya uwanja wa ndege (uk 458) Palikuwepo pia na makarani. Mwandishi anaeleza;

Nilimwuliza karani wa Shirika la Ndege la Interflug kama pale uwanja wa ndege lilikuwepo duka la kubadilisha pesa. Alinijibu kuwa lilikuwepo na alinieleza lilipokuwepo (uk 459)

Mazungumzo hayo yalitokea wakati mwandishi alikuwa akitafuta pesa za kulipia kodi ya uwanja wa ndege. Katika duka hilo alikuwepo mhudumu wa kiume. Alimweleza Shafi kwamba noti ile haikufaa kutumika wakati huo. Katika mazingira haya ya usafiri kuna mwanamke mmoja mpokezi katika ndege ya Skendinevia na mabanati wahudumu. Wahudumu wengine wote ni wanaume. Wanawake wamehusishwa kwa ufinyu. Kazi wanazofanya ni za kisaidizi. Kuhusisha wanaume katika kazi za urubani na wanawake kwa upokezi na uhudumu kunaelezwa kianthropolojia na kihistoria kama ubanifu katika nafasi za kazi za kihadhi.

3.7 Hitimisho

Katika sura hii tumeeleza dhana ya kutokuwepo kwa wahusika wa kike katika *Mbali na Nyumbani*. Kutokuwepo kumetumiwa kubainisha mazingira na miktadha fulani ambamo wanawake wamehusishwa kwa ufinyu na vile vile kubainisha mazingira na miktadha mingine ambamo wanawake hawapo. Tumeona kwamba, kuwepo finyu kwa wanawake katika miktadha fulani kunaelezeka kuwa ucheleweshwaji wao katika shughuli zinazotekelawa kuliko kudai kwamba wamenyimwa nafasi. Ucheleweshwaji wao unaelezeka kianthropolojia na kihistoria. Mazingira ambayo wanawake wamewasilishwa kwa ufinyu ni ya kisiasa. Katika mazingira ya kijeshi wanawake hawakuhusishwa. Katika mazingira na miktadha ya kidini, tumeona kwamba, katika dini ya Kiislamu, wanawake hawajapewa majukumu kama viongozi wa kidini au kuhusishwa katika mazungumzo ya kidini bali majukumu yao ni kutayarisha na kuandaa sherehe za kidini. Katika mazingira ya uhamaji na uhamiaji wanawake hawajahusishwa na uhamaji au uhamiaji wenye malengo ya kielimu, kisiasa, kidini au kijeshi.

SURA YA NNE

UKIMYA NA UCHELEWESHWAJI: SABABU ZA UWEPO NA UTOKUWEPO WA WAHUSIKA WA KIKE KATIKA *MBALI NA NYUMBANI*

4.0 Utangulizi

Katika sura ya pili tulibainisha wahusika wa kike katika *Mbali na Nyumbani* kwa kuonyesha uwepo wao katika mazingira na miktadha fulani pamoja na majukumu wanayotekeleza. Katika sura ya tatu, tumebainisha uwepo finyu wa wanawake katika mazingira na miktadha fulani na utokuwepo wao katika mazingira na miktadha mingine. Tumeona kwamba, majukumu ya kimsingi yanayoteklezwa na wanawake ni ya kijamii kama kuzaa na kulea watoto, kupika na kutunza nyumba. Majukumu ya kiuchumi na kikazi ambayo wanawake wanatekeleza katika *Mbali na Nyumbani* ni ya kiusaidizi tu. Majukumu ya kibiashara na utafutaji wa riziki yamepewa wanaume. Tumeona kwamba, pana uwepo finyu wa wanawake katika mazingira ya kielimu na kisiasa. Utokuwepo wa wanawake umejitokeza katika mazingira na miktadha yote ya kijeshi, miktadha fulani ya kidini, miktadha ya kisiasa, na miktadha fulani ya kikazi. Katika sura hii, tutajadili sababu za uwepo na utokuwepo wa wahusika wa kike katika *Mbali na Nyumbani*. Mijadala kuhusu sababu za uwepo na utokuwepo wa wanawake katika mazingira na miktadha itahusishwa na kipengele cha ukimya na cha ucheleweshwaji kwa mujibu wa Miller (1990) kama inavyodai nadharia ya anthropopolojia.

4.1 Uwepo wa wanawake kimajukumu: Ukimya wa kianthropolojia.

Katika sura ya pili, tumebainisha uwepo wa wanawake katika mazingira na miktadha ya kijamii kama vile, mazingira ya kijamii, mazingira ya kiuchumi na mazingira ya kielimu. Tumeona

kwamba, katika mazingira ya kijamii majukumu makuu ambayo wanawake wamepewa ni uzazi na ulezi pamoja na shughuli nyingine za kijamii kama kupika na kupanga nyumba. Katika mazingira ya kiuchumi tumeona kwamba, majukumu ya wanawake katika miktadha ya kikazi ni ya kiusaidizi kama kuhudumia wateja na kuwapokea katika hoteli na ofisi. Katika mazingira ya kielimu wanawake wana jukumu la kiusaidizi pia. Kianthropolojia, majukumu haya yalihusishwa na wanawake kwa kuwa mgao wa kazi kijinsia ulikuwa hivyo. Kihistoria wanawake walikuwa wategemezi huku wanaume wakiwa mihimili katika familia. Kwa misingi hii, mwandishi wa *Mbali na Nyumbani*, halengi kuwadhulumu, kuwadharau, kuwaonea au kuwanyima hadhi wanawake kama inavyoweza kutathminiwa na watafiti wengine. Katika hali halisi ya maisha ya wanawake, majukumu ya kinyumbani yalihusishwa na wanawake. Kwa hivyo, mwandishi amewawasilisha wahusika halisi wanaotekeleza majukumu halisi Kihistoria na Kianthropolojia. Ukweli ni kwamba, wanaume hawakuhusishwa na majukumu ya kinyumbani kama, kulea watoto, kupika, kufua nguo, kutafuta kuni na kuchota maji. Hii ndio sababu wahusika wa kiume katika *Mbali na Nyumbani*, kama Mzee Abdalla Ngazi anahuishwa na biashara huku bibi yake Biti Siti, bibi yake, akihusishwa na upishi (uk 57). Kwingineko wanaume manamba katika shamba la miwa la Kakira wanahuishwa na kazi huku wake zao wakihuhsishwa na ulezi wa watoto (uk 279). Hadi kufikia miaka ya sabini, jamii za Kiafrika hazikuwakubalia wanawake kufanya kazi nje ya miktadha ya kinyumbani kutokana na sababu ya uzazi na ulezi. Fauka ya hayo, watoto wachanga hukaa muda mrefu na mama zao kuliko muda wanaokaa na baba zao. Majukumu haya huchukua muda mrefu kukamilika kwa hivyo, wanawake wanalazimika kubakia nyumbani ili wayatekeleze majukumu hayo kwa njia inayofaa. Uwasilishwaji zaidi wa wanawake katika mazingira na miktadha ya kijamii pamoja na majukumu wanayotekeleza katika

Mbali na Nyumbani ni uhalisi wa maisha yao kianthropolojia, bali sio kuonewa, kudhulumiwa, kudhalilishwa au kunyimwa hadhi katika jamii.

4.2 Uwepo finyu wa wanawake: Ucheleweshwaji

Uwepo finyu wa wanawake katika mazingira na miktadha fulani katika *Mbali na Nyumbani* unahusiana na ucheleweshwaji wa wanawake kujiunga au kujihusisha na shughuli katika mazingira hayo. Ucheleweshwaji kwa mujibu wa Miller (1990:247-248) ni suala la Kihistoria ambalo linapaswa kuchunguzwa kwa kuangalia maendeleo ya wanawake wa Kiafrika Kihistoria katika mifumo ya kitamaduni, kielimu, kisiasa, kidini na kiuchumi yalicheleweshwa na taratibu na michakato ya kikoloni. Uchunguzi kuhusu historia ya wanawake utachangia pakubwa kuelewa jinsi maisha ya wanawake yalivyokuwa katika kipindi fulani cha kihistoria yakilinganishwa na jinsi yalivyo sasa. Kwa mfano, pale ambapo wanaume walikwenda vitani kutetea himaya ya mkoloni, wanawake walibaki nyumbani. Wanaume waliorudi kutoka vitani walikuwa na tajriba mpya, tajriba iliyowapanua mawazo, tajriba iliyowapa mwonoulimwengu mpya, iliyowawezesha kuona manufaa na faida za elimu, wakafahamu umuhimu wa kufanya kazi, kuekeza katika elimu. Wanaume walibadilishana tajriba hizi na wanaume wenzao, na kwa njia hiyo kuwapa msukumo. Wakati haya yakitendeka, wanawake walikuwa wamesalia pale pale walipokuwa. Hii ina maana kwamba kufikia wakati walipoanza kutanabahi, wanaume walikuwa wamepiga hatua kubwa. Hii ndiyo hali halisi inayojibainisha na kuibuka katika uwasilishwaji wa wahusika wa kike katika *Mbali na Nyumbani*.

4.3 Utokuwepo wa wanawake: Ukimya

Utokuwepo wa wanawake katika mazingira na miktadha mingine katika *Mbali na Nyumbani* unachukuliwa kama ukimya wao katika miktadha hiyo. Kama tulivyotaja hapo awali, ukimya kwa mujibu wa Miller (1990:248), waweza kuelezwa kianthropolojia na kihistoria. Katika jamii za Kiafrika, kulikuwepo na mila na desturi ambazo zilienziwa na kuheshimiwa na wanajamii. Mifumo ya kijamii pia ilikuwa na taratibu na mipangilio ambayo ilikubaliwa na wanajamii kwa jumla. Mifumo kama ya kitamaduni, kisiasa, kielimu na kidini iliongozwa na itikadi fulani za kijamii katika kipindi fulani kihistoria. Kwa mfano, katika jamii nyingi za Kiafrika, wanawake walikuwa wakiozwa baada ya kufikisha miaka kumi na miwili. Wasichana walipitishwa katika mila na desturi kama vile kutahiriwa kabla ya kuolewa. Zoezi hili lilienziwa na kuheshimiwa na hakuna msichana yejote angekiuka mila hii. Wachache waliokiuka walibandikwa majina na ilikuwa aibu kubwa kwao. Wanaume hawakukubali kuoa msichana ambaye alikuwa hajatahiriwa au kuoa msichana ambaye hakuwa ametimiza umri wa kuolewa. Ukoloni ulipoingia barani Afrika, mila na desturi nyingi za Waafrika ziliathiriwa sana na majilio ya dini. Baadhi ya masuala kama kuwatahiri wasichana yalianza kupingwa na wamishonari. Itikadi iliyokuwepo ilianza kubadilika ikawa kwamba, ni hatia kuwatahiri wasichana. Waafrika walianza kukubali mabadiliko kwa kuaminishwa kwamba, tamaduni zao zilikuwa chafu na zilikuwa zimepitwa na wakati. Waafrika wengi walianza kukubali na kufuata tamaduni za Kimagharibi. Kwa misingi hii, hali za maisha ya wanawake barani Afrika zilibadilika. Ukimya wa wanawake katika mazingira na miktadha fulani ni wa kihistoria. Ukimya katika elimu, siasa, jeshi mionganii mwa mifumo mingine ya kijamii ulivunjwa baada ya wanawake kutambua umuhimu wa elimu na faida zilizotokana na elimu yenyewe. Baada ya utambuzi huu, wanawake walianza kupigania haki na usawa katika mifumo ya kijamii na hii ndio maana hali zao za kimaisha zilibadilika.

Uwasilishwaji wao katika *Mbali na Nyumbani* unaakisi hali zao za kimaisha kipindi hicho, bali uwasilishwaji wao haulengi kuwapembeza au kuwatenga katika mifumo ya kijamii. Ukimya na ucheleweshwaji ni vipengele vinavyohusiana na kuchangizana kwa mapana. Ukoloni na ubeberu vilileta mabadiliko makubwa katika nchi za Afrika, mabadiliko ambayo yaliathiri masuala ya wanawake katika jamii. Baadhi ya mifumo na taasisi ambazo zilibadilika ni za kielimu, kisiasa, kidini na kijeshi. Ukimya wa wanawake katika miktadha fulani unamaanisha kuwepo kwa wanaume. Ucheleweshwaji wa wanawake katika miktadha fulani unamaanisha kwamba japo wanajitokeza, wanaume walikuwa tayari wametawala mazingira husika.

4.4 Ukimya na ucheleweshwaji wa wanawake katika elimu.

Karoki (2014:64) anasema kwamba, elimu ni ufunguo wa maisha na zaidi ya kumfaidi msomi mwenyewe, huifaidi jamii yake kwa jumla. Sisi tunasema kwamba, elimu ndiyo nguzo ya kuijendeleza kwa binadamu ye yote katika jamii. Mtu anapojipatia elimu, huwa amepata uwezo wa kujiendeleza na kujikuza katika shughuli za kisiasa, kiuchumi, kikazi na kidini mi ongoni mwa zingine. Kwa kujipatia elimu mtu hutambua umuhimu na faida zake. Kulingana na Miller (1990: 274-275), elimu ina uwezo wa kumpa mtu ujasiri. Usomaji humpa mtu uwezo wa kuujua na kuufikia ulimwengu wa nje, tamaduni zake na mifumo ya kijamii. Elimu ya nje humwezesha mtu kutambua mifumo tofauti nje ya jamii yake. Kujifunza tamaduni mpya humpa mtu kutambua baadhi ya mifumo katika jamii yake inayoonekana kumdunisha, kumdhalilisha na kumdhulumu na hivyo, inampa mtu uwezo wa kuvunja ukimya katika mifumo na taasisi za kijamii. Elimu anazungumzia Miller (k.h.j), ni ya nje, sio ya Kijamii. Yeyote anayeitaka lazima avuke mipaka ya Kijamii na kimaeneo ndipo akaipate. Sisi tunasema kwamba, elimu ya mwanamke ni ngao na nguzo yake katika masuala yote yanayomzunguka. Mwanamke

akielimika anapata uhuru wa kujiamulia na kutazama mifumo na itikadi za jamii yake kwa njia ya kiulimwengu kuliko kuvitazama kwa jicho la jamii yake tu. Katika taasisi za elimu mwanamke hupata kuingiliana na kutangamana na watu wenye tamaduni tofauti na wake na hivyo, anapata fursa ya kutambua ukweli na uhalisi wa mambo. Elimu ya nje, tofauti na ile ya kitamaduni humpa mtu fursa ya kuvuka mipaka ya jamii yake, nchi yake na hata bara lake na hivyo, mwono - ulimwengu wake unabadilika kabisa.

Kihistoria, kabla ya majilio ya wakoloni barani Afrika, elimu iliyotolewa kwa vijana ilinua kuwatayarisha kuchukua nafasi katika jamii zao, bali sio kuwapa fursa ya kuvuka mipaka au kujihuisha na shughuli za jamii nje ya mipaka ya Kiafrika. Mafunzo waliyopewa yalikuwa ya kisanaa, michezo, uimbaji, uchoraji na utamaduni kwa jumla. Wavulana walifunzwa peke yao nao wasichana walipokea mafunzo bila kutangamana na wavulana. Elimu hii ilikuwa ikipitishwa kwa mifumo na mipangilio ya kitamaduni. Wasichana walipata elimu kuhusu majukumu ya kinyumbani kwa lengo la kuwatayarisha kuwa wake, mama, wapishi, walezi na watekelezaji wa shughuli nyingine za kinyumbani. Mafunzo kama vile ukunga yalikuwa yakirithishwa familia fulani fulani. Si wasichana wote walifunzwa ukunga. Hii ilikuwa kazi muhimu sana na wakunga waliipitisha kwa kizazi chao tu, ili kuhifadhi sifa na faida zilizotokana nayo. Wakunga walikuwa wakilipwa au kupewa zawadi baada ya kuwasaidia kina mama kujifungua. Njia kuu ya kuptisha maarifa ya ukunga ilikuwa kuiga ambapo walihitajika kuangalia kwa makini kilichofanywa na kuiga kwa kufanya vivyo hivyo. Ilitarajiwa kwamba, kabla ya msichana kubaleghe, awe amehitimu mafunzo yote ili aozwe. Jamii nyingi ziliwaoza wasichana wakiwa na umri wa miaka kumi na miwili. Mafunzo ya kitamaduni hayakuvuka mipaka ya jamii husika. Mafunzo hayo yalifanana na kutofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine. Hapakuwepo na vitabu vyat

kusomwa kuhusu tamaduni za jamii nyingine hadi kufikia miaka ya sabini. Elimu hii ilipitishwa kwa njia ya nyimbo, methali, vitendawili na nahau yaani, fasihi simulizi ya jamii husika.

Wavulana nao walipewa mafunzo nje ya miktadha ya kinyumbani kama ya ufugaji, usasi, utabibu kwa kutumia miti shamba, uchongaji, ulinzi, mafunzo ya kivita na uhunzi mionganoni mwa mengine. Nia kuu ilikuwa kuwatayarisha kuwa wasimamizi na walinzi wa familia ambao wangechukua nafasi zao katika jamii. Baadhi ya kazi zilikuwa za kurithishwa katika familia. Kazi kama utabibu na uhunzi zilikuwa zikienziwa na zenye faida kwa familia kwa hivyo wazee walitaka zibakie tu katika familia zao. Ujuzi huu ulifunzwa kwa njia ya siri ili usienee. Mifumo hii ya elimu ilienziwa na kuheshimiwa hadi ilipoanzishwa elimu ya kikoloni. Ukoloni na ubeberu uliibadilisha kabisa elimu ya kitamaduni barani Afrika. Elimu ya kikoloni haikukusudiwa kutoa mafunzo ya jando na unyago, bali ilikusudiwa kuwaandaa vijana wapate elimu itakayowakengeusha ili wawe watumishi waaminifu kwa mfumo wa kikoloni na wasaliti wa mfumo mzima wa jadi wa jamii zao. Baadhi ya Waafrika waliamini kwamba, kuelimisha mwanamke kungeathiri majukumu yake kama mke na mzazi. Katika jamii ambazo wasichana waliolewa baada ya kutimiza miaka kumi na miwili, elimu ilionekana kama kikwazo katika maendeleo ya kijamii. Wavulana walihimizwa kujiunga na taasisi za elimu huku wasichana wakifungiwa kulingana na mila na desturi za jamii. Wanaume walipata fursa kubwa ya kupokea elimu ya kimagharibi na hivyo wakawa wa kwanza kutambua faida zake. Wanaume walipata fursa ya kuujua ulimwengu wa nje kupitia elimu ya kikoloni kinyume na awali ambapo elimu ya kitamaduni ilifungiwa katika mipaka ya jamii husika. Wanaume walianza kujihusisha na masuala ya kisiasa, kiuchumi, kijeshi na kidini kufuatia mabadiliko yaliyotokana na elimu ya kimagharibi. Kihistoria, nchi za Afrika zilianza kujipatia uhuru katika miaka ya hamsini. Misri

ilipata uhuru mnamo mwaka wa 1956, nayo Sudan mwaka mnamo wa 1958.Baadaye nchi nyiningine zilipatia uhuru kuanzia mwaka wa 1960. Ni katika kipindi hiki ambapo masimulizi ya *Mbali na Nyumbani* yanajikita.

Katika mazingira ya kielimu tumeona kwamba, kuna miktadha ambapo wanawake hawakuhusishwa. Shafi amewataja wanafunzi wenzake na wote ni wanaume. Kwa mfano, Mohammed Masoud Seif na Mohammed Khamis Nura waliosoma naye *Chuo cha Seyyid Khalifa*, mwaka wa 1957, kisiwani Zanzibar. Katika *Comorian School* Shafi alisoma na Abdalla Juma Bulushi, Abdalla Elyas na nduguye Kassim. Utokuwepo wa wanafunzi wa kike katika taasisi hizi ni ukimya halisi. Ukimya wa wanawake katika taasisi hizi za elimu unatokana na masuala ya kihistoria, kitamaduni pamoja na miundo ya kijamii kabla ya ukoloni na baada ya ukoloni. Elimu ya wakoloni ilipokelewa kwa njia ya kupembeza kwa wanawake huku wavulana wakipewa nafasi chanya. Itikadi iliyokuwepo kwamba elimu ya mwanamke haina thamani kwa kuwa kimsingi mwanamke akishabaleghe ataolewa na imani kwamba mwanamke hapaswi kujihusisha katika utafutaji wa riziki vilichangia sana kupembeza kwa wanawake katika taasisi za elimu. Mwanamke alitarajiwa kuwa mzazi, bibi na mama bali hakutarajiwa kuwa mfanyakazi. Wanaume ndio walikuwa mihimili katika familia kwa hivyo walihimizwa kuijiunga na taasisi za kielimu ili wapate kazi nzuri za kuwasaidia kukimu familia zao. Amadiume (1998:134) ameelezea jinsi wanawake walijiunga na taasisi za elimu nchini Nigeria. Ameonyesha idadi ya wavulana na ile ya wasichana katika shule mbali mbali. Katika shule nne zilizosimamiwa na *United Free Church of Scotland* zilikuwa na wavulana 1,592 na wasichana 132. Katika shule nne zilizosimamiwa na *Roman Catholic Church* wavulana walikuwa 213 na wasichana 109. Shule tisa zilizosimamiwa na *Niger Delta Pastorate* zilikuwa na wavulana 538

huku wasichana wakiwa 184. Shule iliyokuwepo ya umma ilikuwa moja tu na ilikuwa ya wavulana pekee. Shule mbili tu ndizo zilikuwa zikitoa elimu ya juu. Masomo yaliyofunzwa ni ushonaji, useremala na upigaji chapa na yalichukuliwa kuwa ya wanaume. Nafasi za kazi katika serikali ya kikoloni basi zilikuwa wazi kwa wanaume kwa kuwa ndio waliopata elimu na mafunzo. Amadume (k.h.j) amehitimisha kwa kusema kwamba wanawake walitengwa. Sisi tunasema kwamba, huku si kutengwa bali ni uhalisi wa mambo jinsi yalivyokuwa miaka ya hamsini. Kutokana na maelezo haya wanawake walicheleweshwa kuijunga na taasisi za elimu ya kimagharibi na hivyo mwandishi wa *Mbali na Nyumbani*, ameonyesha hali halisi ya wanawake katika mazingira ya elimu katika nchi ya Zanzibar. Hatuwezi kudai kwamba, walikuwa wametengwa. Idadi ya wavulana na wasichana waliojiunga na shule kipindi hicho katika mifano ya Amadume ni dhihirisho la uhalisi Kihistoria. Kwamba idadi ya wanawake waliojiunga na taasisi za kielimu ilikuwa ndogo. Elimu ya wanawake ilianza kuhimizwa na kupata kasi miaka ya sabini. Kwa hivyo, utokuwepo wa wanafunzi wa kike *Comorian School* na *Chuo cha Ualimu cha Seyyid Khalifa* katika *Mbali na Nyumbani* sio kunyimwa nafasi kwa wanawake ila ni ukimya unaotokana na itikadi za kijamii pamoja na taratibu na mipangilio ya kijamii kuhusu maisha ya wanawake. Kucheleweshwa kwa elimu ya wanawake kuliathiri kazi za wanawake. Nwabara (1977: 60 - 62) amesema kwamba, wanaume ndio walioajiriwa kama makarani na wahudumu katika mashirika ya wakoloni barani Afrika kwa kuwa wao ndio walikuwa wamepata elimu yao. Wanawake walianza kutambua umuhimu wa elimu na faida zake kuanzia miaka ya sabini. Vyama vinavyotetea elimu ya wasichana viliundwa na vikaanza kuwashamasisha wasichana na wazazi kuhusu umuhimu na faida za kuwapa watoto wasichana elimu sawa na watoto wavulana.

Kwa upande mwingine, wanawake wamehusishwa kwa ufinyu katika taasisi za juu za elimu. Huo ulikuwa mwaka wa 1961 wakati Shafi alisafiri kwenda Kairo kupata elimu baada ya kutoroka katika *Chuo cha Ualimu cha Seyyid Khalifa* kule Zanzibar akiwa mwaka wa tatu. Katika *Mbali na Nyumbani* wanawake waliohusishwa na elimu ya juu nje ya miktadha ya nchi zao ni wawili; Zainabu na Najaat. Zainabu, mwanamke pekee katika Chuo Kikuu cha Khartoum na Naajat pia ndiye alikuwa mwanamke pekee katika Chuo Kikuu cha Kairo. Miller (1990 : 261) anasema kwamba, katika jamii nyingi za Kiafrika, wanawake walicheleweshwa kielimu. Kwa maoni yetu ucheleweshwaji huu katika taasisi za juu za kielimu ultokana na itikadi na mifumo ya kijamii pamoja na masuala mengine kama kutokuwepo kwa taasisi za juu za kielimu za wanawake katika nchi hizo na kubanwa kwa wanawake katika uhamaji na uhamiaji. Vinginevyo, wanawake hawakutambua umuhimu na faida za elimu mapema kama wanaume kwa kuwa hawakuruhusiwa kushiriki katika Vita vya Kwanza na Vya Pili vya Dunia. Kushiriki kwa wanaume katika vita hivi kuliwazindua wanaume kielimu na kisiasa baada ya kuingiliana na watu nje ya miktadha ya jamii za Kiafrika. Wanaume waligundua mapema faida za Elimu ya Kimagharibi, kwa hivyo wakawa na hamu ya kuipata. Wanawake wachache waliojiunga na taasisi za juu za elimu walitoka katika familia ambazo zilikuwa zimetambua umuhimu na faida za elimu hii. Miller (1990:273) anatoa mfano wa Mariama Bâ, ambaye baada ya kupata Elimu ya Kimagharibi aliitumia kifasihi kuwahamasisha wanawake wenzake. Mariama Ba alitambua kwamba, vitabu vilimpa mwanamke utambuzi wa maisha ya nje ya jamii yake. Kwamba Elimu ya Kimagharibi ingemwezesha kupata vyeo na daraja sawa na wanaume katika jamii yake. Alikuwa ametambua kwamba hapakuwa na tofauti kati ya mwanamke na mwanaume na kwamba, tamaduni za jamii yake ndizo ziliwaaminisha watu kuwa, mwanamke alipaswa kuwa chini ya mwanaume. Mariama Bâ alitambua kwamba, wanawake katika jamii yake wakipata

Elimu ya Kimagharibi wangekuwa na uwezo wa kufanya mambo kwa njia tofauti kabisa kinyume na taratibu za jamii yake. Baba yake Mariama Bâ alikuwa mtumishi wa umma na hivyo, alikuwa ametambua umuhimu na faida za elimu ya mwanamke.

Kwa upande mwengine, Naajat ni mfano mzuri wa wasichana waliobahatika kupata elimu ya juu. Mama yake alikuwa Mmisri na baba yake alikuwa Mwingereza aliyejamia Misri kuchimba vifusi na kuselelea Misri baada ya kukutana na mama yake Naajat. Kwa maoni yetu, Naajat alitoka katika familia iliyotambua umuhimu na faida za elimu ya mwanamke kwa kuwa baba yake mwenyewe alikuwa msomi. Vinginevyo ni kwamba, nchi ya Misri ilijipatia uhuru mnamo mwaka wa 1956 na inatarajiwa kwamba uhuru huu uliwakomboa na kuwastaarabisha Waafrika. Hata hivyo, ni wazi kwamba, wanawake waliojiunga na taasisi za juu walikuwa wachache mno. Tumeshataja kwamba, elimu ya kikoloni iliwfikia wanawake wachache na hata katika baadhi ya nchi za barani Afrika hapakuwepo na mwanamke hata mmoja aliyejapata elimu ya juu hadi kufikia miaka ya sitini. Miller (1990:268-270) amesema kwamba, idadi ya wanawake wasiojua kusoma na kuandika barani Afrika ni mara nne ile ya wanaume wasiojua kusoma na kuandika. Jinsi kiwango cha elimu kinavyopanda ndivyo idadi ya wanawake inavyopungua.

Katika *Mbali na Nyumbani*, Zainabu amevuka mipaka ya Zanzibar ili kuisaka elimu ya juu, yeye ndiye mwanamke wa pekee katika Chuo Kikuu cha Khartoum. Uwepo wa Zainabu katika Chuo Kikuu cha Khartoum, mbali na kushadidia ucheleweshwaji wa wanawake katika elimu ya juu, unaashiria kuvunjwa kwa ukimya wa wanawake katika elimu ya juu. Uwasilishwaji finyu wa wanawake katika mazingira ya elimu basi umesababishwa na ucheleweshwaji wao katika kuijunga na taasisi za elimu ambazo zingewapa fursa ya kuvuka mipaka ili kuisaka elimu ya juu.

Zainabu na Naajat sio wawakilishi wa wanawake wachache waliobahatika kupata elimu ya juu kama inavyoweza kukisiwa au kuchukuliwa kiusawiri, bali ni uhalisi wa wanawake katika taasisi za juu za elimu Kihistoria. Hadi kufikia mkesha wa Vita vya Pili vya Dunia, kama anavyooleza Miller (k.h.j), elimu ya wanawake ilisemwa kwamba haikuwepo. Taasisi za elimu za wanawake zilikuwa chache hadi kufikia mwaka wa 1960. Kianthropolojia, wakati wa ukoloni barani Afrika, watawala na watawaliwa hawakuona umuhimu wa kuwaelimisha wasichana kwa kuwa itikadi iliyotawala ni kwamba, elimu ya mwanamke haikuwa na faida yoyote kwa kuwa majukumu ya wanawake yalikuwa ya jikoni. Waafrika wenyewe waliamini kwamba, hata msichana akipata elimu ataishia kuolewa tu, jambo ambalo lingekatisha matarajio yake ya kufanya kazi. Kwa misingi hii, wanawake katika *Mbali na Nyumbani* hawajatengwa wala kunyimwa nafasi katika taasisi za elimu, bali ucheleweshwaji wao unaakisi uhalisia wa kihistoria.

Katika Chuo cha Bernau, Ujerumani, palikuwa na wanafunzi wengi. Wanafunzi hao walitoka nchi tofauti tofauti za ulimwengu kama Uingereza, Afrika Mshariki, Afrika Magharibi, Afrika Kaskazini na India. Katika muktadha huu, hakuna mwanafunzi wa kike anayetajwa. Sababu ya utokuwepo wa wanafunzi wa kike kutoka Afrika katika Chuo cha Bernau, Ujerumani, kwa maoni yetu, kunatokana na ubanifu wao katika uhamaji na uhamiaji kwa shughuli za kielimu kipindi hicho cha kihistoria. Hata hivyo, wanawake katika nchi za Ulaya pia walicheleweshwa kielimu. Dyhouse (1995) katika “*No Distinction of Sex? Women in British Universities 1870-1939*”, anasema, wanawake walipoanza kugundua kwamba elimu ndiyo ingekuwa nguzo kuu ya kuijunga na nyanja zingine walianzisha harakati za kielimu na kisiasa. Ametoa mfano wa wanawake watatu kule Uingereza, Emilly Davies na dada wawili Elizabeth na Millicent Garrett. Wanawake hawa waligawana majukumu na kuanzisha taasisi za wanawake. Emilly alianzisha,

Girton, chuo cha kwanza cha wasichana huko *Cambridge* mwaka wa 1869. Elizabeth Garrett alikuwa mwanamke wa kwanza kuhitimu utabibu katika chuo hicho. Millicent alianza kutetea haki za wanawake za kupiga kura. Juhudi za wanawake hawa zilichochea pakubwa kuvunjwa kwa ukimya wa wanawake kielimu na kisiasa. Hata hivyo, elimu ilitangulia siasa. Kilichochea wanawake hawa wavunje ukimya wao katika elimu ni kutokubaliwa kupiga kura, kutopewa shahada baada ya kuhitimu na kutokubaliwa kufanya masomo yaliyohusishwa na wanaume. Changamoto zilizoandamana na kuanzishwa kwa elimu ya wanawake kule Uingereza ni thibitisho kwamba, elimu ya wanawake ulimwenguni haikuthaminiwa na ndio maana ilicheleweshwa. Kwanza, masomo ya wasichana yalikuwa tofauti na ya wavulana. Wasichana hawakufunzwa sayansi, uhandisi, hesabu na matibabu. Herbert Spencer (1912) alidai kuwa wanawake kujihusisha na masomo hayo kungepunguza uwezo wao wa kupata watoto. Utafiti ulifanywa kuchunguza ukweli huu na matokeo yakaonyesha kwamba, wanawake waliosoma walikuwa na nafasi pana na bora zaidi ya kupata watoto kuliko wale ambao hawakuwa wameelimika. Alidai pia, kuwafunza wasichana hesabu kulihitaji mafunzo mengi na muda mwingi ilhali matokeo yalikuwa ya chini. Pili, hata wanawake wachache waliobahatika kuhitimisha masomo yao ya juu hawakutuzwa shahada kwa imani kwamba wakipewa shahada watakuwa na mamlaka ya kupiga kura, kuwania nyadhifa kuu serikalini na taasisi za kielimu. Wanaume walipinga vikali jambo hili hasa katika chuo cha Cambridge na Oxford hadi kufikia mwaka 1920 na 1921 wakati wanawake wa kwanza walipewa shahada. Kufikia mwaka 1926, wanawake kumi na wawili walipata nafasi kama wahadhiri. Hata hivyo, hawakukubaliwa kushiriki katika mazungumzo au kupiga kura katika idara zao chuoni. Dorothy Garrod wa *Newnham* ndiye alikuwa mwanamke wa kwanza kuwa Profesa wa akiolojia mnamo mwaka wa 1939. Kufikia mwaka wa 1948, wanawake walianza kutambuliwa kama wanachama katika vyuo

vikuu lakini uwezo na mamlaka ya kuwasajili wanawake ulibakia mikononi mwa wasimamizi wa vyuo hadi kufikia miaka ya sabini. Mfano wa Uingereza unatuchorea picha nzuri ya masuala yaliyochangia ucheleweshwaji wa elimu ya wanawake. Tumeona kwamba, itikadi za kijamii pamoja na masuala ya kijinsia vilichangia kucheleweshwa kwa elimu ya wanawake. Masomo ambayo Shafi na wenzake walipata yalikuwa yakihuishwa na wanaume. Shafi alisomea mambo ya uchumi na biashara nao wenzake Suleiman na Hamisi wakasomea masuala ya kisiasa. Utoaji wa Elimu ya Kimagharibi hata ulipoanza kuwafikia wanawake, palikuwa na tofauti kati ya nyanja za wanawake na zile za wanaume. Wanaume walihuishwa zaidi na uhandisi, udaktari, masuala ya biashara na uchumi, hesabu na ujenzi. Wanawake walihuishwa na masuala ya upishi. Masomo haya ndiyo yaliwawezesha wanaume kupata kazi zinazochukuliwa kuwa za hadhi ya juu huku zile za wanawake zikichukuliwa kuwa za hadhi ya chini. Suala la ukimya na ucheleweshwaji wa wanawake katika elimu ndilo linalochangia pakubwa kucheleweshwa kwa wanawake katika mazingira ya kijeshi na kisiasa katika *Mbali na Nyumbani*.

4.5 Ukimya na Ucheleweshwaji katika kujiunga na jeshi.

Mojawapo ya mazingira ambayo wanawake hawapo ni mazingira ya kijeshi kama tulivyobainisha katika sura ya tatu. Katika mazingira haya, kuna askari polisi, askari wa magereza, askari jeshi na wapiganiaji uhuru. Katika miktadha hii yote, hakuna wanawake waliopewa majukumu yoyote. Askari polisi wamepewa majukumu ya ulinzi, ukaguzi wa tiketi na kodi, kushika doria katika maeneo ya mipaka, kulinda mahabusu katika vituo vya polisi na kutia wahalifu mbaroni. Sababu kuu ya utokuwepo wa wanawake katika mazingira ya kijeshi ni kwamba, hizi ni kazi ambazo kihistoria na kianthropolojia zilihusishwa na wanaume. Kihistoria, wanawake waliohusishwa na masuala ya kivita hawakupewa majukumu ya kupigana au hatia

kutumia silaha. Jones (2000 : 131), katika “*Women Warriors: A History*” anasema kuwa, wanawake walianza kuhusishwa na mazingira ya kijeshi wakati wa Vita vya Kwanza vya Dunia. Miaka karibu mia moja baada ya Vita vya Kwanza vya Dunia, tamaduni nyingi bado haziwaruhusu wanawake kuwa katika mstari wa mbele katika mapigano. Sababu zinazochangia kutohusishwa kwao ni za kitamaduni, kijamii na kimaumbile. Kwa mfano, katika taifa la Israel, watu wengi hufikiri kwamba wanawake wakishiriki katika mapigano, mshikamano waweza kuvunjika kutokana na hali ya wanawake kupata mimba, au kutekwa nyara na kuteswa, Harfield (2005:243). Wanawake walianza kushiriki katika mapigano miaka ya sabini na themanini japo palikuwepo na nchi ambazo zilianza kuwapa mafunzo ya kivita kabla ya miaka hii. Kwa mfano, Holm na Jean (1993) wanasema kwamba, mwaka wa 1967, nchini Congo, wanawake mia moja na hamsini walipata mafunzo ya “makomando”, japo haijulikani walihuushwa kwa kiasi gani katika mapigano. Kwa upande mwingine, Israel ilianza kuwafunza wanawake upiganaji mwaka wa 1948 hasa wanawake ambao hawakuwa wameolewa na wale hawakuwa na watoto. Wakati huo walitumika kama wauguzi, wapokezi wa simu, makarani na wakufunzi katika vitengo vya kivita. Kwa sasa katika nchi hiyo, inamlazimu kila mwanamke kupata mafunzo ya kupigana. Tumeona kwamba, wanawake ambao waliruhusiwa kupata mafunzo ya kivita katika nchi ya Israel Kihistoria ni wale ambao hawakuwa wameolewa na wale hawakuwa na watoto. Jambo hili linashadidia ukweli kwamba, maumbile ya wanawake na majukumu yao ya kijamii yaliwazuia kuingia katika shughuli za kivita. Rosaldo (1974:24) ametathmini tofauti kati ya kazi za wanaume na wanawake kwa njia ya ukinzani. Amesema kuwa, wanawake walihuushwa na kazi za kinyumbani kimsingi huku wanaume wakihuushwa na kazi za kiziada nje ya miktadha ya kinyumbani kama vile, siasa na shughuli nyingine katika nyanja za kijeshi. Itikadi ilikuwa

kwamba, mazingira nje ya miktadha ya kinyumbani si salama kwa wanawake na vile vile, kazi nje ya miktadha ya kinyumbani zilikuwa ngumu kwa wanawake.

Rosaldo (k.h.j) amedai kuwa, kushiriki kwa wanawake katika nyanja tendaji kama vile kutafuta riziki na nyanja za kivita kwaweza kukatizwa kutokana na wakati wao kujitolea katika uzazi na ulezi. Anasisitiza kwamba, haya si mambo ya kiakili na hayahitaji mpangilio. Kwa misingi hii sababu za utokuwepo wa wanawake askari polisi, wanajeshi au wapigania uhuru katika *Mbali na Nyumbani* unatokana na ukimya kianthropolojia kwamba, masuala ya kijamii na kitamaduni kama vile maumbile yao na majukumu yao ya kimsingi kama vile kulea, kuzaa na kutunza watoto yaliwazuia kuingia katika shughuli za kijeshi au kivita. Kufungiwa kwa wanawake katika mazingira ya kinyumbani wakizaa na kulea watoto ni mambo yaliyochangia kucheleweshwa kwao kujiunga na taasisi za kielimu ambazo zingewafungulia nafasi za kuajiriwa katika jeshi. Hii ndio maana, baada ya miaka ya sabini, wanawake walianza kuonekana katika nyanja za kijeshi na hata baadhi wakapewa vyeo. Kwa mfano, hapa nchini Kenya, wanawake walicheleweshwa kuingia katika majeshi ya nchi kavu, ya angani na ya majini. Ucheleweshwaji huu haupaswi kutathminiwa kama kutengwa bali masuala ya kimaumbile na majukumu ya kimsingi ndiyo yalichangia pakubwa. Wanawake walipoanza kupigania usawa wa kijinsia, baadhi ya majukumu ambayo yalifikiriwa kuwa ya wanaume yalianza kutekelezwa na wanawake. Wanawake walioanza kujiunga na jeshi mwanzoni walipewa kazi za uuguzi, ukarani na uendeshaji wa mitambo ya simu. Baadaye wanawake katika majeshi ya Kenya walianza kupewa vyeo na nafasi ya kupigana sambamba na wanaume. Hadi kufikia mwaka wa 1991, palikuwa na mwanamke mmoja tu aliyeendesa gari la kivita. Kulingana na gazeti la “*The Standard*,” 26, Oktoba 2011, msemaji wa Majeshi Meja Emmanuel Chirchir, alisema kwamba kati ya wapiganaji waliokuwa

wamepelekwa Somalia kwa shughuli ya “*Operation Linda Nchi*”, walikuwepo wapiganaji hodari wa kike zaidi ya mia moja. Katika utafiti wetu, tumegundua kwamba, pana wanawake katika majeshi yote yanayolinda nchi yetu walio na vyeo sawa na wanaume. Kwa mfano, Meja Nora Koech ndiye aliyekuwa mwanamke wa kwanza kujiunga na chuo cha mafunzo ya uendeshaji ndege za kivita mwaka wa 2001 na akahitimu mwaka wa 2006. Kwa sasa anaendesha *Y 12* (ndege ya kivita). Koplo Benedict Kikechi kwa sasa ni afisa msimamizi mkuu katika idara ya ndege. Wengine ni Kopro Ann Mbaluka, mhandisi anayehusika na urekebishaji wa ndege zikiwa angani. Sagenti Lina Chebet naye ni mhandisi katika ndege inayombeba Raisi wa Taifa la Kenya. Kutokana na maelezo haya tunaweza kusema kwamba, japo wanawake walicheleshwa katika masuala ya kivita hatuwezi kudai mwandishi wa *Mbali na Nyumbani* amewatenga katika kazi yake. Kwa maoni yetu, amewasilisha wanaume kihalisia katika mazingira na miktadha ya kijeshi, uhalisia ambao ni wa Kihistoria. Katika masharti ya kuwaajiri wanawake katika majeshi, sharti la saba katika barua za kuwaalika wanaotaka kujiunga na kazi za kijeshi linasema; “*Wananake wanaotaka kujiunga na mafunzo ya kijeshi, WASIWE wajawazito au wapate mimba wakati wa kusajiliwa au wakati wa mafunzo*”. Kwa maoni yetu, sharti hili linatokana na maumbile ya wanawake bali sio kuwadhalilisha au kuwanyima nafasi katika jeshi. Ni muhimu kutaja kwamba, mwanamke akiwa mjamzito hawezi kuvumilia mazoezi yanayoandamana na mafunzo ya kijeshi na hata akivumilia mimba ile inaweza kuathiriwa.

Mataifa yaliyoendelea kama Marekani yalianza kuwaajiri wanawake katika jeshi lakini kufikia miaka ya sabini wanawake hawakuruhusiwa kuwa mstari wa mbele katika vita. Wanawake pia hawakuruhusiwa kushiriki katika shughuli za kivita kwa kuwa yalichukuliwa kuwa mazingira hatari kwao. Hadi kufikia sasa, kuna nyanja ambazo huhusishwa na wanaume pekee. Kwa

mfano, nchi ya Marekani kwa sasa inaruhusu wanawake kujiunga na jeshi. Hata hivyo, Skaine na Rosemarie (1999) wanasema kwamba, pana vizuizi vyta kimaumbile ambavyo wanawake hawawezi kufikia. Wanatoa mfano wa wanawake kumi na tisa ambao walijiunga na *Ranger School* mwaka wa 1996 kwa mafunzo ya upiganaji yaani “makomando”. Wanawake hao walishindwa kufaulu katika mazoezi yao. Kumi na mmoja walijiondoa baada ya siku nne. Kati ya wanane waliobakia, watatu ndio walipewa nafasi ya kuanza mafunzo tena. Kwa maoni yetu, mafunzo hayo yalikuwa magumu kwa wanawake au yalihitaji nguvu nyingi na uvumilivu, masharti ambayo wanawake hawawezi kufikia tulikilinganisha na wanaume. Kwa misingi hii, jamii nyingi za Kiafrika na ulimwengu mzima zinachukulia shughuli za kijeshi kuwa hatari kwa wanawake kwa hivyo wanawake hushiriki tu katika nyanja zisizo hatari. Hivyo basi, suala la kutowahusisha wanawake katika shughuli za kijeshi katika *Mbali na Nyumbani* ni la kihistoria na kianthropolojia. Kwa misingi hii, mwandishi hakusudii kuwatenga wanawake katika mazingira hayo kwa kuwa kianthropolojia, maumbile ya wanawake hayakuwaruhusu kupigana.

4.6 Ukimya na Ucheleweshwaji katika shughuli za siasa

Ukimya wa wanawake katika siasa umejitokeza wazi katika *Mbali na Nyumbani*. Siasa kama tulivyoeleza awali hutekelezwa kuititia taasisi mbali mbali za kijamii. Kabla ya majilio ya wageni barani Afrika, Waafrika walikuwa na mifumo yao ya kisiasa ambayo iliongozwa kulingana na taratibu za jamii husika. Wakati wa ukoloni mifumo ya kisiasa ya Waafrika ilibadilika na uongozi ukatwaliwa na Wazungu. Kihistoria tangu majilio ya Wazungu mwaka wa 1895 hadi kufikia miaka ya hamsini, nchi za Afrika ziliwa katika harakati za kupigania uhuru. Waafrika walitumia njia na mbinu mbali mbali kudai uhuru wao. Baadhi ya nchi zilitumia mifumo ya mazungumzo kuititia vyama vya wafanyakazi. Vyama hivyo vilikuwa na malengo ya

kutetea haki za wafanyikazi kama tulivyotaja awali. Baadaye vyama vingi vya wafanyikazi vilibadilika na kuwa vyama vya kisiasa. Kwa mfano, nchini Kenya, Harry Thuku aliunda chama kilichoitwa *Young Kikuyu Association* (Y.K.A) mwaka wa 1921. Ward (1980:155) anasema kuwa Harry Thuku alifanya kazi katika serikali ya kikoloni kama mpokeaji na mtumaji wa ujumbe kwa njia ya simu. Aliungana na Waafrika waliofanya kazi katika mashamba ya Wazungu ili waweze kutetea haki zao za kikazi. Thuku alialika serikali ya kikoloni katika mazungumzo ili kujadili masuala ya wafanyikazi tarehe 24 Juni, 1921 kule Dagoreti. Thuku alitaka Waafrika wasilazimishwe kufanya kazi katika mashamba ya Wazungu, wasipunguziwe ujira wao, pawe na njia mwafaka ya usajili wa watu, kuanzishwe shule za kiserikali kando na zile za kimishenari na kuwapa Waafrika hati za kumiliki mashamba kama walivyowapa Wazungu. Chama hicho hakikuwasajili wanawake. Rosaldo (1974:7), anasema kwamba, wanaume walikuwa na nafasi nzuri ya kuunda vyama na taasisi za kisiasa na kujijenga kimamlaka kando na miktadha ya kinyumbani. Kwa kufanya hivyo, wao ndio walikuwa viongozi wa kisiasa au viongozi wa vyama vilivyopigania uhuru. Mfano mzuri ni Harry Thuku ambaye baada ya kujijenga kisiasa alikuwa Mwfrika wa kwanza kuwakilisha Waafrika katika mbuge la kikoloni (Legislative Council) mnamo mwaka wa 1944. Hata hivyo, Hornsby (2012) anaeleza kwamba, wanawake katika eneo la kati nchini Kenya waliunda chama cha kisiasa kilichoitwa *Mumbi Central Association* mwaka wa 1930. Hii ilikuwa baada ya *Kikuyu Central Association* kukataa kuwashirikisha wanawake kikamilifu katika masuala ya chama hicho. Mnamo mwaka wa 1933, vyama hivi viwili viliafikiana kuwa chama kimoja na kitengo cha wanawake kikafunguliwa. Wanawake walianza kujihusisha na masuala ya kupigania uhuru mwaka wa 1948, hasa shughuli ya kulisha watu kiapo. Baadhi ya wanawake ambao walishiriki katika shughuli za Mau Mau ni Rebbecca Njeri Kari na Wambui Wangarama. Jukumu lao kuu lilikuwa kuchunguza mienendo na mipango ya

Wazungu kisiri. Walikuwa kati ya maelfu ya wanawake walioshikwa na kuteswa na Wazungu. Baada ya Kenya kunyakua uhuru, wanawake walionekana kutohusika kisiasa kwa kuwa, ni wachache tu walikuwa wamepata elimu ya kikoloni. Nafasi zilizokuwepo zilihitaji watu waliosoma. Uundaji wa vyama vyta kisiasa ulihitaji elimu. Tulikwishataja kwamba, wanawake kihistoria walihuishwa na majukumu ya kinyumbani kutokana na masuala ya kianthropolojia. Kutokana na majukumu hayo, mazingira ya kinyumbani hayangewawezesha kuunda vyama vyta kisiasa na kujijenga jinsi wanaume walivyojijenga. Vinginevyo katika jamii za Kiafrika, siasa zilichukuliwa kama kazi chafu ambayo wanawake hawakukubaliwa kushiriki.

Obbo (1957:159) amechunguza hali za wanawake kisiasa katika eneo la Afrika Mashariki. Anasema kwamba, hadi kufikia miaka ya sabini, wanawake walichukulia siasa kuwa zoezi la kuchukiza hasa wale walikuwa wamesoma. Hili lilitokana na imani na itikadi kwamba, mwanamke kuzungumzia masuala ya kisiasa ni hatia, wacha hata kujihuisha kwao katika harakati za kisiasa. Walidhania kwamba kazi yao ilikuwa ni kuwaunga mkono wanaume. Wanawake ambao walijihuisha na siasa walichukuliwa kuwa wakora na wenye tabia mbaya. Uchukulizi huu uliwafanya wanawake kujitenga na siasa kwa hofu ya kuvunjiwa heshima na kutengwa na familia au jamii zao. Vile vile, ilikuwa vigumu kwa wanawake kuunda mashirika au vyama vyao kama wanaume kwa kuwa walijishughulisha na majukumu ya kimsingi kama kulea watoto, kupika, kutafuta kuni, kuchota maji na kufua nguo. Kwa mujibu wa Rosaldo (1974) kazi hizi ni za kurudiarudia, zinahitaji muda mrefu na ni za lazima. Wanawake huanza kutekeleza majukumu hayo pindi wanapoamka hadi usiku. Kwa misingi hii wanawake hawakuwa na muda wa kukutana na wenzao kwa shughuli za kisiasa kama wanaume ambao wangekutania nje ya miktadha ya kinyumbani. Japo wanawake walianza kuunda vyama vidogo

vidogo vya kuwaunganisha tangu miaka ya hamsini wanasiasa walianza kuvitumia ili kuendesha shughuli zao za kisiasi. Kwa mfano, nchini Ghana kufikia mwaka wa 1957 wanawake kama Mabel Dove, Ruth Botsio, Ama Nkurumah, Ramatu Baba, Sophia Doku na Daktari Evelyn Amarteifo walikuwa waandalizi wakuu na waandishi wa habari za kisiasi. Walichangia pakubwa kuwaingiza wanawake wa matabaka mbali mbali katika chama cha wanawake cha kitaifa cha Ghana. Ziporah Kittony ni mwanasiasa ambaye tunaweza kudai anashadidia ukweli kwamba, sababu ya utokuwepo wa wanawake katika mazingira ya kisiasi katika *Mbali na Nyumbani* unatokana na kucheleweshwa kwao katika elimu. Ziporah alipata elimu miaka ya hasmsini na akaajiriwa kama mwalimu miaka ya sitini. Aliacha kazi ya ualimu mwaka wa 1964 na kuanza kampeni za upangaji uzazi huko Kericho. Alishirikiana na Shirika ya Maendeleo ya vijana ulimwenguni kufanya utafiti ili kuwashamasisha vijana juu wa nidhamu na mbinu za kujitegemea. Utafiti huu ilimfungulia njia ya kusafiri hadi Mexico kuhudhuria mkutano wa wanawake ulimwenguni mwaka wa 1975. Kutangamana kwake na wanawake kutoka maeneo mbali mbali ya ulimwengu kulimpa mtazamo mpya kuhusu elimu, siasa na uchumi miongoni mwa mengine. Ziporah alikuwa mwanamke Mwaafrika wa kwanza kuandaa maonyesho ya kilimo kule Eldoret baada ya kuchaguliwa kama mwenyekiti wa maonyesho ya kilimo nchini Kenya. Alijiunga na chama cha Maendeleo ya wanawake mwaka wa 1980 na kuchaguliwa mwenyekiti kwa muda wa miaka kumi na mitatu. Mnamo mwaka wa 1996 alichaguliwa mwenyekiti wa kitaifa wa chama hicho na kufanya kazi hadi mwaka wa 2005. Kupitia chama hicho Ziporah aliweza kujijenga kisiasi hasa wakati Chama cha Wanawake kiliungana rasmi na chama cha kisiasi K.A.N.U wakati wa utawala wa Moi. Ingawa lengo kuu la Chama cha Maendeleo ya Wanawake lilikuwa kuimarisha na kuboresha maisha ya wanawake kijamii, kiuchumi na kisiasi, kilitazamwa na Wakenya wengi zaidi kwa jicho la kisiasi kuliko kimaendeleo. Baadaye tarehe 5, Desemba,

1991 Moi aliwataka waache kujihusisha na masuala ya kisiasa ili wazingatie maendeleo yao. Japokuwa hiki kiliitwa Chama cha Maendeleo ya Wanawake, Moi na wanasiasa wenzake walikitumia zaidi katika kampeni za kisiasa. Wanawake hawakupata nafasi ya kujijenga kama wanaume walivyojijenga. Hata hivyo, baadhi ya viongozi wa chama hicho walipata umaarufu kisiasa kupitia kampeni zilizoendeshwa katika mashirika ya kina mama mikoani, wilayani, tarafani na katika lokesheni. Wanawake hao walikuwa wameelimika na ndio walipata nafasi ya kuongoza vyama hivyo. Mfano mzuri ni Ziporah Kittony ambaye hapo baadaye, aliteuliwa kama seneta wa Jimbo la Transnzoia. Mifano hii inathibitisha kwamba, mazingira ya kisiasa yaliwahuisha wanawake kwa njia ya kiusaidizi tu. Hata hivyo, baadhi ya wanawake ambao walikuwa viongozi wa chama hiki waliweza kujijenga na kuwania nyadhifa za kisiasa. Tukiangalia baadhi ya wanawake wengine nchini Kenya ambao walijihuisha na siasa, tunaona kwamba elimu ndiyo iliwawzesha kuwania nyadhifa za uongozi. Hao ni pamoja na Daktari Julia Ojiambo, Grace Ogot na Martha Karua.

Suala la elimu linajitokeza wazi katika ukimya wa wanawake katika miktadha ya kisiasa. Tukichukua mfano wa Thuku, yeye alikuwa amepata elimu ya kikoloni ambayo ilimpa fursa ya kufanya kazi. Kupitia elimu hii, Thuku alikuwa ametambua umuhimu wa kupigania uhuru kupitia uundaji wa vyama vya wafanyakazi ambavyo vingetumika kama kifaa cha kuzungumza na wakoloni. Ujuzi wa kikazi aliokuwa nao pia ungemwezesha kutuma na kupokea ujumbe kutoka kwa serikali ya kikoloni. Ucheleweshwaji wa elimu ya wanawake basi ulichangia ukimya wao katika shughuli za kisiasa. Wanaume waliopata elimu ya Kimagharibi walikuwa na uwezo mkubwa kuunda vyama pamoja na tajriba ya kuongoza vyama hivyo. Kwa misingi hii viongozi waliotajwa katika *Mbali na Nyumbani* kama vile, Jomo Kenyatta, Oginga Odinga, Dennis

Okumu, Tom Mboya, Ben Opar Mboya, Dokta Banda, Amilca Cabral, Ben Bella, Edward Mondalene, Augustino Neto, Patrice Lumumba, Kwame Nkurumah walikuwa tayari wamepata elimu ya Kikoloni. Kwa misingi hii sababu za utokuwepo wa wanawake katika mazingira ya kisiasa katika *Mbali na Nyumbani* ni ucheleweshwaji wa elimu na itikadi kwamba siasa ni zoezi chafu ambalo linaweza kumvunzia mwanamke heshima katika jamii. Hii ndio maana hata sasa wanawake wengi huchukulia siasa kuwa zoezi chafu.

Wapiganiaji uhuru katika muktadha wa kisiasa katika *Mbali na Nyumbani* ni kama Dedan Kimathi kiongozi wa Mau Mau, vijana waliopewa mafunzo ya kijeshi Kairo na wanamgambo Ujerumani. Shafi na wenzake walipata mafunzo ya kijeshi baada ya kuhamia Kairo. Wanamgambo katika uwanja wa chuo cha Bernau, pia walikuwa wahamiaji. Tumeshaona kwamba kule Kairo mwandishi na wenzake wanane walifunzwa kutumia vilipuzi na mabomu. Kwingineko, huko Ujerumani, vijana waliokuwa katika uwanja wa Chuo cha Bernau walikuwa wakipewa mafunzo ya kijeshi ili wakirejea nyumbani kwo wapiganie uhuru wao. Katika miktadha hii, hakuna wahusika wa kike. Utokuwepo wao ni uhalisia kwamba, wanawake hawakuhusishwa na uhamaji na uhamiaji kwa shughuli za kivita kwa kuwa katika muktadha wa upiganiaji uhuru katika nchi za Afrika kama vile Kenya, wanawake walianza kujihusisha na mapigano mwaka wa 1948 zoezi lililoendelea hadi mwaka wa 1959, Hornsby (2012). Tunaweza kudai kwamba, wanawake hawakutengwa katika mazingira ya upiganiaji uhuru ila hawakuhusishwa katika uhamaji na uhamiaji kwa shughuli za kupigania uhuru, hazikuwashirikisha.

4.7 Ukimya na ucheleweshwaji katika masuala ya dini

Dini kama tulivyoeleza ni mfumo wa imani ya watu na njia ya kuabudu, kusali, kuheshimu au kumtii muumba wao. Ni muhimu kutaja kwamba, kabla ya Uislamu na Ukristo kuenezwa barani Afrika, kulikuwa na dini za Kiafrika zilizojengwa kwa misingi ya mila na desturi za jamii. Ibada ziliendeshwa mahali maalumu palipotengwa na palipochukuliwa kuwa patakatifu. Sherehe za kidini pia zilikuwepo. Katika jamii nyingi za Kiafrika kiongozi wa jamii ndiye pia alikuwa kiongozi wa kidini. Alipewa majukumu kama vile kuongoza jamii, kutoa amri za kivita , kuamua kesi na kupeana mashamba kama vile *Orkoiyot* wa Wakalenjin na *Oloibon* wa Wamasai.Ilikuwa nadra kupata viongozi wa kidini ambao ni wanawake. Baada ya kuenezwa kwa Uislamu na Ukristo mabadiliko mengi yalitokea katika mifumo ya kidini. Taratibu, mipangilio na taasisi za kijamii, kiuchumi, kisiasa na kidini ziliathiriwa pakubwa. Athari hizo zimeendelea kuonekana katika dini za kilimwengu.

Katika *Mbali na Nyumbani*, dini ya Kiislamu imejitokeza katika mazingira ya misikiti. Viongozi wa kidini kama mashehe na maimamu wamehusishwa na jukumu la kuongoza ibada. Baadhi ya wafuasi wa dini ya Kiislamu wamerejelewa kwa majina kama Maalim na wengine Bwana. Mashehe ni wataalamu wa dini. Katika Uislamu, wapo wanawake wengi Masheihe. Jukumu kuu la maimamu ni kuongoza watu kusali. Kulingana na imani katika dini hii, mwanamke anaweza kuswalisha ila kama pana mwanamume anayejua kuswalisha mwanamke hakubaliwi kuongoza sala. Iwapo mwanamke ataswalisha, anasimama mstari mmoja na wale anaowaswalisha yaani hasimami mbele yao kama imamu mwanamume asimamavyo. Tumeshasema kwamba, jukumu kuu la imamu ni kuswalisha. Hili ni jukumu analolifanya mara nyingi kila siku. Katika dini ya Kiislamu, mwanamke haruhusiwi kuswali akiwa na hedhi. Wanawake hushiriki katika sherehe

za mazishi na ikiwa aliyeaga ni mume au mwana wa kiume au ndugu wa kiume mke ndiye huwaosha. Wanawake wanaruhusiwa kwenda kaburini na hakuna sheria ya kidini hata moja inayowafungia kufika kaburini wakati wa kuzika ila hawaruhusiwi kuchanganyika na wanaume. Katika *Mbali na Nyumbani* tumeona kwamba Shafi alipewa heshima ya kuingia kaburini kumlaza mjomba wake kwenye mwanandani. Hii ni sheria ya kidini. Mwanamume ndiye hukubaliwa kutekeleza jukumu hili. Tumeona pia kwamba, wanawake hawajahusishwa katika shughuli hiyo ya kuzika. Shughuli nyingine za kidini ni kama kujenga misikiti na sherehe kama ile ya ‘*usiku wa dhikiri ya tarika ya shadhili*’ ambayo mwandishi na wenzake walishiriki. Katika sherehe hii, Waislamu hukesha wakikumbuka wema wa Mwenyezi Mungu kwa kutaja jina lake. Vile vile safari ya kwenda Makka kuhiji imejitokeza. Mwandishi anakutana na Ame katika meli ya *M.V.Ubena* akiwa safarini kwenda Makka kuhiji. Mzee Manoti pia anakwenda Makka kwa Hijja (uk 62) Katika sherehe ya kidini ilioandalowi kiamboni mwa Mzee Muhanji Msuo, kule Kampala, wanawake wamehusishwa na maandalizi ya chakula tu. Uhusishwaji huu unaelezeka kianthropolojia kwamba, katika dini ya Kiislamu wanawake wana majukumu tofauti na yale ya wanaume katika sherehe za kidini. Hata hivyo, Robbins (2000:220) anatahadharisha kwamba, katika kazi ya kifasihi uwasilishwaji wa wanawake waweza kuonyesha kutengwa kwao, kupewa nafasi finyu au majukumu yanayofikiriwa kuwadunisha. Anasema kwamba, kutokuwepo kwa wahusika wa kike, kutosawiriwa kwao kama wahusika wakuu, kutopewa usawa katika masuala ya kijamii, kiuchumi, kidini na kitamaduni haina maana kuwa katika hadithi inayohusu wanaume, wanawake hawahusiki. Anadai kuwa, tunajifunza mengi kuhusiana na wanaume katika utamaduni fulani, kipindi maalumu cha kihistoria kwa kuwa hivyo ndivyo hadithi yenyewe inavyowasilishwa. Kwa misingi hii, katika *Mbali na Nyumbani* kuhusishwa kwa wanawake katika muktadha wa upishi nao wanaume wakihuhsishwa na mazungumzo ya kidini na

ibada haina maana kuwa mwandishi amewadunisha au kuwatenga. Tumeweza kufahamu kwamba, katika dini ya Kiislamu wanawake wana majukumu tofauti na yale ya wanaume. Kwa mfano, katika msikiti wa Ijumaa kule Kampala sala iliongozwa na imamu mwanamume. Wanaume waliohudhuria sherehe kiamboni mwa Muhanji Msuo walikuwa wataalamu na walimu wa dini kwa hivyo wanawake hawangeweza kupewa nafasi ya kuongoza sherehe hii ya kidini kutokana na sheria na imani katika dini hii kwamba, pakiwepo na mwanamume ajuaye kuongoza basi mwanamke hapaswi kuongoza ibada. Majukumu ya kidini ya wanaume na yale ya wanawake yamejitokeza katika *Mbali na Nyumbani*.

Miller (1990:265-267) amechanganua mawazo ya Jamin, kuhusu ukimya kama mkakati mbadala wa utokuwepo na anasema kwamba, katika jamii nyingi za Kiafrika, kujifunza kuzungumza huenda sambamba na kujifunza kuwa kimya. Wakati wa kuzungumza na wakati wa ukimya huwekewa mpaka kimuktadha. Uzungumzaji basi hutegemea ukimya kiasi kwamba walio na mamlaka watawategemea wasio na mamlaka kwa hivyo, ukimya haufai kuchukuliwa kama kudhalilishwa, kutengwa au kuonewa. Kwa misingi hii, ukimya wa wanawake katika miktadha ya kidini katika *Mbali na Nyumbani* sio kutengwa. Kwa maoni yetu, japo wanawake wa Kibaganda hawazungumzi, majukumu wanayotekeleza ndiyo yanayofanikisha sherehe yenewe. Matayarisho na maandalizi ya upishi mchana kutwa usiku kucha yamewashirikisha katika sherehe hiyo kwa kiasi kikubwa. Sababu ya utokuwepo wa wanawake katika mazungumzo ya kidini waweza kuelezwa kama unaotokana na itikadi na imani za dini ya Kiislamu ambazo zilikubaliwa na kuenziwa na wafuasi wake. Ukimya wa wanawake katika muktadha wa dini ya Kiislamu katika *Mbali na Nyumbani* ni uhalsia kianthropolojia kwamba, majukumu ya wanawake katika dini ya Kiislamu ni tofauti na yale ya wanaume. Kwa misingi hii utokuwepo

wa wanawake katika mazungumzo ya kidini na kutohusishwa kwao katika shughuli ya kutia maiti kwenye mwanandani katika sherehe ya mazishi ni uhalisi wa mambo bali sio kutengwa kwao katika dini.

Kwa upande wa dini za kienyeji, Wabukusu wamehusishwa na *Dini ya Msambwa*. Tunaelezwa kwamba, kiongozi wao Elijah Masinde aliishi katika kilele cha Mlima Elgon. Tumeona kwamba, Wabukusu walikuwa wametangaza vita dhidi ya wakoloni na waliamini kwamba, ukombozi ungetoka kileleni cha Mlima Elgon mahali alipoishi Elijah Masinde. Katika mazingira na miktadha yote ya dini hizi mbili, tumeona kwamba, wanawake hawajahusishwa kama viongozi wa kidini. Sababu za utokuwepo wa viongozi wa dini wa kike katika *Mbali na Nyumbani* ni ukimya ambao unaelezeka kianthropolojia. Kwamba mila, desturi na itikadi za dini katika jamii ziliwaruhusu wanawake kutekeleza majukumu tofauti na yale ya wanaume. Kwa misingi hii, mwandishi katika *Mbali na Nyumbani* amewawasilisha wanawake kihalsia na kihistoria katika mazingira na miktadha ya dini, na haiwezi kutathminiwa kuwa amewatenga katika shughuli za kidini.

Tukichunguza dini ya Kikristo ambayo inaongozwa na mafundisho ya Biblia tunaona kwamba, katika agano la kale na agano jipya, wapo wanawake wanaohusishwa na shughuli za kidini. Kwa mfano, katika kitabu cha (Kutoka 15: 20-21), tunaeleza kwamba, Miriamu dadake Aroni na Mose, aliwaongoza wana wa Israeli katika ibada ya kumshukuru Mungu baada ya kuvuka bahari ya Shamu na wanawake wote wakamfuata wakiimba. Vile vile mwanamke mwingine aliyekuwa kiongozi wa kidini ni Debora. Katika kitabu cha (Waamuzi 4: 1-5), tunaelezwa kwamba Debora alikuwa muamuzi na amiri jeshi mkuu kwa miaka arobaini. Wengineo ni Huldah, ambaye

alikuwa nabii, (Waamuzi 22:14) Mhubiri Filipo alikuwa na mabinti wanne ambao walikuwa manabii na wahubiri, (Matendo ya Mitume 21:8) Hata hivyo, wanaume ambao walikuwa viongozi wa kidini katika biblia walikuwa wengi kuliko wanawake. Japo viongozi wa kike wamewasilishwa kwa ufinyu katika biblia, inafaa ikumbukwe kwamba, dini ya ukristo imeundwa kwa mila na tamaduni za Wayahudi na katika kuchunguza ni muhimu mila na desturi hizo zitiliwe maanani. Maendeleo ya wanawake katika dini ya Ukristo yanaonekana kihistoria. Kuna wanawake wengi ambao ni viongozi wa makanisa na hata wengine ambao wameanzisha madhehebu yao. Katika miaka ya sabini ilikuwa nadra kupata wanawake ambao ni wachungaji wa makanisa au wenye vyeo katika makanisa. Kwa mfano, *Church of England* waasisi wa dhehebu la kianglikana walipinga vikali kutawazwa kwa wanawake kama makasisi au maaskofu hadi kufikia mwaka wa 1994. Dhehebu la kianglikana hapa nchini Kenya lilipitisha sheria ya kuwatawaza wanawake kama makasisi mwaka wa 1980 na kasisi wa kwanza mwanamke katika dhehebu hilo, Lucia Okuthe akatawazwa mwaka wa 1983. Wanaamini kwamba, injili ni ya wote waliobatizwa pasi kubagua jinsia. Hata hivyo, katika katiba yao Kifungu cha VI, kipengele cha 4, kinasema kwamba lazima Askofu awe mwanaume huku kipengele cha 5 kikisema kasisi anaweza kuwa mwanamume au mwanamke. Baada ya katiba mpya ya Kenya kuidhinishwa mwaka wa 2010, baadhi ya makanisa yamepuuza sheria hii na kukubali kutawazwa kwa wanawake kama maaskofu kama vile, dayosisi ya Eldoret mwaka wa 2013 na ile ya Maseno mwaka wa 2014. Wametambua kwamba, katiba imefungua nafasi zote katika taasisi zote kuwaniwa na jinsia zote na wanawake wakifungiwa wanaweza kushtaki kanisa. Kwa maoni yetu, katika *Mbali na Nyumbani*, wanawake wamewasilishwa kihalisia bali sio kudhalilishwa au kutengwa.

4.8 Ubanifu wa uhamaji na uhamiaji

Uhamaji kama tulivyoeleza awali ni hali ya mtu au watu kuondoka mahali na kwenda kuishi mahali pengine. Uhamaji ni zoezi linafanywa na watu kila wakati katika maisha yao. Kuhama kunaweza kuchochewa na shughuli za kiuchumi, kielimu, kisiasa au hata kivita. Wakenya wengi huhama kutoka mashambani na kwenda kuishi mijini ambapo watapata elimu bora, ulinzi mzuri, maji safi na hata kazi bora. Uhamiaji nao tulisema ni hali ya mtu au watu kuondoka nchi yao na kuingia nchi ngeni kwa madhumuni hayo hayo tuliyotaja ya uhamaji. Katika sura ya tatu, tulieleza shughuli zinazochochea uhamaji na uhamiaji kama vile, kupata elimu, kutafuta kazi, kupokea mafunzo ya kijeshi, kupigania uhuru mionganii mwa nyingine. Tumeona kwamba, katika *Mbali na Nyumbani*, shughuli hizo za kuhama na kuhamia nchi ngeni, hazikuhusisha wanawake. Sababu kuu ya utokuwepo wa wanawake katika shughuli za kuhamia nchi ngeni ni ubanifu uliokuwepo wa wanawake katika shughuli za kielimu, kivita, kisiasa na kidini. Obbo (1957:87) katika ‘*Town Migration is not for Women*’ anasema kwamba, kuibuka kwa miji wakati wa ukoloni kulileta mabadiliko mengi katika jamii za Kiafrika. Katika kazi yake anasema kwamba wanawake wa Kibaganda hawakuruhusiwa kuhamia mijini na wale walifanya hivyo walichukuliwa kuwa malaya na kuishia kutengwa kijamii. Walichukuliwa kama waliokiuka mila na desturi za jamii. Itikadi hii ilikuwepo katika jamii nyingi za Kiafrika. Illichukuliwa kwamba, wanaume ndio vitega uchumi na mihimili katika familia. Wao ndio walihamia mijini kutafuta vibarua. Wanawake wangebaki mashambani wakinanza watoto kwa kuwa wao walichukuliwa kuwa vitegemezi vyta wanaume. Baada ya kuingia mijini, wanaume walipata nafasi za kuijendeleza kielimu au kuanzisha biashara ndogo ndogo.

Uhamiaji unaotokea katika *Mbali na Nyumbani* unafanywa kwa lengo la kupata elimu na kupata mafunzo ya kijeshi kwa nia ya kukomboa nchi zilizokuwa chini ya ukoloni. Shafi aliamua kuhamza Zanzibar kwenda Ulaya kusoma baada ya kuchochewa na rafiki yake Mohammed Khamisi Nura aliyezua ametangulia kwenda London. Katika uhamiaji na uhamiaji, Shafi anaandamana na vijana wenzake. Katika mazingira na miktadha yote ya uhamiaji na uhamiaji, kwa shughuli za kielimu na kijeshi, hakuna wanawake. Mwanamke wa pekee aliyezamia Khartoum kwa shughuli za kielimu ni Zainabu. Hii inaonyesha kwamba, ubanifu wa wanawake katika uhamiaji na uhamiaji ulichangia kucheleweshwa kwao kielimu. Katika miktadha ya mafunzo ya kijeshi nje ya Afrika, hakuna mwanamke hata mmoja. Abdalla na Shabaani wanahamia Cuba na Urusi ili kupata mafunzo zaidi ya kijeshi. Ubanifu wa wanawake katika uhamiaji kwa shughuli za kijeshi ndio sababu kuu ya utokuwepo wao katika mazingira ya uhamiaji. Kutopata mafunzo ya juu katika jeshi kulichangia kucheleweshwa kwa wanawake katika shughuli za kijeshi. Kwa ujumla, kihistoria wanawake hawakushirikishwa katika uhamiaji na uhamiaji kwa shughuli za kielimu, kijeshi na kiuchumi. Hii ndio maana tuliona kwamba, wanawake waliokuwa wakisafiri katika treni, mabasi au meli walikuwa wakihama kwa shughuli za kinyumbani.

4.9 Hitimisho

Katika sura hii, tumeona ya kwamba, uwepo finyu wa wanawake katika mazingira ya kielimu unatokana na ucheleweshwaji wa elimu ya kikoloni kwa wanawake katika jamii ya Waswahili. Ucheleweshwaji huu ulichangiwa na utamaduni pamoja na taratibu za kijamii ambazo zinaelezeka kianthropolojia kwa njia chanya. Tumeona kwamba, utokuwepo wa wanawake katika mazingira ya kijeshi ni ukimya unaotokana na masuala ya kianthropolojia na kihistoria.

Kwamba jamii za ulimwengu hufikiri kuwa shughuli za kivita ni hatari kwa wanawake, zinahitaji nguvu nyingi na uvumilivu mwingi. Kwa jamii nyingi hizi ni shughuli za wanaume. Tumeona kwamba, kutohusika kwa wanawake katika shughuli fulani za kidini ni ukimya kianthropolojia. Kwamba wanawake walihusishwa katika masuala fulani ya kidini na kutohusishwa na masuala mengine. Kwa misingi hii, ukimya wa wanawake katika dini ni uhalisi kianthropolojia. Uhamaji na uhamiaji uliwabana wanawake na ubanifu huu umechangia ucheleweshwaji wao katika miktadha ya elimu ya juu, shughuli za kisiasa na kijeshi kama zinazyojitokeza sasa.

SURA YA TANO

MAHITIMISHO

5.0 Utangulizi

Utafiti huu ulikuwa na madhumuni ya kuchunguza sababu za kuwepo na kutokuwepo kwa wahusika wa kike katika *Mbali na Nyumbani*. Tuliazimia kubainisha uwepo wa wahusika wa kike katika mazingira na miktadha mbali mbali kimajukumu. Tuliazimia pia kubainisha kuwepo kwao finyu katika mazingira na miktadha fulani na kutokuwepo kwao kabisa katika mazingira na miktadha mingine. Tumegundua kwamba, wanawake wamewasilishwa zaidi katika mazingira ya kijamii na majukumu wanayotekeleza ni yale ya kinyumbani. Tumefahamu pia kwamba, wanawake wamewasilishwa kwa ufinyu katika mazingira na miktadha ya kielimu, kidini, kiuchumi na kisiasa kutokana na ucheleweshwaji kushirikishwa au kuhusishwa katika harakati za kijamii. Utafiti huu umeonyesha kwamba, katika mazingira na miktadha ya kijeshi wanawake hawapo kabisa. Kutokuwepo kwao kunafasiriwa kuwa ukimya, ukimya amba ni chanya kwani umetokana na mila, desturi, itikadi na mipangilio ya kijamii kipindi hicho cha kihistoria cha mwandishi. Ukimya huu unaakisi ukweli wa maisha ya wanawake. Tumeng'amuwa kwamba, sababu za kuwepo na kutokuwepo kwa wahusika wa kike katika *Mbali na Nyumbani* ni za kianthropolojia na kihistoria.

5.1 Matokeo

Katika sura ya pili, tumewabainisha wahusika wa kike katika *Mbali na Nyumbani*. Wahusika wa kike wamewasilishwa katika mazingira ya kijamii, kiuchumi, katika safari, kielimu na kiburudani. Uwasilishwaji wao kimajukumu umeonyesha kwamba, katika mazingira ya kijamii kama muktadha wa kinyumbani na safari, mwanamke ana majukumu ya uzazi, ulezi, upishi na

upambaji nyumba. Katika mazingira ya kiuchumi kama katika muktadha wa kikazi na kibiashara, utafiti huu umegundua kwamba, wanawake wamewasilishwa kwa ufinyu na wamepewa majukumu ya kiusaidizi huku wanaume wakipewa majukumu makuu. Katika mazingira ya kielimu, tumegundua kwamba, pana ukimya wa wanawake katika elimu ya msingi na sekondari. Vile vile, wanawake wamehusishwa kwa ufinyu katika taasisi za juu za elimu kama katika vyuo vikuu.

Katika sura ya tatu, tumbainisha utokuwepo wa wanawake katika mazingira ya kijeshi, kisiasa, kidini na yale ya uhamaji na uhamiaji. Tumegundua kwamba, katika *Mbali na Nyumbani*, wanawake hawajahusishwa kabisa katika mazingira na miktadha yote ya kijeshi, kisiasa na uhamaji na uhamiaji kwa shughuli za kikazi au kielimu. Vile vile, tumbaini kwamba, katika dini za kiislamu na ya kienyeji, wanawake hawajahusishwa kama viongozi wa kidini kama vile mashehe na maimamu au walimu wa dini katika miktadha yote ya kidini. Tumeona kwamba, wanawake wana jukumu muhimu la maandalizi ya sherehe za kidini kama maulidi na mazishi mionganoni mwa mengine.

Katika sura ya nne, tumejadili sababu za uwepo na utokuwepo wa wahusika wa kike katika *Mbali na Nyumbani*. Tumeona kwamba, uwepo finyu wa wanawake katika mazingira ya kielimu umetokana na ucheleweshwaji wao katika taasisi za kielimu. Ucheleweshaji huu unatokana na itikadi, taratibu na mipangilio ya mifumo ya kijamii. Ni dhahiri kwamba, kihistoria elimu kimagharibi haikuhusishwa na wanawake. Kucheleweshwa kwa wanawake katika elimu ya msingi na ya sekondari, kuliwabana katika uhamaji na uhamiaji kwa shughuli za kielimu na kikazi. Tumegundua kwamba, ukimya wa wanawake katika mazingira ya kijeshi umesababishwa

na itikadi kwamba, jamii za kilimwengu zinaamini kwamba, maumbile ya mwanamke pamoja na majukumu yake ya uzazi hayamruhusu kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijeshi. Wanawake walianza kuhusishwa katika shughuli za kijeshi miaka ya sabini japo hawakupewa jukumu la kupigana. Utafiti umegundua kwamba, ucheleweshwaji wa wanawake katika elimu ulichangia pakubwa ukimya wao katika mazingira ya kisiasa. Wanaume walipata nafasi ya kuunda na kujiunga na vyama vya kisiasa mapema zaidi kuliko wanawake. Majukumu ya wanawake ya kinyumbani na hali zao ni mambo yaliyochangia wasiweze kuunda vyama ambavyo vingewawezesha kujijenga kisiasa. Fauka ya hayo, siasa zilihusishwa na wanaume huku wanawake wakiwa wasaidizi wao. Itikadi iliyokuwepo wakati huo ni kwamba, mwanamke angejivunja heshima yake katika jamii iwapo angejihuisha na siasa. Ukimya wa wanawake katika mazingira ya kidini umeelezeka kianthropolojia kwamba, imani na itikadi za kidini hufungamana na mila na desturi za kijamii. Wanawake wana majukumu tofauti na wanaume katika dini ya Kiislamu kwa hivyo, kutohusika kwao katika miktadha fulani sio kutengwa bali ni uhalisi wa kihistoria.

5.2 Mapendekezo

Kulingana na upeo na mipaka tulijojiwekea katika utafiti huu, tulijibana katika suala la kuwepo na kutokuwepo kwa wahusika wa kike katika *Mbali na Nyumbani* kwa kutumia vipengele vyatadharia ya anthropolojia vyatadhelweshwaji na ukimya. Ni matarajio yetu kwamba, kazi hii itawachochea watafiti wa baadaye katika kuchunguza upya tathmini ambazo utafiti huu umedai kuwa zimehitimishwa kihisia au kwa chukulizi fulani. Kwa kutafiti upya kazi hizo, watawezeza kutoa tathmni chanya kuhusu wanawake. Tunapendekeza pia watafiti wa baadaye watathmini mbinu za waandishi wa tawasifu za awali na zile zinazotumiwa na waandishi wa sasa katika fasihi ya Kiswahili.

MAREJELEO

Amadiume, I. (1987) *Male Daughters, Female Husbands*.London: Zed Books.

Bâ, M. (1980) *Barua Ndefu Kama Hii* (Kilichotafsiriwa na Maganga, C, 1994) Nairobi : Focus Publications Limited.

Bertонcini, E.Z (1989) *Outline of Swahili Literature: Prose Fiction and Drama*. E.J. Brill: Leiden.

Bressler, C. E. (2003) *Literary Criticism: An Introduction to Theory and Practice*. (Third Edition), New Jersey: Prentice Hall.

Cara, E. Richards (1976) *People in Perspective:An Introduction to Cultural Anthropology*. Randsom House: New York.

Carolline B. Bretell na Carolyn F.Sargent (1993) *Gender in Cross Cultural Perspective*, *Englewood Cliffs*. New Jersey: A Simon and Schister Company.

D'Ann Campell (1993) "Women in Combat: The World War Two Experience in the U.S, Great Britain, German, and the Soviet Union" *Journal of Military History*.April 1993 Vol. 57 pp 301-323

Deckard na Barbara Sinclair (1979) *The Womens Movement: Political Socio economic and Psychological Issues*. New York : Harper & Row.

Dyhouse Mc. Williams (1995) *No Distinction of Sex: Women in British Universities 1870- 1970*. New York : Routledge.

Ember, C.R., na Ember, M. (2009). *Cross Cultural Research Methods*. Lahham : Atlamira Press.

Harris, Marvin (1968) *The Rise of Anthropological Theory: A History of Themes of Culture*. New York : Crowell.

Hartfield A. (2005) “The Women’s Auxillary Corps”, *Journal of the Society for Army Historical Research*, 83, no. 335 pp 243-254.

Hommes, N.J., (1969) “Let Women Be Silent In Church”*Calvin Theological Journal*, vol.4, 5-22

Hornsby (2012) Kenya: *A History since Independence*.London/New York : I . B Tauris.

Karoki, E. (2014) *Suala la Uhamaji na Uhamiaji kama linavyoendelezwa katika “Mbali na Nyumbani’ ya Adam Shafi*.Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Katola, E. (2006); *Udhalimu dhidi ya Wahusika wa Kike*.Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Kisiroche, R. (2008) *Sauti ya Mwanamke Dhidi ya Ubabedume katika Tamthilia za Kiswahili*. Tasnifu ya M. A. Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Lebeuf, M.D (1963) “*The Role of Women in the Political Organizations of African Societies*”.In Paulme (ed)

Little, Kenneth (1973) *Women in Towns*.Cambridge:Cambridge University Press.

Lugano, R. (1989) *Mwanamke katika Riwaya za Kezilahabi* .Tasnifu ya M.A (Haijachapishwa)

Malinowski (1965) *Methods of Study of Culture Contact in Africa*.International African Institute: Oxford University Press.

Madumulla, J.S (2009) *Riwaya ya Kiswahili*.Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Mbughuni, P. (1982) “*The Image of Woman in Kiswahili Prose Fiction*” *Kiswahili Juzuu 49/2*. Tuki : Dar es Salaam.

Miller, C. (1990) *Theories of Africans*. New York : Routledge.

Momanyi, C. (1998) *Usawiri wa Mwanamke Mwislamu katika Jamii ya Waswahili kama inavyobainika Katika Ushairi wa Kiswahili*. Tasnifu ya Ph.D. Chuo Kikuu Cha Kenyatta (Haijachapishwa)

Moore, Henrietta L. (1988) *Feminism and Anthropology*. Cambridge:U.K, Polity Press.

Mulila, J. (2009) *Usawiri Chanya wa Wahusika Wanawake*.Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Njogu, K na Chimera, R.M. (2007) ; *Nadharia ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi : J.K.F.

Nwabara, E.N (1977) *A Century of Contact with Britain 1860-1960*.Hodder and Stoughton.

Nyaosi, K. (2008) *Taswira ya Asasi ya Ndoa katika Riwaya za Kiu na Msimu wa Vipepeo*.Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu Cha Nairobi.(Haijachapishwa)

Obbo, C. (1957) *African Women, Their Struggle for Economic Independence*. London : Zed Press.

Ominde, H.S (1952) *The Luo Girl from Infancy to Marriage*. Nairobi : MacMillan Publishers.

Onyoni, J. (2012) *Usawiri wa wahusika wanawake katika Tamthilia za Natala na Mama ee*. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Rita J, Simons (2007) *Womens Roles and Statuses, the World over*. Lexington : Lexington Books.

Robbins, R. (2000) *Literary Feminism*.New York : Palgrave.

Rosaldo na Wengine (1974) *Woman, Culture, and Society*. California: Stanford University Press.

Skaine, R. (1999) *Women at War: Gender Issues of Americans in Combat*.Farland: Mc Farland.

Tullberg, G. (1998) *Women at Cambridge*. Cambridge : Cambridge University Press.

Saskia, W. (1995) *Subversive Women: Historical Experiences of Gender and Resistance*.London and New Jersey : Zed Books Limited.

Shaaban, R. (1966) *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini*.Nairobi: Thomas Nelson & Sons Limited.

Shafi, A. (1978) *Kasri ya Mwinyi Fuad*.Nairobi:Vide – Muwa Publishers.

____ (1979) *Kuli*. Nairobi: Longmann Publishers Limited

____ (2003) *Haini*. Nairobi: Longhorn Publishers Limited.

_____ (2013) *Mbali na Nyumbani*. Nairobi : Longhorn Publishers Limited.

Sirucha, B. (1986) *Hadhi na Hali ya Mwanamke katika riwaya za S.A. Mohammed*.Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Sullerot, E. (1971) *Woman, Society and Change*. London : World University Library.

Swaleh, A. (2011) *A Critique of the Mapping and Construction of Gender Identity and Authority in selected Kiswahili Novels* Ph.D. Thesis University of Nairobi (Haijachapishwa)

Wallace, A. (1972) *Religion : An Anthropological View*.New York : Random House.

Wamitila, K.W (2008) *Kanzi ya Fasihi 1:Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi : Vide-Muwa Publishers Limited.

Ward, W.E.F (1963) *A History of Africa, Book Two, Egypt and the Sudan.Uganda. Kenya. Tanzania*. New Edition. London: George Allen & Unwin Ltd

White (1963) *The Ethography and Ethnology of Franz Boas*. Texas : University of Texas.

Winthrop, R. H. (1991) *Dictionary of Concepts in Cultural Anthropology*. New York: Greenwood Press.